# Nyumba ya Haki ya Ulimwengu



## MAKUSANYO YALIYOANDALIWA NA IDARA YA UTAFITI

Februari, 2021

# Nyumba ya Haki ya Ulimwengu

## MAKUSANYO YALIYOANDALIWA NA IDARA YA UTAFITI

Februari, 2021

*Kijitabu hiki kimeandaliwa maalum kwa ajili ya Maadhimisho*

*ya Miaka Mia Moja ya Kupaa kwa* ‘Abdu’l-Bahá,

***na kuchapishwa na:***

*Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji*
*ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha’i wa Tanzania*
*Simu: +255  685 637 422*
*S.L.P. 585, Dar Es Salaam, Tanzania.*
**Barua Pepe:** *secretariat@bahai.or.tz*
*literature@bahai.or.tz*

***Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili na:***
*Kamati ya Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili ya Kitaifa*
*ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha’i wa Tanzania*

© Baraza la *Kiroho la Kitaifa la Wabaha’i wa Tanzania*

***Toleo la kwanza: 2022***

# Yaliyomo

Kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh……………………………………Uk 1

Kutoka Maandiko na Maneno ya 'Abdu'l-Bahá……………………..Uk 5

Kutoka Maandiko na Barua za Shoghi Effendi………………………Uk 14

Kutoka katika Katiba na Barua za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu…Uk 39

Faharasa …………………………………………….…………………...Uk 116

**Kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh**

Mizania ya ulimwengu imepinduliwa kupitia athari itetemeshayo ya Utaratibu huu mkuu kabisa, Mpya wa Ulimwengu. Utaratibu wa maisha ya binadamu umepinduliwa kupitia uwakala wa Mfumo huu wa kipekee wa ajabu—ambao mfano wake macho ya umauti hayajapata kushuhudia kamwe.
*(Kitáb-i-Aqdas, Aya ya 181)*

2.1 Enyi Watu wa Haki! Katika ufalme wa Mungu, muwe wachungaji wa kondoo Wake na muwalinde kutokana na mbwa-mwitu wakali ambao wamejitokeza katika mavazi ya kilaghai, kama ambavyo mngewalinda vijana wenu wenyewe. Hivyo ndivyo Mshauri, Mwaminifu anavyowasihi.
*(Kitáb-i-Aqdas, Aya ya 52)*

3.1 Mali wakfu kwa ajili ya hisani hurejea kwa Mungu, Mfunuaji wa Ishara. Hakuna aliye na haki ya kuzitoa bila ruhusa kutoka kwa Yeye Ambaye ni mahali pa mapambazukio ya Ufunuo. Baada Yake, mamlaka haya yanaenda kwa Aghsan, na baada yao kwa Nyumba ya Haki—iwapo itakuwa imesimikwa katika ulimwengu kwa wakati huo—ili kwamba waweze kutumia mali wakfu hizi kwa manufaa ya zile Sehemu ambazo zimekwisha tukuzwa ndani ya Hoja hii, na kwa ajili ya chochote ambacho kimeagizwa kwao na Yeye Ambaye ndiye Mungu wa uweza na nguvu. Vinginevyo, mali wakfu hizo zitarejeshwa kwa watu wa Bahá ambao huwa hawasemi ila kwa idhini Yake na wala hawahukumu ila kufuatana na kile ambacho Mungu ameamuru ndani ya Waraka huu—lo, wao ni mashujaa wa ushindi katikati ya mbingu na dunia—ili waweze kuzitumia kwa namna ambayo imewekwa ndani ya Kitabu na Mungu, Muweza, Mkarimu.
*(Kitáb-i-Aqdas, Aya ya 42)*

4.1 "Toa shukrani kwa Bwana wako, Ewe Carmel. Moto wa kutengwa kwako kutoka Kwangu ulikuwa unakuteketeza kwa haraka, wakati bahari ya uwepo Wangu ilipojimwaga mbele ya uso wako, ikiyaburudisha macho yako na yale ya muumbo mzima, na kuvijaza kwa furaha kuu vitu vyote

vionekanavyo na visivyoonekana. Shangilia, kwa kuwa katika Siku hii Mungu amesimika juu yako kiti Chake cha enzi, amekufanya kuwa mahali pa mapambazuko pa ishara Zake na chimbuko la shuhuda za Ufunuo Wake. Heri ni yake yule akuzungukaye wewe, yule atangazaye ufunuo wa utukufu wako, na kusimulia kile ambacho neema ya Bwana Mungu wako amekinyunyizia juu yako. Ikamate Kalisi ya Umilele katika jina la Bwana wako, Mwenye Utukufu Wote, na toa shukrani Kwake, kwa kuwa Yeye, kama ishara ya huruma Yake kwako, amegeuza huzuni yako kuwa furaha, na kubadili majuto yako kuwa shangwe kuu. Yeye, kwa hakika, hupapenda mahali ambapo pamefanywa kiti cha enzi Yake, ambapo nyayo Zake zimekanyaga, ambapo pametukuzwa kwa uwepo Wake, kutoka hapo Yeye hupaza mwito Wake, na ambapo alimwaga machozi Yake.

4.2 Iite Sayuni, Ewe Carmel, na tangaza habari njema za furaha: Yule ambaye alikuwa amefichika kutoka macho ya umauti amekuja! Enzi Yake ishindayo vyote imedhihirishwa, utukufu Wake ukumbatiao vyote umefunuliwa. Jihadhari usije ukasitasita au kusimama. Jitokeze haraka na ukauzunguke Mji wa Mungu ambao umeshuka kutoka mbinguni, Kaaba ya mbinguni ambayo kwayo huzungukwa kwa kusujudu na wapendelewa wa Mungu, walio safi moyoni na kikosi cha malaika waliotukuka kabisa. Ee, ni jinsi gani ninavyotamani kutangazia kila pahali kwenye uso wa dunia, na kupeleka kwa kila moja ya majiji yake, habari njema za furaha za Ufunuo huu—Ufunu ambao moyo wa Sinai umevutiwa kwake, na katika jina lake Kichaka Kiwakacho kinapaza sauti: ‘Kwa Mungu, Bwana wa Mabwana, falme za duniani na mbinguni ni zake.’ Kwa hakika hii ndiyo Siku ambamo vyote nchi na bahari hulishangilia tangazo hili, Siku ambayo kwayo vimewekwa vile vitu ambavyo Mungu mwenyewe, kupitia majaliwa yaliyo mbali na mipaka ya akili au moyo wa umauti, imekusudiwa kwa ajili ya ufunuo. Muda si mrefu Mungu atatua nanga ya Safina Yake juu yako, na atawadhihirisha watu wa Bahá ambao wametajwa katika Kitabu cha Majina.”

*(Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas (Shirika la Uchapishaji la Kibaha’i; Wilmette: chapisho la 1988, 2005), uk. 4–5)*

5.1 Inawapasa Wadhamini wa Nyumba ya Haki washauriane pamoja kuhusiana na yale mambo ambayo kwa muonekano wa nje hayajafunuliwa katika Kitabu, na kuagiza utekelezwaji wa kile kikubalikacho kwao. Kwa hakika Mungu atawavuvia na chochote Akitakacho, na Yeye, kwa hakika, ndiye Mtoaji, Mwenye Maarifa Yote.
*(Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas, uk. 68)*

6.1 Tunawasihi watu wa Nyumba ya Haki na kuwaamuru kuhakikisha ulinzi na usalama wa wanaume, wanawake na watoto. Inawapasa wajali kwa hali ya juu kabisa manufaa ya watu katika nyakati zote na katika hali zote.
*(Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas, uk. 69 - 70)*

7.1 Inawapasa watu wa Nyumba ya Haki ya Mungu kukazia macho yao mchana na usiku juu ya kile ambacho kimeng'aa kutoka Kalamu ya Utukufu kwa ajili ya ufunzaji wa watu, ujenzi wa mataifa, ulinzi wa watu na hifadhi ya hadhi yao.
*(Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas, uk. 125)*

8.1 Kifungu hiki, kinachoandikwa sasa kwa Kalamu ya Utukufu, kinahesabika kama sehemu ya Kitabu Kitakatifu Kabisa: Watu wa Nyumba ya Haki ya Mungu wamepewa dhamana ya mambo ya watu. Kwa hakika, wao ni Wadhamini wa Mungu miongoni mwa watumishi Wake na vyanzo vya mamlaka katika nchi Zake.

8.2 Enyi watu wa Mungu! Kile ambacho huufunza ulimwengu ni haki, nayo hushikilwa na nguzo mbili, thawabu na adhabu. Nguzo hizi mbili ndiyo vyanzo vya uhai kwa ulimwengu. kwa kuwa kila siku kuna tatizo jipya na kwa kila tatizo kuna suluhu inayofaa, mambo kama hayo yarejelewe kwa Nyumba ya Haki ya Ualimwengu ili wajumbe wake waweze kutenda kufuatana na haja na mahitaji ya wakati. Wale ambao, kwa ajili ya Mungu, huinuka kuhudumia Hoja Yake, ndiyo wapokeaji wa uvuvio mtakatifu kutoka Mbingu isiyoonekana. Inawapasa wote wawe watiifu kwao. Masuala yote ya Nchi yanapaswa yarejelewe kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, lakini matendo ya ibada lazima yafanyike kufuatana na kile

ambacho Mungu amekifunua katika Kitabu Chake.

*(Nyaraka za Baha'u'llah Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas, uk. 128 – 129)*

9.1 Dini humjalia mtu tunu yenye thamani kubwa kuliko zote, humgawia kikombe cha usitawi, humpatia uzima wa milele na hunyunyizia manufaa yasiyo na mwisho kwa mwanadamu. Inawabidi machifu na watawala wa ulimwengu, na hususan Wadhamini wa Nyumba ya Haki ya Mungu, wajitahidi kwa uwezo wao wa hali ya juu kabisa kuhifadhi daraja lake, kuendeleza raghba zake na kutukuza daraja lake machoni pa ulimwengu. Vivyo hivyo inawapasa kuchunguza ndani ya hali za watu wao na kujifahamisha wenyewe mambo na shughuli za jamii mbalimbali zilizo ndani ya mamlaka yao. Tunatoa wito kwa wadhihirishaji wa uwezo wa Mungu—viongozi na watawala duniani—kujishughulisha wenyewe na kufanya yale yote yaliyo katika uwezo wao ili huenda waweze kuondoa mfarakano kutoka katika ulimwengu huu na kuuangazia kwa mwanga wa mapatano.

*(Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas, uk. 130)*

**Kutoka Maandiko na Maneno ya ‘Abdu’l-Bahá**

10.1 Tawi takatifu na chipukizi, Mlinzi wa Hoja ya Mungu, pamoja na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, itakayochaguliwa na kuanzishwa na wote, wote wapo chini ya uangalizi na ulinzi wa Uzuri wa Abhá, chini ya hifadhi na muongozo usiokosea wa Yule Aliyetukuka (maisha yangu na yatolewa dhabihu kwa ajili yao wote). Lolote waamualo ni la Mungu. Yeyote asiyemtii yeye, wala kuwatii wao, hajamtii Mungu; yeyote anayeshindana nao ameshindana na Mungu; yeyote anayebishana naye amebishana na Mungu; yeyote anayemkana yeye amemkana Mungu; yeyote ambaye hamuamini yeye hamuamini Mungu; yeyote akengeukaye, ajitengaye mwenyewe na ageukiaye kando kutoka yeye kwa hakika amekengeuka, amejitenga mwenyewe na kugeukia kando kutoka kwa Mungu. Ghadhabu, hasira kali, kisasi cha Mungu viwe juu yake! Ngome imara itabakia isiyopenyeka na salama kwa kupitia utii kwa yeye ambaye ni Mlinzi wa Hoja ya Mungu. Inawapasa wajumbe wa Nyumba ya Haki, kwa Aghṣán wote, Afnán, Mikono wa Hoja ya Mungu kuonesha utii wao, kujisalimisha, na kujishusha kwa Mlinzi wa Hoja ya Mungu, kumgeukia yeye na kunyenyekea mbele yake.
*(Wasia na Agano la ‘Abdu’l-Bahá (Shirika laa Uchapishaji la Kibahá’í; chapisho la 1944, 2013), uk. 21–22)*

11.1 Na sasa, kuhusiana na Nyumba ya Haki ambayo Mungu ameiamuru kama chanzo cha mema yote na huru kutokana na makosa yote, ni lazima ichaguliwe kwa kura za wote, yaani, na waumini. Wajumbe wake lazima wawe wadhihirishaji wa hofu ya Mungu na chemchemi ya maarifa na ufahamu, lazima wawe thabiti katika imani ya Mungu na watakia mema wa binadamu wote. Kwa Nyumba hii humaanishwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, yaani, katika nchi zote Nyumba ya Haki lazima ianzishwe, na Nyumba hizi za Haki lazima zichague wajumbe wa ile ya Ulimwengu. Kwenye chombo hiki mambo yote yanatakiwa kurejelewa. Kinatunga sheria zote na kanuni ambazo hazipatikani kwenye Maandiko Matakatifu dhahiri. Kwa chombo hiki matatizo yote magumu yatatatuliwa na Mlinzi wa Hoja ya Mungu atakuwa mkuu wake mtakatifu na mjumbe wa kipekee

wa maisha ya chombo hicho. Asipohudhuria vikao mwenyewe lazima ateue mtu wa kumwakilisha. Endapo mjumbe yeyote atatenda dhambi yenye kudhuru ustawi wa wengi, Mlinzi wa Hoja ya Mungu ana uwezo wa haki ya kumfukuza. ambapo watu lazima wachague mwingine badala yake. Hii Nyumba ya Haki hutunga sheria na serikali huzisimamia. Chombo cha kutunga sheria lazima kikipe nguvu kile cha utendaji, na chombo cha utendaji lazima kihudumie na kukisaidia chombo cha kutunga sheria ili kwamba kupitia muungano wa karibu na upatano wa ngome hizi mbili msingi wa usawa na haki uweze kuwa imara na wenye nguvu, ili maeneo yote ulimwenguni yaweze kuwa kama Paradiso yenyewe.
*(Wasia na Agano la ‘Abdu’l-Bahá uk. 28–30)*

12.1 Huu ndiyo msingi wa imani ya watu wa Bahá (maisha yangu yaweze kutolewa kwa ajili yao): “Mtakatifu, Aliyetukuka (Báb), ni Mdhihirishaji wa Umoja na Upekee wa Mungu na Mtangulizi wa Uzuri wa Kale: Mtakatifu Uzuri wa Abhá (maisha yangu yawe dhabihu kwa ajili ya marafiki Zake thabiti) ni Mdhihirishaji Mkuu Kabisa wa Mungu na ni Chimbuko la Asili Yake Takatifu Kabisa. Wengine wote ni watumishi Kwake na hutenda amri Zake.” Kwa Kitabu Kitakatifu Kabisa kila mmoja sharti akigeukie na kile ambacho hakikuelezwa wazi wazi humo sharti kirejewe kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Kile ambacho shirika hili, iwe kwa kauli moja au ya walio wengi hukubaliana kutenda, hicho kwa hakika ndiyo Ukweli na Kusudi la Mungu Mwenyewe. Yeyote akengeukaye hapo kwa hakika ni kati ya wale ambao hupenda mifarakano, ameonesha husuda na kumpa kisogo Bwana wa Agano. Kwa Nyumba hii humaanisha ile Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo kwamba inapaswa kuchaguliwa kutoka nchi zote, yaani kutoka sehemu zile za Mashariki na Magharibi ambako wapendwa hupatikana, kwa namna ya chaguzi za kiutamaduni katika nchi za Magharibi kama vile ya Uingereza.

12.2 Inawapasa wajumbe hawa (wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu) kukusanyika eneo fulani na kushughulikia matatizo yote yanayoleta tofauti, maswali ambayo hayaeleweki vizuri na mambo ambayo hayajaandikwa moja kwa moja katika Kitabu. Chochote wanachoamua kina athari sawa

sawa na Andiko lenyewe. Na kama ambavyo hii Nyumba ya Haki ilivyo na mamlaka kutunga sheria juu ya masuala ambayo hayajaelezwa moja kwa moja kwenye Kitabu kwa ajili ya uendeshaji wa mambo ya kila siku pia inayo mamlaka kufuta sheria hizo. Hivyo, kwa mfano, Nyumba ya Haki inatunga sheria fulani leo na kuitumia, baada ya miaka mia moja kukiwa kumetokea mabadiliko makubwa mno na hali kuwa imebadilika, Nyumba ya Haki nyingine itakuwa na mamlaka, kulingana na mahitaji ya wakati huo kuibadilisha sheria hiyo. Hili linaweza kufanyika kwa sababu sheria hiyo siyo sehemu ya Maandiko Matakatifu moja kwa moja. Nyumba ya Haki inakuwa ni mtunzi na mbatilishaji wa sheria zake yenyewe.
*(Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá, uk. 39–41)*

13.1 Jihadharini mtu yeyote asije kufasiri maneno haya kwa upotofu, na kama wale ambao wamevunja Agano kufuatia Siku ya Kupaa (kwa Bahá'u'lláh) kuleta kisingizio, kuinua bendera ya uasi, kupandisha hasira za ununda na kuacha wazi mlango wa fasiri za uwongo. Hakuna yeyote anayepewa haki ya kuweka maoni yake au kuelezea imani yake maalum. Wote sharti waombe muongozo na kugeukia Kitovu cha Hoja na Nyumba ya Haki. Na yule akigeukiaye kingine chochote kile kwa kweli yu katika kosa kubwa.
*(Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá, uk. 54)*

14.1 Suala ni kwamba, kabla ya kwisha kwa miaka elfu moja, hakuna mtu anayeweza kutia neno. Wote sharti wajione kuwa walio katika utaratibu wa kutii, wanyenyekevu na watiifu wa amri za Mungu na sheria za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Endapo yeyote akikengeuka japo kwa kiwango cha ncha ya sindano kutii amri za Nyumba ya Haki ya Ualimwengu, au kusita kuzikubali, basi yeye atakuwa miongoni mwa watu waliotengwa na kukataliwa.

(Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í; chapisho la 1997, 2009), aya ya 33.6)

15.1 Fahamu Ee kijakazi, kwamba machoni pa Bahá, wanawake wanahesabika sawa na wanaume, na Mungu amewaumba binadamu wote

kwa sura na mfano Wake mwenyewe. Yaani, wanaume na wanawake kadhalika ni wafunuaji wa majina na sifa Zake, na kutoka katika mtazamo wa kiroho hakuna tofauti baina yao. Yeyote ajisogezaye karibu zaidi na Mungu, huyo ndiye anayependelewa kabisa, awe mwanaume au mwanamke. Ni vijakazi wangapi, wakiwa na shauku na waliojifunga kibwebwe, wakiwa ndani ya kivuli kihifadhicho cha Bahá, wamethibitisha kuwa bora kuliko wanaume, na kuwapita kabisa wenye umaarufu duniani.

15. 2 Nyumba ya Haki, walakini, kulingana na maandiko dhahiri ya Sheria za Mungu, imefungiwa kwa wanaume tu; hii ni hekima Zake Bwana Mungu, ambazo muda si mrefu zitadhihirishwa wazi kama vile jua la utosini.
*(Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá, uk. 38.3–38.4).*

16.1 Sifa ziwe kwa Mungu, milango yote kama hiyo imefungwa katika Hoja ya Bahá'u'lláh kwa kuwa Kitovu chenye mamlaka maalum kimeteuliwa—Kitovu ambacho hutatua matatizo yote na kuepushia mbali tofauti zote. Vivyo hivyo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, huepushia mbali tofauti zote na chochote inachoagiza lazima kikubaliwe na yule anayekaidi amekataliwa. Lakini hii Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo ndiyo chombo cha kutunga sheria bado haijaanzishwa.

16.2 Hivyo, inaonekana kwamba hakuna njia iliyoachwa kwa ajili ya mabishano, lakini tamaa za kimwili ndiyo chanzo cha tofauti kama ilivyo kwa wavunja sheria. Hawa hawashuku uhalali wa Agano bali malengo ya ubinafsi yamewaburuzia kwenye hali hii. Si kwamba hawajui kile wanachofanya—wanafahamu fika kabisa na bado wanaonesha upinzani.
*(Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá, uk. 187.2–187.3)*

17.1 Kusudi langu ni hili, kwamba kabla ya kumalizika kwa miaka elfu moja, hakuna yeyote mwenye haki ya kunena neno, hata kudai daraja la Ulinzi. Kitabu Kitakatifu Kabisa ni Kitabu ambacho kwacho watu wote watakirejelea, na ndani mwake Sheria za Mungu zimefunuliwa. Sheria ambazo hazikutajwa katika Kitabu hazina budi zirejelewe kwenye

maamuzi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Hakutakuwa na nafasi kwa ajili ya tofauti….Chondechonde asije mtu yeyote akatengeneza mpasuko au kuamsha uchochezi. Endapo pakiwepo na tofauti za maoni, Nyumba Kuu Kabisa ya Haki mara moja ingetatua matatizo hayo. Vyovyote maamuzi yake yatakavyokuwa, kwa kura za wengi, utakuwa ndiyo ukweli halisi, kwa kuwa Nyumba hiyo ipo chini ya ulinzi, muongozo usiokosea na uangalizi wa Bwana mmoja wa kweli. Yeye ataikinga kutokana na makosa na kuilinda chini ya bawa la utakatifu Wake na utovu wa makosa. Yule aipingaye atatupwa nje na hatimaye atakuwa kati ya walioshindwa.

17.2 Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki sharti ichaguliwe kulingana na mfumo unaofuatwa katika uchaguzi wa mabunge ya Ulaya. Na wakati nchi zitakapokuwa zikiongozwa, Nyumba za Haki za nchi mbalimbali zitachagua Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki….

17.3 Uanzishwaji wa Nyumba hiyo hautegemei juu ya ubadilishwaji wa mataifa yote ya ulimwengu kuwa katika Imani moja. Kwa mfano, kama hali zikiruhusu na hakutakuwa na usumbufu utakaosababishwa, marafiki huko Uajemi watachagua wawakilishi wao, na vivyo hivyo marafiki huko America, India na maeneo mengine pia watachagua wawakilishi wao na hawa wachaguwe Nyumba ya Haki. Nyumba hiyo ya Haki itakuwa ndiyo Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki. Ndiyo ilivyo.
*(Kutoka Waraka uliotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

18.1 Umeuliza kuhusu vigezo vya jumla vinavyohusiana na uasi wa kidini. Uasi wa kidini hurejelea kwenye mambo kama yale ambayo hayakuamriwa katika maandiko dhahiri ya Kitabu na ambayo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haijaidhinisha.
*(Kutoka Waraka uliotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

19.1 Yale masuala yenye umuhimu mkubwa ambayo hufanya msingi wa Sheria za Mungu zilizoandikwa dhahiri katika Maandiko, lakini sheria ndogo ndogo imeachiwa Nyumba ya Haki. Hekima ya hili ni kwamba nyakati kamwe hazibaki vile vile, kwani mabadiliko ni sifa ya lazima na njema muhimu ya ulimwengu huu, na ya wakati na mahali. Kwa hiyo,

Nyumba ya Haki itachukua hatua kama ipasavyo.

19.2 Acha isidhaniwe kwamba Nyumba ya Haki itafanya uamuzi wowote kulingana na dhana na mawazo yake yenyewe. Mungu apishie mbali! Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki itafanya maamuzi na kuanzisha sheria kupitia uvuvio na uthibitisho wa Roho Mtakatifu, kwa sababu ipo katika usalama na chini ya hifadhi na ulinzi wa Uzuri wa Kale, na utii kwa maamuzi yake inapasa na ni wajibu muhimu na jukumu kamilifu na hakuna nafasi ya kukwepa kwa yeyote.

19.3 Sema, Enyi watu: Kwa hakika, Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki ipo chini ya mabawa ya Bwana wenu, Mwenye Huruma, Mwenye Rehema—Zote, yaani, chini ya ulinzi Wake, uangalizi Wake na hifadhi Yake; kwa kuwa Yeye amewaamuru waumini thabiti kutii shirika hilo lililobarikiwa, kutakasika na litiishalo, ambalo mamlaka yake yameamriwa kitakatifu na ya Ufalme wa Mbinguni na ambalo sheria zake huvuviwa na ni za kiroho.

19.4 Kwa kifupi, hii ndiyo hekima ya kurejelea sheria za kijamii kwa Nyumba ya Haki. Katika dini ya Kiislám, vivyo hivyo, siyo kila sheria ilifunuliwa kwa uwazi, la, siyo kila sehemu ya kumi ya sehemu ya kumi ilijumuishwa katika Maandiko; ingawa masuala yote yenye umuhimu mkubwa hususani yalirejelewa, bila shaka zilikuwepo maelfu ya sheria ambazo hazikuainishwa. Hizi zilitungwa na makasisi wa zama za baadaye kulingana na sheria za kiislam vyombo vyake vya kisheria na makasisi binafsi walifanya marekebisho yenye mkanganyiko kutoka kwenye sheria zilizofunuliwa mwanzoni. Zote hizi ziliagizwa zitumike. Leo mchakato huu wa upunguzaji ni haki ya shirika la Nyumba ya Haki, na upunguzaji na mahitimisho ya wasomi binafsi havina mamlaka, vinginevyo kama imeidhinishwa na Nyumba ya Haki. Tofauti kwa uhakika ni hii, kwamba kutokana na mahitimisho na idhini ya shirika la Nyumba ya Haki ambayo wajumbe wake wamechaguliwa na, na wanajulikana kwa Jumuiya ya Kibahá'í kote ulimwengu, hakuna tofauti zitakazoibuka; ambapo mahitimisho ya makasisi binafsi na wasomi, kwa hakika yatasababisha

tofauti, na matokeo yake yatakuwa mfarakano, mgawanyiko na msambaratiko. Umoja wa Neno utaharibiwa, umoja wa Imani utatoweka na jengo la Imani ya Mungu litatikiswa.
*(Kutoka Waraka uliotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

20.1 Sheria kama zile ambazo hazikutajwa katika Kitabu, lazima zote zirejelewe kwa Nyumba ya Haki na siyo kwa 'Abdu'l-Bahá, kwa kuwa yeye ni mfasiri wa sheria ambazo zimetajwa katika Kitabu na siyo mtunzi wa zile ambazo hazimo. Hata hivyo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu iliyoamriwa kitakatifu—ambayo, baada ya tangazo la Hoja ya Mungu, itachaguliwa na Wabahá'í wote kote ulimwenguni—Shirika hilo la ulimwengu limewezeshwa kutunga sheria ambazo hazikuandikwa wazi wazi katika Kitabu. Inapasa, ni faradhi na inabidi kwa kila mmoja kuitii. Na wakati wowote Nyumba ya Haki inapopitisha sheria ambazo hazijaandikwa wazi wazi katika Kitabu, iwe kwa kauli moja au kwa wingi wa kura, yeyote anayehoji kwa nini au kwa namna gani kwa hakika amempinga Mungu katika zoezi la ukuu Wake, amebishia na uthibitisho Wake, amezikaidi ishara Zake, na amezikana amri Zake.
*(Kutoka Waraka uliotafsiriwa kutoka Kiajemi na Kiarabu)*

21.1 Fahamu kwamba kutokuwepo na kosa ni kwa aina mbili: kutokuwepo na kosa katika asili na kutokuwepo na kosa kama njema. Hivyo hivyo ndiyo kweli kwa majina na njema zote: Kwa mfano, kuna ujuzi wa asili ya kitu na ujuzi wa njema yake. Kutokuwepo na kosa katika asili ni kwa Wadhihirishaji wa Mungu wa ulimwengu; kwani kutokuwepo na kosa ni hitaji la lazima la uhalisia Wao, na hitaji la lazima la kitu haliwezi kutenganishwa na kitu chenyewe. Mionzi ni hitaji la lazima la jua na haiwezi kutenganishwa nalo; ujuzi ni hitaji la lazima la Mungu na hauwezi kutenganishwa Naye; uwezo ni hitaji la lazima la Mungu na vile vile hauwezi kutenganishwa Naye. Kama ingewezekana kuvitenganisha hivi kutoka Kwake, Yeye asingekuwa Mungu. Kama mionzi ingeweza kutenganishwa na jua, lisingekuwa jua. Kwa hiyo, laiti mtu angefikiria kuwa Kutokuwepo na kosa kwa Juu Kabisa kungeweza kutenganishwa kutoka kwa Mdhihirishaji wa Mungu wa ulimwengu, Yeye asingekuwa

Mdhihirishaji wa ulimwengu na angekosa ukamilifu muhimu.

21.2 Lakini kutokuwepo na kosa kama njema siyo hitaji la lazima; bali, ni muonzi wa zawadi ya kutokuwepo na kosa unaong'aa kutoka Jua la Ukweli juu ya baadhi ya mioyo na huwapa hisa na sehemu yake. Ingawa roho hizi siyo lazima ziwe zisizokuwa na kosa, walakini zipo chini ya matunzo, ulinzi, uongozi usiokosea wa Mungu—maana yake ni kwamba, Mungu anazilinda kutoka utendaji makosa. Hivyo, zimekuwepo roho nyingi zilizotakasika ambazo zenyewe hazikuwa Chanzo cha Juu Kabisa cha Kutokuwepo na kosa, lakini ambazo, licha ya hilo zimelindwa na kuhifadhiwa kutoka kufanya makosa chini ya kivuli cha uangalizi mtakatifu na ulinzi. Kwa sababu wao walikuwa mifereji ya neema takatifu kati ya Mungu na mwanadamu, na kama Mungu asingewahifadhi kutoka kutenda makosa, wao wangewaongoza waaminifu wote kuingia katika makosa pia, kitu ambacho kingedhoofisha kabisa misingi ya dini ya Mungu na ambacho kisingefaa wala kustahili Uhalisia Wake uliotukuka.

21.3 Kufupisha, kutokuwepo na kosa kiasili ni kwa Wadhihirishaji wa Mungu wa ulimwengu, na kutokuwepo na kosa kama njema kumepewa roho zilizotakasika. Mathalani, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ikiwa itasimikwa chini ya vigenzo vya lazima—yaani, kama itachaguliwa na jumuiya nzima—kwamba Nyumba ya Haki itakuwa chini ya ulinzi na uongozi usiokosea wa Mungu. Kama Nyumba ya Haki ikiamua kwa kauli moja au kwa wingi juu ya suala ambalo halikuandikwa wazi wazi katika Kitabu, uamuzi huo na amri vitalindwa kutoka makosa. Sasa, wajumbe wa Nyumba ya Haki kama watu binafsi siyo lazima kwamba hawawezi kutenda makosa, lakini shirika la Nyumba ya Haki lipo chini ya ulinzi na uongozi usiookosea wa Mungu: huku huitwa kujaliwa kutotenda makosa.

21.4 Kwa kifupi, Bahá'u'lláh husema kwamba "Yule Ambaye ni Mahali pa Mapambazuko pa Hoja ya Mungu" ni mdhihirishaji wa "Yeye hufanya chochote atakacho", kwamba daraja hili limehifadhiwa kwa yule Kiumbe aliyetakasika, na kwamba wengine hawapati fungu lolote katika ukamilifu huu wa lazima. Yaani, kwa kuwa kutokuwepo na kosa kwa lazima kwa

Wadhihirishaji wa Mungu kumeshawekwa, chochote kitokacho Kwao kinafanana na ukweli na kinapatana na uhalisia. Wao hawapo chini ya kivuli cha dini iliyotangulia. Chochote wasemacho ni kauli ya Mungu, na chochote watendacho ni kitendo kinyofu, na hakuna muumini mwenye ruhusa ya kupinga; bali lazima aoneshe utiifu kamili katika suala hili, kwa sababu Mdhihirishaji wa Mungu hutenda kwa hekima kamili, na akili ya mwanadamu yaweza isiwe na uwezo wa kuzingatia hekima iliyofichwa ya baadhi ya masuala. Kwa hiyo, chochote Mdhihirishaji wa Mungu wa ulimwengu asemacho na atendacho ndiyo asili yenyewe ya hekima na kinapatana na uhalisia.
*(Some Answered Questions (Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu: Haifa, 2014), chapisho la 45.2–5)*

22.1 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, au ya kimataifa, pia itaundwa. Maamuzi yake yatafuatana na amri na mafundisho ya Bahá'u'lláh, na kile ambacho Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inachoamuru kitatiiwa na binadamu wote. Nyumba hii ya Haki ya kimataifa itateuliwa na kuratibiwa kutoka Nyumba za Haki za ulimwengu mzima, na ulimwengu wote utakuwa chini ya utawala wake.

22.2 Na kuhusu sifa kuu kabisa ya ufunuo wa Bahá'u'lláh, fundisho maalum ambalo halikutolewa na Mtume yeyote wa zamani: ni agizo na uteuzi wa Kitovu cha Agano. Kwa uteuzi huu na nyenzo, Yeye ameihifadhi na kuilinda dini ya Mungu dhidi ya tofauti na utengano, akifanya isiwezekane kwa yeyote kuunda madhehebu mapya au kikundi kidogo cha imani.
*(Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu, Mazungumzo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá wakati wa ziara Yake ya Muungano wa Majimbo ya America na Canada mnamo 1912 (Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Wilmette, 1982, chapisho la 2012), uk. 642)*

**Kutoka Maandiko na Barua za Shoghi Effendi**

23.1 Katika Hati hii ya ustaarabu wa siku zijazo wa ulimwengu [Kitáb-i-Aqdas] Mtunzi wake—wakati huo huo Jaji, Mtoa sheria, Muunganishaji na Mkombozi wa jamii ya binadamu—huwatangazia wafalme wa dunia tangazo rasmi la "Sheria Kuu Kabisa"…. Ndani yake Yeye anaamuru rasmi uanzishwaji wa "Nyumba ya Haki," huelezea bayana utendaji wake, huweka mapato yake na huwataja wajumbe wake kama "Wanaume wa Haki," "Makaimu wa Mungu," "Wadhamini wa Mwenye Rehema—Kabisa" ....

*(God Passes By (Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1974, chapisho la 2019), uk. 338–339)*

24.1 Pamoja na Mabaraza haya, ya mahali kadhalika na ya kitaifa, yanayofanyakazi kwa upatano, kwa juhudi kubwa, kwa ufasaha kote katika ulimwengu wa Kibahá'í, njia pekee kwa ajili ya usimikwaji wa Nyumba ya Juu ya Haki itakuwa imepatikana. Na pale ambapo Shirika hili Kuu litakapokuwa limesimikwa barabara, litalazimika kufikiria upya hali nzima na kuweka kanuni zitakazoongoza masuala ya Hoja, ilimradi itaonekana ni busara.

*(Kutoka barua ya 12 Machi 1923 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, katika Baha'i Administration Jumbe Zilizoteuliwa, 1922–1932 (Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1974), uk. 41)*

25.1 Kuhusu utaratibu na usimamizi wa masuala ya kiroho ya marafiki, kile ambacho ni muhimu sana sasa ni uimarishaji wa Mabaraza ya Kiroho katika kila kituo, kwa sababu juu ya misingi hii madhubuti na isiyotikiswa, Nyumba ya Juu ya Haki ya Mungu itainuliwa na kusimikwa imara katika siku zijazo. Pale jengo hili kuu kabisa litakapoinuliwa juu ya msingi usiotikisika, kusudi la Mungu, hekima, kweli za ulimwengu wote, siri na uhalisia wa Ufalme, ambavyo Ufunuo wa ajabu wa Bahá'u'lláh umeweka ndani ya Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá, pole pole vitafunuliwa na kudhihirishwa.

*(Kutoka barua ya 19 Desemba 1923 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Mashariki —iliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

26.1 Kusudi la msisitizo wa kudumu na shadidi juu ya uhimili na uimarishaji wa Mabaraza haya ya Kiroho ni hili—kwamba msingi wa Hoja ya Mungu lazima upanuke na uwe wenye nguvu siku hadi siku, kwamba hakuna mkanganyiko utakaoingia kamwe katika utaratibu mtakatifu, kwamba mafundo mapya na yenye nguvu yaweze kufungwa kati ya Mashariki na Magharibi, kwamba umoja wa Kibahá'í ulindwe na kuangazia macho ya watu wa ulimwengu kwa wangavu wake, ili kwamba juu ya Mabaraza haya Nyumba za Haki za Mungu ziweze kusimikwa imara na juu ya Nyumba za Haki za pili jengo bora la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu liweze, kwa mpangilio kamili, ukamilifu na utukufu, na bila ucheleweshaji wowote, liweze kuinuliwa. Pale Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itakapokuwa imetokeza kutoka milki ya matumaini hadi ule muonekano wa utimilifu na umaarufu wake kusimikwa katika kila kona na hali ya ulimwengu, ndipo shirika hilo kuu takatifu—lililosimikwa kwa uimara na kuwekwa juu ya msingi thabiti na usiotikisika wa jumuiya nzima ya Kibahá'í ya Mashariki na Magharibi, na mpokeaji wa fadhili za Mungu na uvuvio Wake—itasonga mbele na kuunda na kutekeleza miradi muhimu, shughuli za ulimwengu mzima na uanzishwaji wa asasi tukufu. Kwa njia hii, umaarufu wa Hoja ya Mungu utakuwa wa ulimwengu mzima na mwangaza wake utaangazia dunia nzima.

*(Kutoka barua ya 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Ulimwengu kila mahali Mashariki na Magharibi—iliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

27.1 Jamii ya wanadamu, ikiwa imeraruliwa na mafarakano na ikiungua kwa chuki, katika saa hii inalilia kipimo kilichojaa cha ule upendo unaotokana na Mungu, ule upendo ambao hatimaye utathibitika kuwa ule wa ufumbuzi wa shida na matatizo yake yasiyohesabika. Je, haitupasi sisi, ambao mioyo yetu inawaka kwa upendo kwake, kuendelea kufanya juhudi kubwa zaidi, kudhihirisha ule upendo katika usafi wake wote na uwezo katika shughuli zetu na wenzetu? Upendo wetu kwa mpendwa Bwana wetu, wenye shauku kubwa, usio na raghba kabisa katika sura zake zote, na uweze kupata utambulisho wake wa kweli katika upendo

kwa ndugu na dada zetu katika Imani halikadhalika kwa binadamu wote. Ninawahakikishia, marafiki wapendwa, kwamba maendeleo katika maswala kama haya hayana mipaka na ni ya milele, na kwamba juu ya kiwango cha mafanikio yetu katika shughuli hizi, hatimaye kitategemea mafanikio ya dhima yetu maishani.

27.2 Na kadiri tunavyofanya juhudi kuonesha upendo huo kwa ulimwengu pia tuweze kusafisha akili zetu kutokana na mabaki ya dalili zozote za huzuni ya kutokuelewana ambayo yaweza kuficha mawazo yetu yaliyowazi ya kusudi hasa na mbinu za utaratibu mpya wa ulimwengu, wenye changamoto nyingi na ngumu, walakini ni mkamili kabisa na wa busara. Tunaitwa na mpendwa Bwana wetu katika Wasia na Agano Lake siyo kulifuata kwa kusita, bali kufichua thamani yake kwa ulimwengu mzima. Kujaribu kukadiria thamani yake kamili, na kupata maana yake hasa baada ya kupita kwa muda mfupi sana tangu kuanzishwa kwake, ni mapema mno na ujuvi kwetu. Lazima tuwe na imani na wakati, na muongozo wa Nyumba ya Mungu ya Haki ya Ulimwengu, ili kupata uelewa wa wazi na kamili zaidi wa nyenzo na athari zake.
*(Kutoka barua ya 23 Februari 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, katika Bahá'í, uk. 62)*

28.1 Mabaraza haya ya Kiroho kwanza kabisa yameundwa kutekeleza mambo haya, na pili kuweka msingi kamili na madhubuti kwa ajili ya uanzishwaji wa Nyumba takatifu na ya Haki ya ulimwengu. Pale mhimili wa kati wa watu wa Bahá utakapokuwa umenzishwa ipasavyo, kwa ufahari na kwa uthabiti, kipindi kipya kitachomoza, fadhili za mbinguni na neema zitamiminika kutoka Chanzo hicho, na ahadi zikumbatiazo vyote zitatimizwa.
*(Kutoka barua ya 30 Oktoba 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Baraza la Kiroho la Mahali la Ṭehrán—iliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

29.1 Kuhusu utaratibu unaotakiwa kutumika kwa ajili ya uchaguzi wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, ni wazi kwamba maandiko ya Wasia ya Mpendwa hayatupi dalili ya jinsi Mabaraza haya yanavyopaswa

kuchaguliwa. Hata hivyo, katika moja ya Nyaraka Zake za mwanzoni kabisa, iliyoandikwa kwa rafiki mmoja huko Uajemi, yafuatayo yameandikwa dhahiri:

29.2 “Wakati wowote wapendwa wote wa Mungu katika kila nchi wateuapo wajumbe wao, na hawa kwa upande wao huchagua wawakilishi wao, na wawakilishi hawa kuchagua shirika, shirika hilo litachukuliwa kuwa Baytu’l-‘Adl Kuu Kabisa (Nyumba ya Haki ya Ulimwengu)”.

29.3 Maneno haya yanaonesha kwa uwazi kwamba uchaguzi wa hatua tatu umetolewa na ‘Abdu’l-Bahá kwa ajili ya uundaji wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa, na kama ilivyotolewa kwa uwazi katika Wasia na Agano Lake kwamba “Nyumba za Haki za Pili (yaani Mabaraza ya Kitaifa) lazima yachague wajumbe wa Ile ya Ulimwengu”, ni dhahiri kwamba wajumbe wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa watachaguliwa kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja na jamii ya waumini katika majimbo yao husika. Kufuatana na maagizo haya yanayokamilishana, kanuni iliyowekwa wazi katika barua yangu ya 12 Machi, 1923, imeshawekwa ikihitaji waumini (wapendwa wa Mungu) katika kila nchi kuchagua idadi fulani ya wajumbe ambao nao watachagua wawakilishi wao wa kitaifa (Nyumba ya Haki ya Pili au Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa), ambao wajibu na upendeleo wao mtakatifu utakuwa kuchagua kwa wakati Nyumba ya Mungu ya Haki ya Ulimwengu.
*(Kutoka barua ya 12 Mei 1925 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, katika Bahá’í Administration, uk. 84)*

30.1 Muda si mrefu, kwa ruhusa ya Bwana wetu, Mtukufu kabisa, utando utainuliwa kutoka kwenye sura ya Sheria Yake kuu kabisa, na mizania ya katiba Yake ya kushangaza—msingi wa Nyumba Yake ya Haki iliyo bora kabisa, ya juu na yenye uwezo—itawekwa Mahali hapa patakatifu, palipobarikiwa na peupe kama theluji, Kituo ambacho huzungukwa na viumbe vyote. Abarikiwe Mungu, Mtunzi wa Hoja hii ya kushangaza! Abarikiwe Mungu, Mwanzilishi wa Mwanga huu ung’aao na mwangavu! Abarikiwe Mungu, Mwasisi wa Jengo hili la juu kabisa1 katika eneo hilo

la mbali2—nchi ambamo itaakisiwa miangaza ya mahali pa kukusanyikia ya Mbinguni na mianga ya mahali patakatifu pa Ufalme! Atukuzwe kwa hiyo, Bwana wetu, Msaidizi, Mwenye Uwezo—Wote, Mtukufu Kabisa!
*(Kutoka barua ya Novemba 1927 kwa Wabahá'í wa Mashariki—iliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

31.1 Maswali yako kuhusiana na zile amri za Kiroho ambazo zingeainisha maisha ya Kibahá'í ya mtu binafsi na ya pamoja: Shoghi Effendi husema kwamba kwa jibu la haya lazima tusubiri uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa. Ni masuala yenye umuhimu kwa namna fulani na sisi hatupaswi kuamuru kuanzia sasa uanzishwaji wa vigezo vya mfano wa marejeo.
*(Kutoka barua ya 26 Aprili 1928 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

32.1 Sharti ikumbukwe kwa uangalifu kwamba Nyumba za Haki za mahali vile vile ya Kimataifa zimeamriwa mahususi katika Kitáb-i-Aqdas; kwamba asasi za Mabaraza ya Kiroho Ya Kitaifa, kama chombo cha kati, na kinachorejelewa katika Wasia wa Bwana kama "Nyumba ya Haki ya Pili," ina kibali dhahiri cha 'Abdu'l-Bahá; na kwamba mbinu yakufuatwa kwa ajili ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa na za Kitaifa zimeandikwa na Yeye katika Wasia wake, na vilevile katika Nyaraka zake kadhaa. pia katika Nyaraka Zake kadhaa. Aidha, asasi za Mifuko ya Hazina za mahali na za kitaifa, ambazo sasa ni viambatanisho vya lazima kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya mahali na ya kitaifa, siyo tu zimeanzishwa na 'Abdu'l-Bahá katika Nyaraka alizofunua kwa Wabahá'í wa Mashariki, lakini umuhimu wake na ulazima vimesisitizwa mara kwa mara na Yeye katika matamshi na maandiko Yake. Mkolezo wa mamlaka katika mikono ya wawakilishi waliochaguliwa wa waumini; ulazima wa utii wa kila muumini wa Imani kwa maamuzi yatakayofanywa na Mabaraza ya Kibahá'í; matakwa Yake kwa uamuzi wa wengi; tabia ya kufikia maamuzi kutokana na kura za wengi; na hata hitaji la usimamizi wa karibu kwa machapisho yote ya Kibahá'í, vimetiliwa mkazo kwa dhati na 'Abdu'l-

Bahá, kama ilivyoshuhudiwa na Nyaraka Zake halisi na zilizosambazwa mahali pengi. Kuyakubali Mafundisho Yake mapana na ya kibinadamu kwa upande mmoja, na kuyakataa na kuyapuuza kwa dharau pasipokujali maongozi Yake mazitto na ya kipekee zaidi, kingekuwa kitendo dhahiri cha utovu wa utii kwa kile ambacho Yeye amekipenda kuliko vyote maishani Mwake.

32.2 Kwamba utafika wakati, nafasi ya Mabaraza ya Kiroho ya leo itachukuliwa na Nyumba za Haki, na kwa dhamira yote na makusudi yanafanana na wala si mashirika tofauti, imethibitishwa mara nyingi na ‘Abdu’l-Bahá Mwenyewe. Kwa hakika katika Waraka aliowaandikia wajumbe wa Baraza la Kiroho la kwanza la Chicago, shirika la kwanza la Kibahá’í kuchaguliwa katika Muungano wa Majimbo ya Marekani, uliwarejelea kama wajumbe wa “Nyumba ya Haki” kwa ajili ya mji huo, na hivyo kwa kalamu Yake mwenyewe amethibitisha bila shaka yoyote utambulisho wa Mabaraza yaliyopo ya Kiroho ya Kibahá’í pamoja na Nyumba za Haki zilizorejelewa na Bahá’u’lláh. Kwa sababu ambazo siyo vigumu kuzibaini, imeonekana kwamba inafaa kuwapatia wawakilishi waliochaguliwa wa jumuiya za Kibaha’i kote ulimwenguni jina la muda la Mabaraza ya Kiroho, istilahi ambayo, kwa vile daraja na malengo ya Imani ya Kibahá’í yanaeleweka vyema na kutambulika kwa ukamilifu zaidi, ndivyo pole pole nafasi yake itachukuliwa na wadhifa wa kudumu na unaofaa zaidi wa Nyumba ya Haki.

---

[1] *Utaratibu wa Utawala wa Kibahái*

[2]*Bara la America*

Siyo tu kwamba Mabaraza ya Kiroho ya sasa yatakuwa na muundo tofauti katika siku zijazo, bali pia yatawezeshwa kwa kuongezewa zile nguvu, majukumu na haki zinazohitajiwa kutokana na utambulikaji wa Imani ya Bahá'u'lláh, siyo tu kama mojawapo ya mifumo inayotambulika ya kidini ulimwenguni, bali kama Dini ya Dola inayojitegemea yenye madaraka kamili. Na kadiri Imani ya Kibahá'í inavyopenyeza katika umma wa watu wa Mashariki na Magharibi, na ukweli wake kukumbatiwa na sehemu kubwa ya watu wa Dola Huru kadhaa za ulimwengu, ndipo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itakapofikia upeo wa uwezo wake, na kutekeleza, kama chombo cha juu kabisa cha Jumuiya za madola ya Kibahá'í, haki, wajibu na majukumu yote ya lazima juu ya taifa kuu la ulimwengu la siku zijazo.

32.3 Hata hivyo, lazima kutanabahi kwamba, katika muktadha huu, kinyume na kile kilichosemwa kwa kujiamini, usimikwaji wa Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki hautegemei kwa vyovyote vile juu ya kukubaliwa kwa Imani ya Kibahá'í na watu wa ulimwengu, wala hautegemei ukubali wa sehemu kubwa ya wakaazi wa nchi yoyote mojawapo. Kwa kweli, 'Abdu'l-Bahá Mwenyewe, katika mojawapo ya Nyaraka Zake za mwanzoni kabisa, aliwaza juu ya uwezekano wa uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika kipindi cha uhai Wake mwenyewe, na isingekuwa kutokana na hali mbaya zilizokuwepo chini ya utawala wa Kituruki, hatua za mwanzo kwa uwezekano wote zingeweza kuchukuliwa kwa ajili ya usimikwaji wake. Kwa hiyo, itakuwa dhahiri kwamba, kama hali nzuri zingeruhusu, ambapo Wabahá'í wa Uajemi na wa nchi jirani zilizokuwa chini ya utawala wa Kisovieti, wangewezeshwa kuchagua wawakilishi wao wa kitaifa, kufuatana na kanuni za muongozo zilizowekwa katika maandiko ya 'Abdu'l-Bahá, kikwazo pekee ambacho kingebakia katika uundwaji wa hakika wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa kingekuwa kimeondolewa. Kwani Nyumba za Haki za Kitaifa za Mashariki na Magharibi hukabidhiwa kazi, kufuatana na maagizo mahususi ya Wasia, ya kuchagua moja kwa moja wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa. Siyo hadi wao wenyewe watakapokuwa wawakilishi kamili wa tabaka

zote za waumini katika nchi zao husika, siyo hadi wapate uzito na tajiriba vitakavyowawezesha kufanya kazi kwa nguvu katika utaratibu wa maisha ya Hoja, ndiyo waweze kuliendea jukumu lao takatifu, na kuweka msingi wa Kiroho kwa ajili ya uundwaji wa chombo kitukufu kabisa katika ulimwengu wa Kibahá'í.

32.4 Lazima pia ieleweke kinagaubaga na kila muumini kwamba asasi ya Ulinzi kwa vyovyote haifuti, au hata kwa kiwango kidogo kabisa kupunguza, uwezo uliotolewa na Bahá'u'lláh kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika Kitáb-i-Aqdas, na imethibitishwa mara kwa mara na kwa dhati na 'Abdu'l-Bahá katika Wasia Wake. Haifanyizi kinyume kwa namna yoyote ile Wasia na Maandiko ya Bahá'u'lláh, wala haibatilishi maagizo Yake yoyote yaliyofunuliwa. Inaongeza hadhi ya mkusanyiko huo uliotukuka, inaimarisha daraja lake la juu kabisa inalinda umoja wake, inahakikisha uendelevu wa utendaji wa kazi zake, bila kudhani hata kwa kiasi kidogo kuingilia eneo lake la mamlaka lilioainishwa dhahiri. Sisi kwa hakika tupo karibu sana na waraka mkuu kama huo, kuweza kudai kuwa tuna uelewa kamili wa maana yake yote, au kudhani kuwa tumepata siri nyingi za maudhui yake yasiyo na shaka. Ni vizazi vijavyo tu ndivyo vitakavyoweza kuelewa thamani na maana inayoambatana na Kazi hii Kubwa Takatifu, ambayo mkono wa Mjenzi Mkuu wa ulimwengu umeunda kwa ajili ya uunganishaji na ushindi wa Imani ya ulimwengu mzima ya Bahá'u'lláh ya. Ni wale tu watakaokuja baada yetu ndiyo wataweza kutambua thamani ya msisitizo wa kushangaza uliowekwa juu ya asasi ya Nyumba ya Haki na ya Ulinzi.

*(Kutoka barua ya 27 Februari 1929 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, katika World Order of Bahá'u'lláh: Barua Zilizoteuliwa (Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1938, chapisho la 1991), uk. 5–8)*

33.1 Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa sawa na nguzo, pole pole na kwa uthabiti yatasimikwa katika kila nchi juu ya misingi yenye nguvu na iliyoimarishwa ya Mabaraza ya Mahali.

Juu ya nguzo hizi, jengo lenye nguvu, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, litainuliwa, likiinua juu umbo lake bora juu ya ulimwengu wa uwepo.

Umoja wa wafuasi wa Bahá'u'lláh hivyo utatambulika na kutimizwa kutoka ncha moja ya dunia hadi nyingine. Sheria dhahiri za Kitabu Chake Kitakatifu Kabisa zitatangazwa, kutatumika na kutekelezwa ipasavyo kabisa katika ulimwengu wa muumbo, na maji ya uzima wa milele yatatiririka kutoka kile kilele cha chemchemi ya Utaratibu wa Ulimwengu wa Mungu juu ya mataifa na umma wote wa ulimwengu unaopigana vita, kuondolea mbali maovu na udhalimu za milki ya vumbi, kuponya magonjwa na maradhi sugu ya mwanadamu….

33.2 Katika siku hizi vitu ambavyo vinahesabika kuwa vya umuhimu kabisa kuliko vyote na ambavyo juu yake yatategemea maendeleo ya Hoja ya Mungu, ukuzaji wa daraja na hadhi yake na uenezaji wa sheria za Imani Yake, ni kazi mbili za maana sana: ya kwanza, kuharakisha maandalizi ya uundaji wa Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki iliyoamriwa kitakatifu; ya pili, kukamilisha ujenzi wa Hekalu nchini Marekani….

33.3 … Hivyo, baada ya uundwaji wa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá'í wa nchi takatifu ya Iran—ambayo, katika Wasia na Agano, inaitwa "Nyumba ya Haki ya pili"—hatimaye maagizo ya kawaida kuhusu uchaguzi wa kimataifa wa Kibahá'í, ambao matokeo yatakuwa ni uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kufuatana na kanuni na mafundisho yaliyomo katika Nyaraka Zake na Wasia Wake na Agano, yatatumwa moja kwa moja kutoka nchi hii kwenda kwenye vituo vyote vya Kibahá'í, katika kila nchi na eneo katika Mashariki na Magharibi ya ulimwengu wa Kibahá'í. Hapo ndipo matumaini ya watu wa Bahá yatakapotambulika, na kile ambacho Bwana wetu aliamuru na kuagiza juu yetu katika Maandiko Yake na Wasia na Agano Lake kitatimia. Kisha ndipo Kiti cha Enzi cha mamlaka ya Bahá'u'lláh kitakapoasisiwa katika nchi ya ahadi na mizani ya haki kuinuliwa juu. Kisha ndipo bendera ya uhuru ya Imani itakapokunjuliwa, na Sheria Yake Kuu Kabisa kufunuliwa na mito ya sheria na kanuni kumiminika kutoka pahali hapa peupe kama theluji kwa nguvu yote ya ushindi na ukuu wote wa kuogofya, mfano ambao zama zilizopita hazijawahi kuuona kamwe. Kisha ndipo utajitokeza ukweli wa kile kilichofunuliwa na Ulimi wa Ufahari: Iite Sayuni, Ewe Carmel, na

tangaza habari njema za furaha: Yule ambaye alikuwa amefichika kutoka macho ya umauti amekuja! Enzi Yake ishindayo vyote imedhihirika; wangavu Wake ukumbatiao vitu vyote umefunuliwa." "… Ewe Carmel … Heri ni yake yule ambaye hukuzunguka wewe, yule ambaye hutangaza ufunuo wa utukufu wako, na huzungumzia kile ambacho majaliwa ya Bwana Mungu wako amenyunyizia juu yako… Muda si mrefu Mungu atatua nanga ya Safina Yake juu yako, na atawadhihirisha watu wa Bahá ambao wametajwa katika Kitabu cha Majina." Enyi wapendwa wa Mungu! Uteuzi wa Mikono wa Hoja ya Mungu, usimamizi wa sheria takatifu za Imani Yake, utungaji wa sheria dhahiri zinazotoka ndani ya maandiko ya Kitabu Chake, uitishwaji wa mkutano mkuu wa kimataifa wa wafuasi wa Hoja ya Bahá'u'lláh, na uundwaji wa mafundo kati ya jumuiya ya Kibahá'í na mawakala mbalimbali wa kisayansi, wasomi, na wa kidini na kijamii, kila mmoja wao na wote kwa pamoja, wakitegemea juu ya uundwaji na usimikwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika Nchi Takatifu katika ujirani na yale maeneo bora, maangavu na yaliyotukuka kabisa. Kwani asasi hii ya Juu Kabisa ni chemchemi ya vitendo na shughuli za Wabahá'í wote, na chanzo cha msaada na auni kwa mtumishi huyu mnyonge. Kupitia shirika hilo matumaini ya watu wa Bahá yatatimizwa. Kupitia kwake nguzo za Imani kwenye dunia hii zitasimamishwa kwa uthabiti na nguvu zake zilizofichika zitafunuliwa, ishara zake kung'aa, bendera zake kukunjuliwa na mwanga wake kutawanywa juu ya watu wote.

*(Kutoka barua ya 27 Novemba 1929 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Mashariki —ilitafsiriwa kutoka Kiarabu na Kiajemi)*

34.1 Kwa Bahá'u'lláh, tunapaswa kutambua kwa uwazi, siyo tu amewajaza wanadamu Roho mpya inayohuisha, Siyo tu ametamka baadhi ya kanuni za kiulimwegu, au kueleza falsafa mahususi, hata hizi ziwe na uwezo, za maana na za kiulimwengu namna gani. Nyogeza kwa hizi Yeye, na vile vile 'Abdu'l-Bahá baada Yake, tofauti na Vipindi vilivyopita, ameweka vifungu ya Sheria kwa uwazi na maalum, kuanzisha asasi maalum, na ametoa malekezo kwa ajili ya mahitaji mhimu ya Uchumi Mtakatifu. Haya yamekusudiwa kuwa mtindo wa jamii ya siku zijazo, chombo cha juu kabisa

kwa ajili ya uletaji wa Amani Kuu Kabisa, na chombo pekee kwa ajili ya uunganishaji wa ulimwengu, na utangazaji wa utawala wa uadilifu na haki duniani. Siyo tu wamefunua maelekezo yote yanayohitajika kwa ajili ya utambuzi wenye ufanisi wa mawazo haya ambayo Mitume wa Mungu wameyaona, na ambayo tangu nyakati zisizokumbukika yamehamasisha ubunifu wa watabiri na washahiri katika kila zama. Pia, katika lugha ya uhakika na yenye mkazo, wameteua zile asasi pacha za Nyumba ya Haki na ya Ulinzi kama Warithi wao wateule, zilizokusudiwa kutumia kanuni, kutangaza sheria, kulinda asasi, kutumia Imani kwa utiifu na akili kwa mahitaji ya jamii endelevu, na kukamilisha urithi usiorubunika ambao Waasisi wa Imani wameuzawadia ulimwengu.…

34.2 Katika Ufunuo wa Muḥammad, hata hivyo, ingawa Imani Yake ukilinganishwa na ule wa Kristo, kuhusiana na kutawala wa Kipindi Chake, ulikuwa mkamilifu zaidi na maalum zaidi katika maagizo yake, walakini katika masuala ya urithi wa madaraka, hakuna maelekezo yaliyoandikwa, hakuna maagizo yanayobana na ya mwisho kwa wale wenye dhima ya kusambaza Hoja Yake. Kwani maandiko ya Qur'án, sheria zinazohusu swala, mfungo, ndoa, talaka, mirathi, hija, na mengine kama hayo, baada ya mzunguko wa miaka elfu moja mia tatu, zimebakia zile zile na zinazofanya kazi, hazitoi muongozo mahususi kuhusu Sheria ya Urithi wa madaraka, chanzo cha mafarakano yote, ugomvi, na utengano ambavyo vimetenganisha na kuharibu sifa ya Uislám.

34.3 Siyo hivyo kwa Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Tofautti na Kipindi cha Kristo, tofauti na Kipindi cha Muḥammad, tofauti na Vipindii vyote vya zamani, mitume wa Bahá'u'lláh katika kila nchi, popote wafanyapo kazi na kusulubika, mbele yao, katika lugha ya wazi, ya uhakika na ya mkazo, wanazo amri, taratibu, kanuni, asasi, miongozo, wanazozihitaji kwa ajili ya utekelezaji na ukamilishaji wa jukumu lao. Vyote wiwili, katika mahitaji ya utawala ya Kipindi cha Kibahá'í, na katika masuala ya urithi wa madaraka, kama ilivyowekwa katika asasi pacha za Nyumba ya Haki na ya Ulinzi, wafuasi wa Bahá'u'lláh wanaweza kuitisha kwa msaada wao ushahidi wa uhakika kama huo wa Muongozo Mtakatifu ambao

hakuna anayeweza kuupinga, ambao hakuna anayeweza kuudharau wala kuupuuza. Humo ndimo zilimo sura ainishi za Ufunuo wa Kibahá'í. Humo ndimo ilimo nguvu ya umoja wa Imani, ya uhalali wa Ufunuo ambao hudai kuwa hauharibu wala kudharau Funuo zilizotangulia, bali kujiunga, kuziunganisha na kuzikamilisha. Hii ndiyo sababu Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá wote wawili wamefunua na hata kusisitiza juu ya baadhi ya tondoti kuhusiana na Uchumi Mtakatifu ambao wametuachia kama urithi, wafuasi wao. Hii ndiyo maana mkazo kama huo umewekwa katika Wasia wao na Agano juu ya uwezo na haki za wachungaji wa Imani zao.

34.4 Kwani hakuna chochote zaidi ya maelekezo dhahiri ya Kitabu chao, na lugha yenye mkazo wa kushangaza ambayo kwayo wameitumia kuvika maudhui ya Wasia wao, ambacho kingeweza kulinda Imani ambayo kwa ajili yake wote wawili wameitumikia kwa utukufu kabisa maisha yao yote. Hakuna chochote zaidi ya hiki kingeweza kuilinda kutokana na uzushi na uwongo, ambavyo kwavyo madhehebu, koo na serikali, na kwa nguvu zaidi watavitumia kuishambulia katika siku zijazo.

34.5 Pia hatuna budi tukumbuke kwamba tabia ainishi ya Ufunuo wa Kibahá'í siyo tu katika ukamilifu wake na uhalali usioweza kuhojiwa wa Kipindi ambacho mafundisho ya Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá yameweka. Ubora wake pia umo katika ukweli kwamba vile vipengele ambavyo katika Vipindi vilivyotangulia, bila idhini yoyote kutoka Waasisi wake, yamekuwa chanzo cha ufisadi na madhara yasiyokadirika kwa Imani ya Mungu, vimeachwa kabisa katika matini dhahiri ya maandiko ya Bahá'u'lláh. Zile desturi zisizohitajika, kuhusiana na sakramenti ya ubatizo, za komunio, za maungama ya dhambi, za utawa, za ukandamizaji wa kikasisi, za sherehe za kifahari, za vita vitakatifu na za mitala, kimoja kimoja na vyote kwa jumla vimekatazwa katakata na Kalamu ya Bahá'u'lláh; ambapo msimamo na ukali wa baadhi ya sheria kama vile mfungo, ambayo ni ya lazima kwa maisha ya kiibada ya mtu binafsi, vimepunguzwa sana.

*(Kutoka barua ya 21 Machi 1930 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, katika World Order of Bahá'u'lláh, uk. 19–22)*

35.1 Kizazi chetu cha sasa, hasa kutokana na ufisadi ambao unajiainishwa na mashirika, kinaonekana kusimama dhidi ya asasi yoyote. Dini kama asasi inashutumiwa. Serikali kama asasi inashutumiwa. Hata ndoa kama asasi inashutumiwa. Sisi Wabahá'í tusipofushwe na dhana kama hizo zinazoendelea. Kama hali ingekuwa hivyo, Wadhihirishaji wote watakatifu daima wasingemteua mtu wa kuwarithi. Pasipo na shaka ufisadi uliingia katika asasi hizo, lakini ufisadi huu haukutokana na asili yenyewe ya asasi hizo bali kwa ukosefu wa maelekezo yanayofaa juu ya uwezo wao na asili ya uendelezaji wao. Kile Bahá'u'lláh alichofanya siyo kuziondoa asasi zote katika Hoja bali kuzipatia kinga zilizohitajika ambazo zingeondoa ufisadi uliosababisha kuanguka kwa asasi zilizotangulia. Kinga hizo ni nini, ni jambo la kuvutia sana kujifunza na kutafiti na pia ni muhimu sana kulifahamu. Katika barua ambayo Shoghi Effendi ameandika hivi karibuni kwa marafiki wa Magharibi, yeye anataja sura ainishi za asasi ambayo Bahá'u'lláh ametuachia na vile vile kiasi fulani cha kinga Alizoweka dhidi ya ufisadi wake. Mojawapo ya vitu vikubwa tunavyojivunia ni kwamba wakati dini zilizotangulia kwa namna fulani zilikuwa tuli katika asili zao, mafundisho ya Kibahá'í ni endelevu. Sasa, ingewezaje muelekeo huu wa uendelevu kudumishwa bila asasi kama vile Ulinzi na Nyumba ya Haki, ambazo zinawezeshwa kutunga sheria juu ya masuala ambayo hayakurejelewa na Bahá'u'lláh?
*(Kutoka barua ya 25 Machi 1930 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

36.1 Umeuliza kuhusu hadhi ya serikali mbalimbali pale Nyumba ya Haki itakaposimikwa: hili halijaelezwa kikamilifu katika mafundisho, na kile ambacho hakijatolewa mahususi, ni juu ya Nyumba ya Haki kukitungia sheria mara shirika hilo litakapoundwa.
*(Kutoka barua ya 12 Januari 1933 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

37.1 Nyumba ya Haki, kufuatana na maandiko dhahiri ya Aqdas, haina haki ya kubadilisha sheria yoyote, taratibu au kanuni ambazo zimefunuliwa katika Aqdas au katika Waraka wowote kutoka Kalamu ya Bahá'u'lláh.

Inaweza kubadilisha kanuni yake yenyewe na sheria lakini kamwe siyo zile zilizofunuliwa na Mwasisi wa Imani.
*(Kutoka barua ya 17 Juni 1933 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

38.1 Katika Nyaraka za Bahá'u'lláh ambamo asasi za Nyumba ya Haki ya Kimataifa na za Mahali zimeainishwa mahususi na kusimikwa rasmi; katika asasi ya Mikono wa Hoja ya Mungu ambayo mwanzoni Bahá'u'lláh na baadaye 'Abdu'l-Bahá walianzisha; katika asasi zote mbili, Mabaraza ya Mahali na ya kitaifa ambazo katika hatua yao ya utungo tayari zilikuwa zinafanya kazi kipindi kabla ya kupaa kwa 'Abdu'l-Bahá; katika mamlaka ambayo kwayo Mtunzi wa Imani yetu na Kitovu cha Agano Lake wamechagua kutoa kwao katika Nyaraka zao; katika asasi ya Hazina ya Mahali ambayo ilifanya kazi kufuatana na maagizo maalum ya 'Abdu'l-Bahá yaliyoandikwa kwa baadhi ya Mabaraza ya Uajemi; katika aya za Kitáb-i-Aqdas athari ambazo kwa uwazi zinaitarajia Asasi ya Ulinzi; katika maelezo ambayo 'Abdu'l-Bahá, katika mojawapo ya Nyaraka Zake, aliyoyatoa, na msisitizo Alioweka juu yake, kanuni ya kurithi na sheria ya mtoto wa kwanza kama ilivyotumiwa na Manabii wa kale—katika hizi tunaweza kuona katika mwangaza hafifu na kugundua fununu ya mapema kabisa ya asili na utendaji kazi wa Utaratibu wa Kiutawala ambao Wasia wa 'Abdu'l-Bahá hapo baadaye ulikusudiwa kutangazwa na kusimikwa rasmi.

38.2 Ninadhani, jaribio kwa kipindi hiki lifanywe kuelezea tabia na utendaji wa nguzo pacha zinazohimili Muundo huu wenye nguvu wa Utawala, Asasi ya Ulinzi na ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Kuelezea kikamilifu kabisa vipengele mbalimbali vinavyofanya kazi kwa uwiano na Asasi hizi ni zaidi ya upeo na makusudi ya maelezo haya ya jumla ya kweli za kimsingi za Imani. Kuelezea kwa usahihi na kwa sura ndogo ndogo, na kutanabaisha kabisa asili ya uhusiano ambao, kwa upande mmoja, hufungamanisha pamoja vyombo hivi viwili vya kimsingi vya Wasia wa 'Abdu'l-Bahá na kuunganisha kwa upande mwingine, kila moja yao kwa Mtunzi wa Imani na Kitovu cha Agano Lake ni kazi ambayo

vizazi vijavyo bila shaka vitaikamilisha kikamilifu. Kusudi langu la wakati huu ni kufafanua baadhi ya sura zinazojitokeza za utaratibu huu, ambazo, hata tukisogea karibu sana kwenye muundo wake mkubwa mno, tayari vimeeleza kwa uwazi kabisa kiasi kwamba hatupati kisingizio cha kutoelewa ama kupuuzia.

38.3 Inabidi itamkwe, tangu mwanzoni kabisa, katika lugha ya wazi na isiyojikanganya, kwamba hizi Asasi za Utaratibu wa Kiutawala wa Bahá'u'lláh zinapaswa zichukuliwe kama takatifu katika asili, muhimu katika kazi zao na zinazokamilishana katika shabaha na kusudi lao. Lengo lao la pamoja, lao la msingi ni kuhakikisha muendelezo wa ile mamlaka iliyoteuliwa kitakatifu ambayo hutiririka kutoka Chanzo cha Imani yetu, kulinda umoja wa wafuasi wake na kudumisha uadilifu na unyumbulifu wa mafundisho yake. Zikitendakazi kwa muingiliano wa mmoja kwa mwingine asasi hizi zisizotenganika huendesha mambo yao, huratibu shughuli zao, hukuza raghba zake, hutekeleza sheria zake na kutetea asasi zake saidizi. Mara kadhaa, kila moja hutendakazi ndani ya eneo lake lenye mipaka dhahiri ya kiutawala; kila moja likiwa limejidhatiti barabara kwa asasi saidizi zake lenyewe—vitendeakazi vilivyosarifiwa kwa ajili ya utekelezaji wenye ufanisi wa wajibu na majukumu yao mahususi. Kila moja hutumia, ndani ya mipaka iliyoamriwa juu yake, nguvu zake, mamlaka yake, haki na stahili zake. Hizi hazipingani, wala kukinzana hata kwa kiwango kidogo kabisa kwa nafasi ambayo kila mojawapo ya asasi hizi hushika. Mbali na kutoendana au kuharibiana, zinajalizana kwenye mamlaka na kazi za kila mmoja, na daima na kimsingi zimeungana katika shabaha zao.

38.4 Ukichepushwa kutoka kwenye asasi ya Ulinzi Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh ungekatishwa na kunyimwa moja kwa moja ile kanuni ya urithi ambayo, kama ambavyo 'Abdu'l-Bahá ameandika, imeendelea kushikiliwa na Sheria ya Mungu. "Katika Vipindi vyote Vitakatifu," Yeye hutamka, katika waraka alioandikiwa mfuasi mmoja wa Imani huko Uajemi, "mtoto mkubwa kabisa wa kiume amepewa upekee usio wa kawaida. Hata daraja la unabii limekuwa haki yake ya kuzaliwa."

Bila asasi kama hiyo uadilifu wa Imani ungewekwa rehani, na utengamano wa mfumo mzima ungehatarishwa kabisa. Hadhi yake ingeumia, nyenzo zihitajikazo kuuwezesha uchukue taswira ya muda mrefu, isiyoweza kuingiliwa kwa mfululizo wa vizazi zingeweza kukosekana kabisa, na muongozo muhimu wa kufafanua mipaka ya eneo la kisheria la wawakilishi wake wa kuchaguliwa lingeweza kuondolewa kabisa.

38.5 Ukiondolewa kutoka kwenye asasi yenye umuhimu mkubwa ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu Mfumo huu huu wa Wasia wa ‘Abdu’l-Bahá ungeweza kunyong’onyezwa katika utendaji wake na ungekuwa hafifu kujazia yale mapengo ambayo Mtunzi wa Kitáb-i-Aqdas ameyaacha kwa makusudi katika ule muundo wa sheria Zake za uwekaji misingi ya kiutawala.
*(Kutoka barua ya 8 Februari 1934 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, katika World Order of Bahá’u’lláh, kur. 147–148)*

39.1 Utaratibu wa Utawala wa Imani ya Bahá’u’lláh kwa vyovyote vile sharti usichukuliwe kama wa kidemokrasia kabisa katika sifa kwa kuwa ile dhana ya kimsingi ambalo linawataka wanademokrasia wote kutegemea kimsingi katika kupata mamlaka yao kutoka kwa watu linakosekana kabisa katika Kipindi hiki. Katika uendeshaji wa masuala ya kiutawala ya Imani, katika utungaji wa sheria muhimu katika kujaliza sheria za Kitáb-i-Aqdas, wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, inapaswa izingatiwe, kama matamshi ya Bahá’u’lláh yanavyoashiria wazi, hawawajibiki kwa wale wanaowawakilisha, wala hawaruhusiwi kutawaliwa na hisia, mtazamo wa jumla, na hata ushawishi wa umma wa waaminifu, au wa wale wanaowachagua moja kwa moja. Watatakiwa kufuata, katika hali ya sala, muongozo na ushawishi wa utashi wao. Wanaweza, hakika inawalazimu, wajizoeze wenyewe na hali iliyopo ndani ya jamii, lazima wapime bila upendeleo akilini mwao manufaa ya hoja yoyote inayowasilishwa kwao kwa ajili ya maamuzi yao, lakini lazima wajihifadhie ile haki ya uamuzi usiofungamana. “Mungu kwa hakika atawavuvia kwa chochote kile Atakacho,” ni uhakikisho usiopingika wa Bahá’u’lláh. Ni wao, hivyo, na siyo kundi la wale ambao huwachagua ama kwa njia ya moja kwa moja

au isiyo ya moja kwa moja, ambao wamefanywa kuwa wapokeaji wa muongozo mtakatifu ambao papo hapo ni damu ya uhai na ndiyo kinga ya mwisho ya Ufunuo huu.
*(Kutoka barua ya 8 Februari 1934 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, katika World Order of Bahá'u'lláh, uk. 153)*

40.1 Lakini, kwa sasa hivi—na kwa hili Mlinzi anataka umakini wenu wa uangalifu—hakuna Baraza linaloweza, wala hata yeye mwenyewe anaweza kuwa na haki ya kutunga sheria yoyote kujaliza zile za Aqdas isipokuwa katika mazingira ya kipekee pale Mamlaka zinapohitaji hilo. Na hata katika hali kama hiyo utungaji huo ni wa muda mfupi kabisa. Chombo pekee ambacho kimepewa nguvu kutunga sheria katika masuala kama hayo ni Nyumba ya Haki ya Kimataifa, na Mlinzi anaweza tu kushiriki katika utungaji huo wa sheria kwa hadhi yake kama mjumbe wa chombo hicho. Kama ambavyo ile nguvu ya kufasiri Maandiko ni haki ya Mlinzi pekee, ndivyo ilivyo pia nguvu ya utungaji sheria imewekwa na Bahá'u'lláh kipekee katika Nyumba ya Haki ya Kimataifa. Hivyo, kuna utofauti wa wazi kati ya nguvu za utungaji sheria na ufasiri, ingawa vyote viwili vinahusiana kwa ukaribu.
*(Kutoka barua ya 6 Julai 1935 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

41.1 Kati ya mahitaji haya ya kiroho ya mafanikio, ambayo hufanya msingi ambao juu yake usalama wa mipango yote ya ufundishaji, Miradi ya Mahekalu na miundo ya kifedha, lazima hatimaye viwekwe, kifuatacho kinajitokeza kama kinara na umuhimu …. Mahitaji haya si mengine bali ni hisia ya juu ya unyofu wa kimaadili katika shughuli zao za kijamii na za kiutawala, ubikira kabisa katika maisha yao binafsi, na uhuru kamili kutokana na chuki katika shughuli zao na watu wa mbari, tabaka, imani au rangi tofauti.

41.2 La kwanza, japokuwa siyo kipekee, limeelekezwa kianga kwa wawakilishi wao wa kuchaguliwa, iwe ngazi ya mahali, kanda au kitaifa, ambao, katika wadhifa wao kama waangalizi na wajumbe wa asasi changa

za Imani ya Bahá'u'lláh, wanabeba jukumu kuu katika kuweka msingi usioweza kutikiswa kwa ajili ya ile Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo, kama jina lake linavyoashria, itakuja kuwa mwakilishi na mlinzi wa ile Haki Takatifu ambayo inaweza peke yake kuhakikisha usalama na kusimika utawala wa sheria na utaratibu katika ulimwengu uliovurugika kiajabu-ajabu.
*(Kutoka barua ya 25 Desemba 1938 iliyoandikwa na Shoghi Effendi, The Advent of Divine Justice (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2006, chapishao la 2018), uk. 32–33)*

42.1 Katika uwanda wa 'Akká ndipo kuna Kimbilio lililobarikiwa na takatifu la Uzuri Mtakatifu Kabisa wa Abhá, Kiini ambacho huzungukwa na Umati wa juu, Kibla ya watu wa Bahá na wakazi wa Safina Nyekundu, Moyo wa ulimwengu na Kaaba ya mataifa yote. Na kwenye Mlima Carmel pana Makaburi pacha matakatifu na yaliyotukuka, kiti cha enzi kilichotakaswa cha Yule Mtukufu Nukta ya Kuu, na mabaki maangavu ya Yeye Ambaye majina yote humzunguka—Chimbuko la Miangaza, penye Mkusanyiko wa Mafumbo, Chanzo cha Neema tele kwa wanadamu. Pembezoni mwa sehemu hizi tatu takatifu za mapumnziko—makaburi ya Shina na Masalia Yake3, na ya wadhamini pacha Watakatifu, Tawi Safi Tukufu Kabisa na Mama wa 'Abdu'l-Bahá—kitovu cha utawala wa jamii ya watu wa Bahá, baada ya hapa, kitawekwa polepole. Karibu kabisa na Makaburi hayo nguzo za ile Mahakama ya Haki Takatifu zitainuliwa,

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itasimikwa, na jengo la Mashriqu'l-Adhkár la Nchi Takatifu litainuliwa, ambapo katika kivuli cha kikingacho cha Vituo pacha hivi vya watu wa Mungu4 shughuli tukufu na utawala wa kimataifa, asasi za kisayansi na za kijamii za Imani ya Kibahá'í zitapata umbo, kiti cha enzi cha Ufalme wa Mungu kitasimikwa, bendera ya "Yá Bahá'u'l-Abhá" itapandishwa juu ya vilele vya juu kabisa, na ngurumo za radi za umoja wa wanadamu zitasikika. Hapo kitatimizwa kile kilichokuwa kimefunuliwa katika Waraka wa Carmel na Kalamu yenye utukufu wote na angavu kabisa: "Muda si mrefu Mungu atatua nanga ya Safina Yake juu

yeko, na atawadhihirisha watu wa Bahá ambao wametajwa katika Kitabu cha Majina."

*(Kutoka barua ya 25 Desemba 1939 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Mashariki—iiliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

43.1 Kuwa mjumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kumewekwa kwa ajili ya wanaume tu. Kuweka idadi ya wajumbe, taratibu za uchaguzi na kipindi cha kuwa mjumbe vitajulikana baadaye, kwa kuwa haya hayakufunuliwa wazi wazi katika Andiko Takatifu.

*(Kutoka barua ya 27 Mei 1940 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

---

[3]*Bahíyyih Khánum, Jani Takatifu Kuu Kabisa*

44.1 Hakuna anayeweza kuongezea kwenye sheria za Kipindi cha Kibahá'í ispokuwa Nyumba ya Haki ya Kimataifa. Mabaraza ya Kitaifa kwa sasa yanatunga tu mbinu za utaratibu wa kurahisisha utendaji kazi wa Utaratibu wa Kiutawala na kuhakikisha uendeshaji wenye ufanisi wa shughuli za Hoja ndani ya mipaka yao ya kimamlaka. Hizi zinaweza kuondolewa au kurekebishwa wakati wowote zinapokuwa zimepoteza manufaa yake au mbinu nyingine itakayokuwa yenye ufanisi zaidi.
*(Kutoka barua ya 19 Desemba 1943 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa waumini wawili)*

45.1 Kuna asasi mbili tu ambazo ziko huru kutokana na makosa, moja ni ile ya Ulinzi, nyingine Nyumba ya Haki ya Kimataifa.
*(Kutoka barua ya 19 Oktoba 1947 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

46.1 Kwanza, acha niseme kwamba moja ya sababu Mungu ametupatia asasi ya Ulinzi ni kuwazuia watu kutokana na kuishupaza Hoja kuwa mfumo uliokakamaa. Maswali yako kwa kiasi kikubwa yapo kwenye mstari wa kujaribu kuweka muundo usionyumbulika kwa jamii ya baadaye, mapema kabisa kabla muda kwa ajili ya muundo kama huo kupevuka. Kumbuka kwamba Bahá'u'lláh husema kile ambacho bado hakijafunuliwa, Nyumba ya Haki ya Kimataifa lazima siku zijazo ikitungie sheria, na inaweza kuzitunga na kuzifuta kama ni lazima, sheria zake yenyewe. Hii humaanisha kutoshupaa katika kuongoza jamii, bali kunyumbulika.
*(Kutoka barua ya 31 Machi 1949 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)*

47.1 Ninasali kwa bidii kwamba ushiriki wa kipekee wa Mabaraza ya Kitaifa ya Uingereza, Marekani, Uajemi na Misri, katika shughuli ya kuanza kipindi kipya cha kihistoria katika bara la Afrika iweze kuthibitisha mwanzo wa mkutano wa kwanza wa Kongamano la Ufundishaji barani Afrika ambalo hatimaye ni uanzishwaji wa shughuli zinazohusisha ushirikiano miongoni mwa mabaraza yote ya kitaifa ya ulimwengu wa

Kibahá'í, hivyo kuandaa njia kwa muunganiko wa mwisho ulio hai wa mabaraza haya kupitia uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa inayokusudiwa kuzindua shughuli zinazokumbatia ulimwengu mzima wa Kibahá'í. Karibisheni uzinduzi wa pambano la kiroho linalofungamanisha utendaji wa kiutawala wa mabaraza manne ya kitaifa ya Mashariki na Magharibi ndani ya mabara manne unaoenda sambamba na kuzaliwa kwa Halmashauri ya kwanza ya Kimataifa kwenye Makao Makuu ya Imani Ulimwenguni, ushahidi pacha wa mkunjuko wa utungo usiozuilika wa Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh, uliowekwa kitakatifu.
*(Kutoka waraka wa 17 Januari 1951 ulioandikwa na Shoghi Effendi, katika Citadel of Faith: Jumbe kwa Marekani 1947–1957 (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1965, chapisho la 2014), uk. 90)*

48.1 Juu ya mafanikio ya shughuli hii, isiyopitwa katika wigo wake, ya kipekee katika mwenendo wake na kubwa mno katika nguvu zake za kiroho, sharti utegemee uanzishwaji, kwenye kipindi cha baadaye katika Zama za Utungo wa Imani, wa shughuli zinazokumbatia ndani ya upana wake Mabaraza yote ya Kitaifa yakifanya kazi katika Ulimwengu mzima wa Kibahá'í—shughuli zenye kujumuisha ndani yake maandalizi kwa ajili ya uzinduzi wa shughuli za ulimwengu mzima zinazotazamiwa kuanzishwa, katika vipindi vijavyo vya Zama hiyo hiyo, na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambazo zitaashiria umoja na kuratibu na kuunganisha shughuli za Mabaraza haya ya Kitaifa.
*(Kutoka nyongeza iliyowekwa na Shoghi Effendi iliyoambatanishwa kwenye barua ya 25 Februari 1951 iliyoandikwa kwa niaba yake kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Visiwa vya Uingereza)*

---

[4]*Makaburi Pacha Matakatifu huko Akka na Haifa*

49.1 Katika Waraka huu Mkuu [wa Carmel] ambao hufunua mafumbo matakatifu na hutangulia uanzishwaji wa shughuli mbili kuu, za kifahari na za kihistoria—mojawapo ikiwa ya kiroho na nyingine ya kiutawala, zote mbili kwenye Makao Makuu ya Imani ya Ulimwengu—Bahá'u'lláh hurejelea kwenye "Safina", ambayo wakazi wake ni wanaume wa Nyumba Juu Kabisa ya Haki, ambayo, kwa kufuatana na matakwa halisi ya Wasia na Agano la Kitovu cha Agano lenye Uwezo, ndilo shirika ambalo linapaswa liweke sheria ambazo hazikufunuliwa wazi katika Maandiko. Katika Kipindi hiki, sheria hizi zinatazamiwa kutiririka kutoka kwenye Mlima huu Mtakatifu, kama vile katika Kipindi cha Musa sheria za Mungu zilivyotangazwa kutoka Sayuni. Kule "kutua nanga kwa Safina" ya sheria Zake ni rejeleo la uanzishwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo kwa hakika ndiyo Kiti cha Utungaji Sheria, mojawapo ya matawi ya Kitovu cha Kiutawala cha Ulimwengu cha Wabahá'í juu ya Mlima huu Matakatifu.

*(Kutoka barua ya 21 Machi 1954 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Mashariki—iiliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

50.1 Enyi wapendwa wa Bahá! Siku hii ni siku yenu na saa hii hakika ni saa yenu. Kile ambacho ni shuruti katika siku hii na ambacho, kama vile sumaku, kitavutia thibitisho wa Mungu ni hiki, kwamba idadi kubwa ya waumini, waume kwa wake, vijana kwa wazee, matajiri kwa masikini, wasomi kwa wasiosoma, weupe kwa weusi kadhalika, wajiandae kwa ajili ya ushindi wa Imani Yake iliyotukuka. Wakihuishwa kwa roho ya upendo na ujasiri, lazima, mmoja mmoja na wote, wainuke kama vile jeshi moja, na katika kipindi cha miaka tisa iliyobaki watawanyike kwa marefu na mapana juu ya uso wa dunia. "Kwa miguu ya kujitenga," kama Uzuri wa Kale anavyoonya, wao lazima "watembee chini ya wote walioko mbinguni na duniani" na "watandaze kitambaa cha utakatifu juu ya vyote vilivyoumbwa kutoka kwenye maji na udongo wa mfinyanzi." Kwa mioyo iliyojitenga, nafsi zisizojiambatanisha, roho zilizowashwa, azma isiyojivuta na hatua zisizositasita, lazima wajibidiishe mchana na usiku kusogeza sehemu za kufikika Hoja ya Mungu, kusambaza manukato

yake mazuri, kuimarisha misingi yake, kupaza sauti ya umaarufu wake hadi ng'ambo na kuzidisha safu za wafuasi wake. Wakiinua wito wa "Yá Bahá'u'l-Abhá!" lazima waharakie mbele kwenye majimbo ambayo hayajaguswa na maeneo yaliyofunguliwa hivi karibuni na, wakiweka matumaini yao yote kwa Mungu, waanzishe vituo vilivyo peke yake, ambavyo vinaweza kufananishwa na "vinukta". Lazima, kupitia jitihada zao za kufundisha na kuongoza watu kwa maneno na vitendo, wavigeuze vituo hivi vya peke yake mapema kadiri iwezekanavyo, kuwa vikundi, ambavyo vimefananishwa na "herufi". Kisha lazima waviendeleze vikundi hivi kuwa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali, ambayo ni kama "maneno" kamilifu, na waendelee kujitahidi kuongeza idadi ya Mabaraza haya katika nchi mbalimbali ili kwamba nyenzo kwa ajili ya uitishaji unaofaa wa Mikutano Mikuu ya Kitaifa pole pole ziweze kuandaliwa, Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, ambayo ni kama "aya" zilizo dhahiri, nguzo za Kiti cha Enzi cha Haki Takatifu, yaweze kuinuliwa kiutaratibu, na juu ya nguzo hizi liweze kuinuliwa kuba la Jengo takatifu, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo ni kama "kitabu" fasaha, kilichosimikwa mahali pake pateule kwenye miteremko ya Shamba la Mizabibu la Bwana juu ya Mlima Wake Mtakatifu, kikizipamba asasi za Utaratibu Wake Mpya wa Ulimwengu kwa taji  la upekee wa juu kabisa.

*(Kutoka barua ya 21 Machi 1954 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Mashariki—kilichotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

[4]*Makaburi Pacha Matakatifu huko Akka na Haifa*

49.1 Katika Waraka huu Mkuu [wa Carmel] ambao hufunua mafumbo matakatifu na hutangulia uanzishwaji wa shughuli mbili kuu, za kifahari na za kihistoria—mojawapo ikiwa ya kiroho na nyingine ya kiutawala, zote mbili kwenye Makao Makuu ya Imani ya Ulimwengu—Bahá'u'lláh hurejelea kwenye "Safina", ambayo wakazi wake ni wanaume wa Nyumba Juu Kabisa ya Haki, ambayo, kwa kufuatana na matakwa halisi ya Wasia na Agano la Kitovu cha Agano lenye Uwezo, ndilo shirika ambalo linapaswa liweke sheria ambazo hazikufunuliwa wazi katika Maandiko. Katika Kipindi hiki, sheria hizi zinatazamiwa kutiririka kutoka kwenye Mlima huu Mtakatifu, kama vile katika Kipindi cha Musa sheria za Mungu zilivyotangazwa kutoka Sayuni. Kule "kutua nanga kwa Safina" ya sheria Zake ni rejeleo la uanzishwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo kwa hakika ndiyo Kiti cha Utungaji Sheria, mojawapo ya matawi ya Kitovu cha Kiutawala cha Ulimwengu cha Wabahá'í juu ya Mlima huu Matakatifu.

*(Kutoka barua ya 21 Machi 1954 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Mashariki—iiliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

50.1 Enyi wapendwa wa Bahá! Siku hii ni siku yenu na saa hii hakika ni saa yenu. Kile ambacho ni shuruti katika siku hii na ambacho, kama vile sumaku, kitavutia thibitisho wa Mungu ni hiki, kwamba idadi kubwa ya waumini, waume kwa wake, vijana kwa wazee, matajiri kwa masikini, wasomi kwa wasiosoma, weupe kwa weusi kadhalika, wajiandae kwa ajili ya ushindi wa Imani Yake iliyotukuka. Wakihuishwa kwa roho ya upendo na ujasiri, lazima, mmoja mmoja na wote, wainuke kama vile jeshi moja, na katika kipindi cha miaka tisa iliyobaki watawanyike kwa marefu na mapana juu ya uso wa dunia. "Kwa miguu ya kujitenga," kama Uzuri wa Kale anavyoonya, wao lazima "watembee chini ya wote walioko mbinguni na duniani" na "watandaze kitambaa cha utakatifu juu ya vyote vilivyoumbwa kutoka kwenye maji na udongo wa mfinyanzi." Kwa mioyo iliyojitenga, nafsi zisizojiambatanisha, roho zilizowashwa, azma isiyojivuta na hatua zisizositasita, lazima wajibidiishe mchana na usiku kusogeza sehemu za kufikika Hoja ya Mungu, kusambaza manukato

yake mazuri, kuimarisha misingi yake, kupaza sauti ya umaarufu wake hadi ng'ambo na kuzidisha safu za wafuasi wake. Wakiinua wito wa "Yá Bahá'u'l-Abhá!" lazima waharakie mbele kwenye majimbo ambayo hayajaguswa na maeneo yaliyofunguliwa hivi karibuni na, wakiweka matumaini yao yote kwa Mungu, waanzishe vituo vilivyo peke yake, ambavyo vinaweza kufananishwa na "vinukta". Lazima, kupitia jitihada zao za kufundisha na kuongoza watu kwa maneno na vitendo, wavigeuze vituo hivi vya peke yake mapema kadiri iwezekanavyo, kuwa vikundi, ambavyo vimefananishwa na "herufi". Kisha lazima waviendeleze vikundi hivi kuwa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali, ambayo ni kama "maneno" kamilifu, na waendelee kujitahidi kuongeza idadi ya Mabaraza haya katika nchi mbalimbali ili kwamba nyenzo kwa ajili ya uitishaji unaofaa wa Mikutano Mikuu ya Kitaifa pole pole ziweze kuandaliwa, Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, ambayo ni kama "aya" zilizo dhahiri, nguzo za Kiti cha Enzi cha Haki Takatifu, yaweze kuinuliwa kiutaratibu, na juu ya nguzo hizi liweze kuinuliwa kuba la Jengo takatifu, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo ni kama "kitabu" fasaha, kilichosimikwa mahali pake pateule kwenye miteremko ya Shamba la Mizabibu la Bwana juu ya Mlima Wake Mtakatifu, kikizipamba asasi za Utaratibu Wake Mpya wa Ulimwengu kwa taji  la upekee wa juu kabisa.

*(Kutoka barua ya 21 Machi 1954 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í wa Mashariki—kilichotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

**Kutoka katika Katiba na Barua za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu**

51.1 Bahá'u'lláh, Mfunuaji wa Neno la Mungu katika Siku hii, Chanzo cha Mamlaka, Kilele cha Chemchemi ya Haki, Muumbaji wa Utaratibu mpya wa Ulimwengu, Mwanzilishi wa Amani Kuu Kabisa, Mvuviaji na Muasisi wa ustaarabu wa ulimwengu, Jaji, Mtoa Sheria, Muunganishaji na Mkombozi wa wanadamu wote, ametangaza ujio wa Ufalme wa Mungu duniani, ametunga sheria na amri zake, amezitaja kanuni zake, na kuamuru asasi zake. Kuziongoza na kuzielekeza nguvu iliyoachiliwa na Ufunuo Wake, alianzisha Agano Lake, ambalo nguvu yake imeuhifadhi uadilifu wa Imani Yake, imeudumisha umoja wake na kuchochea upanuzi wake kote ulimwenguni kupitia mfuatano wa utumishi wa 'Abdu'l-Bahá na Shoghi Effendi. Inaendelea kutimiza kusudi lake litialo uzima kupitia utendaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo lengo lake la msingi, kama mmoja wa warithi pacha wa Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá, ni kuhakikisha muendelezo wa yale mamlaka yaliyoteuliwa-kitakatifu ambayo hutiririka kutoka Chanzo cha Imani, kulinda umoja wa wafuasi wake na kudumisha uadilifu na unyumbulifu wa mafundisho yake.
*(The Constitution of the Universal House of Justice (Haifa: Makao Mkuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu, 1972), pg. 3–4)*

52.1 Asili, mamlaka, majukumu, wigo wa kiutendaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu vyote vimetokana na Neno lililofunuliwa la Bahá'u'lláh ambalo, kwa pamoja na fasiri na ufafanuzi wa Kitovu cha Agano na ule wa Mlinzi wa Hoja—ambaye, baada ya 'Abdu'l-Bahá, ndiye mamlaka pekee katika kufasiri Maandiko ya Kibahá'í—vinaunda hadidu za rejea za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na ndiyo msingi wake wa mwamba. Mamlaka ya Maandiko haya ni kamilifu na hayabadiliki mpaka wakati huo ambapo Mwenyezi Mungu atakamfunua Mdhihirishaji Wake mpya Ambaye mamlaka yote na nguvu vitakuwa Vyake.

52.2 Kule kutokuwepo mrithi kwa Shoghi Effendi kama Mlinzi wa Hoja ya Mungu, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ndiyo Kichwa cha Imani na asasi yake ya juu kabisa, ambayo kwake wote lazima wageukie, na juu

yake upo wajibu wa mwisho kabisa kwa ajili ya kuhakikisha umoja na maendeleo ya Hoja ya Mungu.
*(The Constitution of the Universal House of Justice, pg. 4)*

53.1 Miongoni mwa nguvu na majukumu ambayo kwayo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imepewa ni: Kuhakikisha uhifadhi wa Maandiko Matakatifu na kulinda kutopotoshwa kwake; kuchambua, kuainisha na kuratibu Maandiko; na kuitetea na kuilinda Hoja ya Mungu na kuikomboa kutokana minyororo ya uonevu na mateso.

Kuendeleza raghba ya Imani ya Mungu; kutangaza, kusambaza na kufundisha Ujumbe wake; kupanua na kuimarisha asasi za Utaratibu wake wa Kiutawala; kuukaribisha Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh; kukuza ufikiwaji wa zile njema za kiroho ambazo zinapaswa zipambanue maisha ya Kibahá'í ya binafsi na ya pamoja; kufanya kila iliwezalo kwa ajili ya upatikanaji wa ukunjufu na uhusiano mkubwa zaidi wa kirafiki miongoni mwa mataifa na kwa ajili ya ufikiaji wa amani ya ulimwengu; na kuimarisha kile ambacho kina uwezo wa kupitisha wongofu na wangavu wa roho za watu na uendelezaji na uboreshaji wa ulimwengu;

Kutunga sheria na kanuni ambazo hazikuandikwa wazi wazi katika Maandiko Matakatifu; kubatilisha sheria zake yenyewe kulingana na mabadiliko na matakwa ya wakati; kujadili na kuamua juu ya matatizo yote ambayo yamesababisha mifarakano; kufafanua masuala yenye utata; kulinda haki, uhuru na ubunifu wa watu binafsi na kumakinikia kwenye uhifadhi wa heshima ya mwanadamu, kwenye maendeleo ya nchi na utengamano wa madola;

Kuzitangaza na kuzitumia sheria na kanuni za Imani; kulinda na kusimamia ule unyofu wa tabia ambao Sheria ya Mungu huamuru; kuhifadhi na kuendeleza Kituo cha Kiroho na Kiutawala cha Imani ya Kibahá'í, kilichowekwa kwa kudumu katika miji pacha ya 'Akká na Haifa; kusimamia shughuli za jamii ya Kibahá'í kote ulimwenguni; kuongoza, kupanga, kuratibu na kuunganisha shughuli zake; kuanzisha

asasi; kuwajibika kwa kuhakikisha kwamba hakuna mtu au asasi ndani ya Hoja anayebeza haki zake au kulegea katika utekelezaji wa haki na stahili zake; na kuweka utaratibu kwa ajili ya upokeaji, utumiaji, usimamizi na ulindaji wa fedha, mali wakfu na mali zingine ambazo zipo chini ya uangalizi wake;

Kuamua migogoro inayoangukia ndani ya eneo lao; kutoa hukumu katika mashauri ya uvunjifu wa sheria za Imani na kutamka adhabu kwa uvunjifu huo; kuweka utaratibu kwa ajili ya kusimamia maamuzi yake; kuweka utaratibu kwa ajili ya upatanishi na usuluhishi wa migogoro inayoibuka kati ya jamii za watu; na kuwa mwakilishi na mlinzi wa ile Haki Takatifu ambayo pekee ndiyo inaweza kuhakikisha usalama na kuweka utawala wa sheria na utaratibu ulimwenguni.
*(The Constitution of the Universal House of Justice, pg. 5–6)*

54.1 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilichaguliwa kwa mara ya kwanza kwenye siku ya kwanza ya Siku kuu ya Riḍván katika mwaka wa mia moja na ishirini wa Zama za Kibahá'í5, wakati wajumbe wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, kufuatana na maagizo ya Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá, na kwa kuitikia wito wa Mikono wa Hoja ya Mungu, Wakadamu Wakuu wa Dola changa la Ulimwengu wa Bahá'u'lláh, lililoleta huu "uvikwaji wa taji la utukufu" wa asasi za kiutawala za Bahá'u'lláh, "kiini na kitangulizi" chenyewe cha Utaratibu Wake wa Ulimwengu. Sasa, kwa hiyo, katika kutiifu Amri ya Mungu na kwa utegemezi kamili juu Yake, sisi, wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, tunaweka mikono yetu na muhuri wake kwenye Tangazo hili la Wadhamini ambalo, pamoja na Sheria Ndogo zilizoambatishwa hapa, vinaunda Katiba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.
*(The Constitution of the Universal House of Justice, pg. 6–7)*

55.1 Agano la Bahá'u'lláh halikuvunjwa, nguvu zake zikumbatiazo vyote hazikukiukwa. Zile sura mbili za kipekee zinazolitofautisha kutoka maagano yote ya kidini ya nyakati zilizopita hazijabadilishwa na zinatenda kazi. Neno lililofunuliwa, katika usafi wake wa asili, likiongezewa na

fasiri zilizoongozwa kitakatiufu za ‘Abdu’l-Bahá na Shoghi Effendi, hubakia lisilobadilika, lisilochafuliwa na kanuni au mifumo yoyote ya imani ya kutengenezwa na watu, mawazo yasiyoruhusiwa au fasiri zisizo na mamlaka. Njia ya muongozo mtakatifu, ikitoa unyumbulifu katika shughuli zote za mwanadamu, inabakia wazi kupitia ile Asasi ambayo iliasisiwa na Bahá’u’lláh na kujaaliwa Naye mamlaka ya juu kabisa na muongozo usioshindwa, na ambayo kwayo Bwana aliandika: “Kwenye chombo hiki mambo yote lazima yarejelewe.” Ni kwa uwazi ulioje, tunaweza kuona ukweli wa dai la Bahá’u’lláh’: “Mkono wa Mwenye Nguvu Zote umesimika Ufunuo Wake juu ya msingi usioshambulika, unaodumu. Tufani za ugomvi wa wanadamu hazina nguvu kudhoofisha msingi wake, wala nadharia dhanifu za watu kufanikiwa katika kuuharibu muundo wake.”

*(Kutoka ujumbe wa Oktoba 1963 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá’í wa Ulimwengu)*

56.1 Baada ya kusali na kujifunza kwa uangalifu Maandiko Matakatifu yanayojikita juu ya suala la uteuzi wa mrithi kwa Shoghi Effendi kama Mlinzi wa Hoja ya Mungu, na baada ya ushauriano mrefu ambao ulijumuisha kupima uzito wa maoni ya Mikono wa Hoja ya Mungu wanaoishi katika Nchi Takatifu, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huona kwamba hakuna namna ya kumteua au kutunga sheria kufanya iwezekane kumteua Mlinzi wa pili kumrithi Shoghi Effendi.

*(Kutoka ujumbe wa 6 Oktoba 1963 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa)*

---

[5] *21 Aprili 1963 BK*

57.1 Tumefurahi kwamba umeleta mbele yetu maswali yanayowatatiza baadhi ya waumini. Ni bora zaidi kwa maswali haya kuwekwa kwa uhuru na uwazi kuliko kubaki nayo, bila kuyasema, yakielemea mioyo ya waumini thabiti. Mara tu mtu anapozifahamu kanuni fulani za msingi za Ufunuo wa Bahá'u'lláh shaka kama hizo hutawanywa kwa urahisi. Hii siyo kusema kwamba Hoja ya Mungu haina mafumbo. Mafumbo yapo kwa hakika, lakini siyo ya aina ile ya kutikisa imani ya mtu mara tu misingi muhimu ya Hoja na kweli zisizokanushika za hali yoyote zinaeleweka vyema.

57.2 Maswali yaliyowasilishwa na waumini mbalimbali yanaangukia kwenye makundi matatu. Kundi la kwanza linajikita juu ya hoja zifuatazo: Kwa nini hatua zilichukuliwa kuchagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wakati ikifahamika tangu awali kwamba hakungekuwepo Mlinzi? Je, ulikuwa muda muafaka kwa hatua kama hiyo? Je, Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa isingeweza kutekeleza kazi hiyo?

57.3 Wakati wa kifo cha mpendwa wetu Shoghi Effendi ilithibitika, kutokana na mazingira na kutokana na matakwa dhahiri ya Maandiko Matakatifu, kwamba kufuatana na maelekezo ya Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá ilikuwa haiwezekani kwake kuteua mrithi. Hali hii, ambapo Mlinzi alifariki bila kuweza kumteua mrithi, ilizua swali lenye utata ambalo halikutajwa katika Maandiko Matakatifu dhahiri, na ilibidi lirejelewe kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Marafiki wanapaswa waelewe wazi kwamba kabla ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hapakuwa na ufahamu kwamba hakungekuwepo Mlinzi. Hapangeweza kuwepo ufahamu wowote wa awali kama huo, bila kujali maoni yoyote waliyokuwa nayo waumini binafsi.

Siyo Mikono wa Hoja ya Mungu, wala Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa, wala chombo kingine chochote kilichokuwepo kingeweza kufanya uamuzi juu ya suala hili umuhimu kabisa. Nyumba ya Haki tu ndiyo ilikuwa na mamlaka kulitolea tamko. Hii ndiyo ilikuwa sababu moja ya dharura kwa ajili ya uitishaji wa uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haraka iwezekanavyo.

57.4 Kufuatia kufariki kwa Shoghi Effendi utawala wa kimataifa wa Imani uliendelezwa na Mikono wa Hoja ya Mungu kwa makubaliano na uaminifu kamili wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na jamii ya waumini. Hii ilikuwa ni kufuatana na Mlinzi kuwataja Mikono kama "Wakadamu Wakuu" wa Dola changa la Ulimwengu wa Bahá'u'lláh".

57.5 Kutoka mwanzoni kabisa mwa uangalizi wao wa Hoja ya Mungu Mikono walitambua kwamba kwa kuwa hawakuwa na hakika ya muongozo mtakatifu kama ule uliohakikishwa bila kutatanisha kwa Mlinzi na kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, njia yao moja iliyo salama ilikuwa kufuata kwa uthabiti usiokengeuka maelekezo na sera za Shoghi Effendi. Historia nzima ya dini haioneshi kumbukumbu yoyote linganifu ya kujiwekea nidhamu kali kama hiyo, utiifu kamili kama huo na utovu kamili wa nafsi kama huo wa viongozi wa dini wanaojikuta wenyewe ghafla wameondokewa na uongozi wenye uvuvio mtakatifu. Deni la shukurani ambalo wanadamu kwa vizazi, la, zama zijazo, wanawiwa kwa hili fungu dogo la roho zilizoelemewa na huzuni, zilizothabiti, za kishujaa ni mbali na makadirio.

57.6 Mlinzi alikuwa ameupatia ulimwengu wa Kibahá'í mipango dhahiri na yenye utondoti ikijumuisha kipindi hadi kufikia Riḍván 1963, mwisho wa Pambano la Kiroho la Miaka Kumi. Kutoka hapo na kuendelea, vinginevyo kama Imani ingekuwa hatarini, muongozo zaidi wa kiroho ulikuwa muhimu. Hii ilikuwa ni sababu ya pili shinikizi kwa ajili ya uitishwaji wa uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Usahihi wa muda huo ulithibitishwa zaidi na marejeo katika barua za Shoghi Effendi kwa mipango ya Pambano la Kiroho la Miaka Kumi kufuatiwa na mipango mingine chini ya uelekezi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Rejeo moja la namna hiyo ni aya ifuatayo kutoka barua ya 25 Februari 1951 iliyoandikwa kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Visiwa vya Uingereza, ikihusu Mpango wake wa Miaka Miwili ambao ulitangulia kwa kitambo kidogo Pambano la Kiroho la Miaka Kumi: Juu ya mafanikio ya shughuli hii, isiyopitwa katika wigo wake, ya kipekee katika mwenendo wake na kubwa mno katika nguvu zake za kiroho, sharti utegemee uanzishwaji,

kwenye kipindi cha baadaye katika Zama za Utungo wa Imani, wa shughuli zinazokumbatia ndani ya upana wake Mabaraza yote ya Kitaifa yakifanya kazi katika Ulimwengu mzima wa Kibahá'í—shughuli zenye kujumuisha ndani yake maandalizi kwa ajili ya uzinduzi wa shughuli za ulimwengu mzima zinazotazamiwa kuanzishwa, katika vipindi vijavyo vya Zama hiyo hiyo, na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambazo zitaashiria umoja na kuratibu na kuunganisha shughuli za Mabaraza haya ya Kitaifa.

57.7 Wakiwa wamesimamizi wa Hoja ya Mungu kwa miaka sita, Mikono, kwa imani kamili katika Maandiko Matakatifu, waliwataka waumini kuchagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, na hata walienda mbali zaidi kiasi cha kuomba kwamba wao wenyewe wasipigiwe kura. Tukio moja pekee, la kuhuzunisha la mtu yeyote kujaribiwa na tamaa ya madaraka lilikuwa ni jaribio la kuhuzunisha la Charles Mason Remey kupora Wadhifa wa Ulinzi.

57.8 Dondoo zifuatazo kutoka Waraka wa 'Abdu'l-Bahá hutamka kwa uwazi na kwa msisitizo misingi ambayo marafiki tayari wana ufahamu nayo kutoka Wasia na Agano la Bwana na barua mbalimbali za Shoghi Effendi, na zinaeleza msingi wa uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Waraka huu ulitumwa Uajemi na mpendwa Mlinzi mwenyewe, katika miaka ya mwanzoni ya utumishi wake, kwa ajili ya kusambazwa miongoni mwa waumini.

… kwa kuwa 'Abdu'l-Bahá yumo katika dhoruba ya hatari na daima Yeye huzichukia tofauti za maoni… Sifa ziwe kwa Mungu, hakuna nafasi ya mafarakano.

Báb, Yule Aliyetukuka, ni Asubuhi ya Ukweli, Ambaye wangavu wa Nuru Yake hung'aa kwenye maeneo yote. Yeye pia ni Mtangulizi wa Mwanga Mkuu Kabisa, Mwanga wa Abhá. Uzuri Uliobarikiwa ndiye Yule aliyeahidiwa na vitabu vitakatifu vya zamani, ufunuo wa Chanzo cha mwanga ambao uling'aa juu ya Mlima Sinai, Ambaye moto wake ulichaga katikati ya Kichaka Kiwakacho. Sisi, mmoja mmoja na wote, tu watumishi wa Kizingiti Chao, na tunasimama kila mmoja kama bawabu

mnyenyekevu kwenye mlango Wao.

Kusudi langu ni hili, kwamba kabla ya kumalizika kwa miaka elfu moja, hakuna yeyote mwenye haki ya kusema neno lolote, hata kudai daraja la Ulinzi. Kitabu Kitakatifu Kabisa ni Kitabu ambacho kwacho watu wote watakirejelea, na ndani mwake Sheria za Mungu zimefunuliwa. Sheria ambazo hazikutajwa katika Kitabu hazina budi zirejelewe kwenye maamuzi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Hakutakuwa na nafasi kwa ajili ya tofauti….Chondechonde asije mtu yeyote akatengeneza mpasuko au kuamsha uchochezi. Endapo pakiwepo na tofauti za maoni, Nyumba Kuu Kabisa ya Haki mara moja ingetatua matatizo hayo. Vyovyote maamuzi yake yatakavyokuwa, kwa kura za wengi, utakuwa ndiyo ukweli halisi, kwa kuwa Nyumba hiyo ipo chini ya ulinzi, muongozo usiokosea na uangalizi wa Bwana mmoja wa kweli. Yeye ataikinga kutokana na makosa na kuilinda chini ya bawa la utakatifu Wake na utovu wa makosa. Yule aipingaye atatupwa nje na hatimaye atakuwa kati ya walioshindwa.

Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki sharti ichaguliwe kulingana na mfumo unaofuatwa katika uchaguzi wa mabunge ya Ulaya. Na wakati nchi zitakapokuwa zikiongozwa, Nyumba za Haki za nchi mbalimbali zitachagua Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki….
Wakati wowote wapendwa wote wa Mungu katika kila nchi wateuapo wajumbe wao, na hawa kwa upande wao huchagua wawakilishi wao, na wawakilishi hawa kuchagua shirika, shirika hilo litachukuliwa kuwa Nyumba Kuu Kabisa ya Haki.

Uanzishwaji wa Nyumba hiyo hautegemei juu ya ubadilishwaji wa mataifa yote ya ulimwengu kuwa katika Imani moja. Kwa mfano, kama hali zikiruhusu na hakutakuwa na usumbufu utakaosababishwa, marafiki huko Uajemi watachagua wawakilishi wao, na vivyo hivyo marafiki huko America, India na maeneo mengine pia watachagua wawakilishi wao na hawa wachaguwe Nyumba ya Haki. Nyumba hiyo ya Haki itakuwa ndiyo Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki. Ndiyo ilivyo.
*(“Makátíb-i-‘Abdu’l-Bahá”, vol. III, uk. 500–501)*

57.9 Marafiki wanapaswa watambue kwamba hakuna chochote katika Maandiko kinachoonesha kwamba uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ungeweza kuitishwa tu na Mlinzi. Kinyume chake, ‘Abdu’l-Bahá aliona taswira ya uitishaji wa uchaguzi wake katika kipindi cha uhai wake. Wakati ulioelezewa na Mlinzi kama “nyakati za giza totoro za maisha Yake [Bwana], chini ya utawala wa ‘Abdu’l-Ḥamíd, alipokuwa tayari kusafirishwa kwenda maeneo yasiyokalika kabisa ya Afrika kasikazini”, na hata wakati maisha Yake yalipotishiwa, ‘Abdu’l-Bahá alimwandikia Ḥájí Mírzá Taqí Afnán, binamu wa Báb na mjenzi mkuu wa Hekalu la ‘Ishqábád, akimuamuru kufanya maandalizi kwa ajili ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ikiwa vitisho dhidi ya Bwana vingefanikiwa. Sehemu ya pili ya Wasia wa Bwana pia inahusika kwa hali hiyo na inapaswa isomwe na marafiki.

57.10 Mfuatano wa pili wa matatizo yanayowachusha baadhi ya marafiki ni kwenye suala la utovu wa kufanya makosa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na uwezo wake wa kufanya kazi bila uwepo wa Mlinzi. Ugumu maalum umeonekana katika kuelewa athari ya tamko lifuatalo lililotolewa na mpendwa Mlinzi:

Ungetengwa kutoka kwenye asasi ya Ulinzi Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá’u’lláh ungekatishwa na kunyimwa moja kwa moja ile kanuni ya urithi ambayo, kama ambavyo ‘Abdu’l-Bahá ameandika, imeendelea kushikiliwa na Sheria ya Mungu. “Katika Vipindi vyote Vitakatifu,” Yeye hutamka, katika waraka alioandikiwa mfuasi mmoja wa Imani huko Uajemi, “mtoto mkubwa kabisa wa kiume amepewa upekee usio wa kawaida. Hata daraja la unabii limekuwa haki yake ya kuzaliwa.” Bila asasi kama hiyo uadilifu wa Imani ungewekwa rehani, na utengamano wa mfumo mzima ungehatarishwa kabisa. Hadhi yake ingeumia, nyenzo zihitajikazo kuuwezesha uchukue taswira ya muda mrefu, isiyoweza kuingiliwa kwa mfululizo wa vizazi zingeweza kukosekana kabisa, na muongozo muhimu wa kufafanua mipaka ya eneo la kisheria la wawakilishi wake wa kuchaguliwa lingeweza kuondolewa kabisa.
*(“Dispensation of Bahá’u’lláh”, “The World Order of Bahá’u’lláh”, pg. 148)*

57.11 Acha marafiki wanaotaka uelewa wa ufasaha zaidi wa aya hii katika wakati huu waipime katika mwanga wa maandiko mengine mengi ambayo yanashughulika na mada hiyo hiyo, kwa mfano aya zifuatazo zilizokusanywa kutoka barua za Shoghi Effendi:

Wao pia, katika lugha ya wazi, ya uhakika na ya mkazo, wameteua asasi pacha za Nyumba ya Haki na ya Ulinzi, kama chaguo la Warithi wao, wakitazamiwa kutumia kanuni, kuzitangaza sheria, kuzilinda asasi, kuitumia kwa utiifu na kwa akili Imani kwa mahitaji ya jamii endelevu, na kuutimiliza urithi usioweza kuchafuliwa ambao Waasisi wa Imani wameukabidhi kwa ulimwengu.
*(Barua ya 21 Machi 1930, "World Order of Bahá'u'lláh", pg. 19–20)*

Lazima pia ieleweke kinagaubaga na kila muumini kwamba asasi ya Ulinzi kwa vyovyote haifuti, au hata kwa kiwango kidogo kabisa kupunguza, uwezo uliotolewa na Bahá'u'lláh kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika Kitáb-i-Aqdas, na imethibitishwa mara kwa mara na kwa dhati na 'Abdu'l-Bahá katika Wasia Wake. Haifanyizi kinyume kwa namna yoyote ile Wasia na Maandiko ya Bahá'u'lláh, wala haibatilishi maagizo Yake yoyote yaliyofunuliwa. Inaongeza hadhi ya mkusanyiko huo uliotukuka, inaimarisha daraja lake la juu kabisa, inalinda umoja wake, inahakikisha uendelevu wa utendaji wa kazi zake, bila kudhani hata kwa kiasi kidogo kuingilia eneo lake la mamlaka lilioainishwa dhahiri. Sisi kwa hakika tupo karibu sana na waraka mkuu kama huo, kuweza kudai kuwa tuna uelewa kamili wa maana yake yote, au kudhani kuwa tumepata siri nyingi za maudhui yake yasiyo na shaka…
*(Barua ya 27 Februari 1929, "World Order of Bahá'u'lláh", uk. 8)*

Kutoka matamko haya imekuwa wazi na dhahiri pasipo shaka kwamba Mlinzi wa Imani amefanywa kuwa Mfasiri wa Neno na kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imepewa kazi ya kutunga sheria juu ya masuala ambayo hayakufunuliwa wazi wazi katika mafundisho. Kazi ya kufasiri ya Mlinzi, ikitenda kazi ndani ya mipaka yake mwenyewe, ni ya kimamlaka na yenye kufunga kama ilivyo utungaji wa sheria wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa, ambayo haki na stahili yake ya kipekee ni kuzitolea

matamko na kutoa hukumu ya mwisho juu ya zile sheria na amri ambazo Bahá'u'lláh hakuzifunua wazi wazi. Hakuna anayeweza, wala kamwe kuthubutu, kuingilia milki takatifu na iliyoagizwa ya mwingine. Hakuna atakayetafuta kuhujumu mamlaka mahususi na yasiyo na shaka ambayo wote wawili wamepewa kitakatifu.

*("The Dispensation of Bahá'u'lláh", "World Order of Bahá'u'lláh", pg. 149–50)*

Kila kimoja hutumia madaraka yake, mamlaka yake, haki na stahili zake ndani ya mipaka kilichowekewa. Hizi hazipingani, wala hazipunguzi hata kidogo kutoka kwenye nafasi ambayo kila moja ya asasi hizi hushikilia.

*("The Dispensation of Bahá'u'lláh", "World Order of Bahá'u'lláh", pg. 148)*

Ingawa Mlinzi wa Imani amefanywa kuwa Mkuu wa kudumu wa chombo cha juu kabisa hawezi kamwe, hata kwa kitambo tu, kujinyakulia haki pekee ya kutunga sheria. Hawezi kufanya maamuzi dhidi ya uamuzi wa wajumbe-wenza walio wengi …

*("The Dispensation of Bahá'u'lláh", "World Order of Bahá'u'lláh", pg. 150)*

Juu ya yote, acha mioyo ya marafiki ihakikishiwe kwa maneno haya ya Bahá'u'lláh:

Mkono wa Mwenye Nguvu Zote umesimika Ufunuo Wake juu ya msingi usioshambulika, unaodumu. Tufani za ugomvi wa wanadamu hazina nguvu kudhoofisha msingi wake, wala nadharia dhanifu za watu kufanikiwa katika kuuharibu muundo wake."

*("The World Order of Bahá'u'lláh", pg. 109)*

*Na haya ya 'Abdu'l-Bahá:*

Kwa hakika, Mungu husababisha kile Yeye akipendacho; hakuna kinachoweza kufuta Agano Lake; Hakuna kinachoweza kuzuia mapenzi Yake wala kupinga Hoja Yake! Yeye hufanya kwa utashi Wake kile apendacho na Yeye ana nguvu juu ya vitu vyote! …

*("Tablets of Abdul-Baha Abbas", tol. III, pg. 598)*

57.12 Inapaswa ieleweke na marafiki kwamba kabla ya kutunga sheria juu ya jambo lolote lile Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huchunguza kwa uangalifu na kikamilifu vyote viwili Maandiko Matakatifu na Maandiko ya Shoghi Effendi juu ya mada husika. Fasiri zilizoandikwa na mpendwa Mlinzi zinagusa eneo kubwa mno la mada na zinafunga kisawia kama lilivyo Andiko lenyewe.

57.13 Kuna tofauti kubwa mno kati ya fasiri za Mlinzi na fafanuzi za Nyumba ya Haki katika kutenda kazi yake "kujadiliana juu ya matatizo yote ambayo yamesababisha mfarakano, maswali yenye utata na mambo ambayo hayakufunuliwa wazi wazi katika Kitabu". Mlinzi hufunua kile ambacho Andiko humaanisha; fasiri yake ni kauli ya ukweli ambao hauwezi kugeuzwa. Juu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kwa maneno ya Mlinzi, "imepewa haki ya kipekee ya utungaji sheria juu ya masuala ambayo hayajafunuliwa wazi wazi katika Maandiko ya Kibahá'í". Matamko yake, ambayo yanaweza kubadilishwa au kuondolewa na Nyumba ya Haki yenyewe, yanajaliza na kutumia Sheria ya Mungu. Ingawa haijapewa kazi ya kufasiri, Nyumba ya Haki ina nafasi ya kufanya kila kitu kinachohitajika kusimika Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh hapa duniani. Umoja wa itikadi hudumishwa na uwepo wa matini hai ya Maandiko na fasiri iliyosheheni ya 'Abdu'l-Bahá na Shoghi Effendi, pamoja na katazo kabisa dhidi ya mtu yeyote kutoa mawazo mbadala ya fasiri "za kimamlaka" au "zilizovuviwa" au kupora kazi ya Mlinzi. Umoja wa utawala unahakikishwa na mamlaka ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

"Hivi", kwa maneno ya Shoghi Effendi, "ndivyo lisivyobadilishika Neno Lake lililofunuliwa. Huo ndiyo unyumbulikaji ambao huziainisha kazi za watumishi Wake wateule. Wa kwanza huhifadhi utambulisho wa Imani Yake, na kulinda uadilifu wa sheria Yake. Wa pili huiwezesha, kama vile kiumbe hai, kupanuka na kujirekebisha yenyewe kwa ajili ya mahitaji na matakwa ya jamii ibadilikayo daima."
*(Barua ya 21 Machi 1930, ("The World Order of Bahá'u'lláh", pg. 25)*

57.14 Kila muumini wa kweli, kama anataka kujizamisha katika uelewa wa Hoja ya Bahá'u'lláh, lazima anahitaji kuchunguza kwa imani ya kina katika ubora usioshindwa wa Ujumbe Wake na Agano Lake, kwa unyenyekevu wa kutambua kwamba hakuna hata mmoja wa kizazi hiki awezaye kudai kuwa ameukumbatia ukubwa wa Hoja Yake wala kuwa amezifahamu siri na nguvu lukuki zisizodhihirika ilizonazo. Maneno ya Shoghi Effendi yanatoa ushuhuda tosha kwenye ukweli huu:

Jinsi gani ulivyo mkubwa mno Ufunuo wa Bahá'u'lláh! Jinsi gani zilivyo kuu Baraka Zake zilizomiminwa juu ya wanadamu katika siku hii! Na bado, jinsi gani ulivyo hafifu, pungufu ufahamu wetu wa umuhimu na utukufu wake! Kizazi hiki kipo karibu mno na Ufunuo ulio mkuu mno kutoweza kuzitambua kikamilifu, zile fursa zisizo na kikomo za Imani Yake, ile tabia isiyo na mfano wa kurejelea ya Hoja Yake, na Kipindi cha ajabu cha Majaliwa Yake.
*(Barua ya 21 Machi 1930, ("The World Order of Bahá'u'lláh", pg. 24)*

Tunaitwa na mpendwa Bwana wetu katika Wasia na Agano Lake siyo kulifuata kwa kusita, bali kufichua thamani yake kwa ulimwengu mzima. Kujaribu kukadiria thamani yake kamili, na kupata maana yake hasa baada ya kupita kwa muda mfupi sana tangu kuanzishwa kwake, ni mapema mno na ujuvi kwetu. Lazima tuwe na Imani na wakati, na muongozo wa Nyumba ya Mungu ya Haki ya Ulimwengu, ili kupata uelewa wa wazi na kamili zaidi wa nyenzo na athari zake….
*(Barua ya 23 Februari 1924, iliyochapishwa katika "Bahá'íAdministration", pg. 62)*

Kuhusu utaratibu na usimamizi wa masuala ya kiroho ya marafiki, kile ambacho ni muhimu sana sasa ni uimarishaji wa Mabaraza ya Kiroho katika kila kituo, kwa sababu juu ya misingi hii madhubuti na isiyotikiswa, Nyumba ya Juu ya Haki ya Mungu itainuliwa na kusimikwa imara katika siku zijazo. Pale jengo hili kuu kabisa litakapoinuliwa juu ya msingi usiotikisika, kusudi la Mungu, hekima, kweli za ulimwengu wote, siri na

uhalisia wa Ufalme, ambavyo Ufunuo wa ajabu wa Bahá'u'lláh umeweka ndani ya Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá, pole pole vitafunuliwa na kudhihirishwa.

*(Barua ya 19 Desemba 1923—iliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)*

57.15 Matamko kama haya huashiria kwamba maana kamili ya Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá, kadhalika uelewa wa athari za Utaratibu wa Ulimwengu ulioletwa na waraka usio kifani, linaweza kufunuliwa tu pole pole machoni pa watu, na baada ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kuwa imeundwa. Marafiki wanaitwa kuwa na imani na wakati, na kusubiri muongozo wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo kadiri hali zinavyohitaji, itatoa matamko itatua kufafanua masuala yenye utata.

57.16 Kundi la tatu la maswali yanayoulizwa na marafiki huhusu tondoti za utendaji kazi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu bila uwepo wa Mlinzi, hususan suala la ufukuzaji wa wajumbe wa Nyumba ya Haki. Maswali kama hayo yatafafanuliwa katika Katiba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambapo utunzi wake ni lengo la Mpango wa Miaka Tisa. Wakati huo huo marafiki wanaarifiwa kwamba mjumbe yeyote anayetenda "dhambi yenye madhara kwa maslahi ya wengi", anaweza kufukuzwa ujumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa kura za wengi za Nyumba yenyewe. Iwapo mjumbe yeyote, Mungu apishie mbali, akipatikana na hatia ya kuvunja Agano, suala hilo lingechunguzwa na Mikono wa Hoja ya Mungu, na mvunja-Agano angefukuzwa kwa uamuzi wa Mikono wa Hoja ya Mungu wanaoishi katika Nchi Takatifu, kutegemea idhini ya Nyumba ya Haki, kama ilivyo katika tukio la muumini mwingine yeyote Uamuzi wa Mikono katika shauri kama hilo ungetangazwa ulimwengu wa Kibahá'í na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

*(Kutoka barua ya 9 Machi 1965 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa)*

58.1 Umeuliza uwekaji muda wa uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muktadha wa tamko hili la Mlinzi: "… kama hali nzuri zingeruhusu, ambapo Wabahá'í wa Uajemi na wa nchi jirani zilizokuwa chini ya utawala wa Kisovieti, wangewezeshwa kuchagua wawakilishi

wao wa kitaifa, kufuatana na kanuni za muongozo zilizowekwa katika maandiko ya 'Abdu'l-Bahá, kikwazo pekee ambacho kingebakia katika uundwaji wa hakika wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa kingekuwa kimeondolewa. Mnamo 19 Aprili 1947 Mlinzi, katika barua iliyoandikwa kwa niaba yake na katibu wake, aliyajibu maswali ya muumini mmoja kuhusu aya hii: "Wakati alipoitaja Urusi kulikuwa na Wabahá'í kule, sasa Jamii kiuhalisia haipo; kwa hiyo, uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa hauwezi kutegemea juu ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Urusi. Lakini Mabaraza mengine ya Kiroho ya Kitaifa yenye nguvu yatatakiwa yaundwe kabla haijaweza kusimikwa."

58.2 Unapendekeza uwezekano kwamba, kwa ajili ya maslahi ya Hoja, taarifa fulani kuhusiana na urithi kwa Shoghi Effendi inazuiliwa kuwafikia waumini. Tunakuhakikishia kwamba hakuna chochote kile kinachozuiliwa kuwafikia marafiki kwa sababu yoyote ile. Hakuna shaka kabisa kwamba katika Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá Shoghi Effendi alikuwa mamlaka iliyotajwa kumteua mrithi wake, lakini hakuwa na watoto na Aghṣán wote waliokuwa hai walikuwa wamevunja Agano. Hivyo, kama Mikono wa Hoja walivyosema mnamo 1957, ni wazi kwamba hakukuwa na yeyote aambaye angeweza kumteua kufuatana na maelekezo ya Wasia. Kufanya uteuzi nje ya maelekezo yaliyo wazi na mahususi ya Wasia na Agano la Bwana ni dhahiri ingekuwa njia isiyowezekana na isiyofikirika kwa Mlinzi kuitumia, mteule mtakatifu na mbebaji na mlinzi wa Agano. Zaidi, Wasia ule ule uliweka wazi njia kwa ajili ya uthibitisho wa Mlinzi kumteua mrithi wake, kama ujuavyo. Wale Mikono tisa watakaochaguliwa na kundi la Mikono walikuwa watoe ridhaa yao kupitia kura ya siri kwa chaguo la Mlinzi. Mnamo 1957 kundi zima la Mikono, baada ya kulichunguza jambo hilo, walitangaza kwamba Shoghi Effendi hakumteua mrithi na hakuacha wasia. Hili limeandikwa na limethibitishwa.

58.3 Ukweli kwamba Shoghi Effendi hakuacha wasia hauwezi kutumika kama ushahidi wa yeye kushindwa kumtii Bahá'u'lláh—badala yake inatupasa tukubali kwamba katika ukimya wake wenyewe kuna hekima na ishara ya uongozi usiokosea.  Inatupasa tuyatafakari kwa kina maandiko

tuliyonayo, na tutafute kuuelewa umuhimu mwingi ambao yanaubeba. Usisahau kwamba Shoghi Effendi alisema mambo mawili yalikuwa muhimu kwa ajili ya uelewa uongezekao wa Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh: kupita kwa muda na uongozi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

58.4 Kutokuwa na makosa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ikitenda kazi ndani ya eneo lake lililoamriwa, hakujafanywa kutegemee juu ya kuwepo kwa Mlinzi wa Hoja miongoni mwao. Ingawa katika milki ya fasiri matamko ya Mlinzi daima yanafunga, katika nafasi ya ushiriki wa Mlinzi katika kutunga sheria daima ni uamuzi wa Nyumba yenyewe ndiyo lazima utamalaki. Hili linaungwa mkono na maneno ya Mlinzi: Kazi ya kufasiri ya Mlinzi, ikitenda kazi ndani ya mipaka yake mwenyewe, ni ya kimamlaka na yenye kufunga kama ilivyo utungaji wa sheria wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa, ambayo haki na stahili yake ya kipekee ni kuzitolea matamko na kutoa hukumu ya mwisho juu ya zile sheria na amri ambazo Bahá'u'lláh hakuzifunua wazi wazi. Hakuna anayeweza, wala kamwe kuthubutu, kuingilia milki takatifu na iliyoagizwa ya mwingine. Hakuna atakayetafuta kuhujumu mamlaka mahususi na yasiyo na shaka ambayo wote wawili wamepewa kitakatifu.

58.5 Ingawa Mlinzi wa Imani amefanywa kuwa Mkuu wa kudumu wa chombo cha juu kabisa hawezi kamwe, hata kwa kitambo tu, kujinyakulia haki pekee ya kutunga sheria. Hawezi kufanya maamuzi dhidi ya uamuzi wa wajumbe-wenza walio wengi, lakini analazimika kusisitiza juu ya ufikiriwaji tena na wao wa sheria yoyote anayoamini kwa ufahamu wake kamili kuwa inapingana na maana na kukengeuka kutoka moyo wa maneno yaliyofunuliwa na Bahá'u'lláh."

58.6 Hata hivyo, mbali kabisa na kazi yake kama mjumbe na mkuu mtakatifu wa maisha wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, Mlinzi, akitenda kazi ndani ya eneo lake mwenyewe, alikuwa na haki na jukumu "kufafanua eneo la kiutendaji la kutunga sheria" la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Kwa maneno mengine, alikuwa na mamlaka kutamka iwapo jambo hilo lilikuwa au halikuwa tayari limeongelewa na Maandiko

Matakatifu na kwa hiyo iwapo lilikuwa ndani ya mamlaka ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kulitungia sheria. Hakuna mtu mwingine, mbali na Mlinzi, aliye na haki au mamlaka kutoa fafanuzi kama hizo. Hivyo swali huibuka: Katika kutokuwepo kwa Mlinzi, je, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imo katika hatari ya kwenda nje ya eneo lake sahihi na hivyo kuangukia kwenye kosa? Hapa lazima tukumbuke vitu vitatu: Kwanza, Shoghi Effendi, kwa kipindi cha miaka thelathini na sita cha Ulinzi wake, amekwishafanya fafanuzi nyingi sana kama hizo, kujaliza zile zilizofanywa na 'Abdu'l-Bahá na Bahá'u'lláh Mwenyewe. Kama ambavyo tayari imekwishatangazwa kwa marafiki, uchunguzi makini wa Maandiko na fasiri juu ya mada yoyote ambayo Nyumba ya Haki inapendekeza kuitungia sheria daima hutangulia kitendo chake cha kutunga sheria. Pili, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, yenyewe ikihakikishiwa uongozi mtakatifu, inafahamu vyema kutokuwepo kwa Mlinzi na itayaendea mambo yote ya kutunga sheria pale tu inapokuwa na hakika ya eneo lake la kiutendaji, eneo ambalo Mlinzi amelielezea kwa kujiamini kuwa "limefafanuliwa wazi wazi". Tatu, sharti tusisahau tamko lililoandikwa la Mlinzi kuhusu hizi Asasi mbili: "Hakuna anayeweza, wala kamwe kuthubutu, kuingilia milki takatifu na iliyoagizwa ya mwingine."

58.7 Kuhusu haja ya kufanya upunguzaji kutoka kwenye Maandiko ili kusaidia katika utungaji sheria wa Nyumba ya Haki, kuna andiko lifuatalo kutoka kalamu ya 'Abdu'l- Bahá:

> Yale masuala yenye umuhimu mkubwa ambayo hufanya msingi wa Sheria za Mungu zilizoandikwa dhahiri katika Maandiko, lakini sheria ndogo ndogo imeachiwa Nyumba ya Haki. Hekima ya hili ni kwamba nyakati kamwe hazibaki vile vile, kwani mabadiliko ni sifa ya lazima na njema muhimu ya ulimwengu huu, na ya wakati na mahali. Kwa hiyo, Nyumba ya Haki itachukua hatua kama ipasavyo.
>
> Acha isidhaniwe kwamba Nyumba ya Haki itafanya uamuzi wowote kulingana na dhana na mawazo yake yenyewe. Mungu apishie mbali! Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki itafanya maamuzi na kuanzisha sheria kupitia uvuvio na uthibitisho wa Roho Mtakatifu, kwa sababu ipo katika

usalama na chini ya hifadhi na ulinzi wa Uzuri wa Kale, na utii kwa maamuzi yake inapasa na ni wajibu muhimu na jukumu kamilifu na hakuna nafasi ya kukwepa kwa yeyote.

Sema, Enyi watu: Kwa hakika, Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki ipo chini ya mabawa ya Bwana wenu, Mwenye Huruma, Mwenye Rehema—Zote, yaani, chini ya ulinzi Wake, uangalizi Wake na hifadhi Yake; kwa kuwa Yeye amewaamuru waumini thabiti kutii shirika hilo lililobarikiwa, kutakasika na litiishalo, ambalo mamlaka yake yameamriwa kitakatifu na ya Ufalme wa Mbinguni na ambalo sheria zake huvuviwa na ni za kiroho.

Kwa kifupi, hii ndiyo hekima ya kurejelea sheria za kijamii kwa Nyumba ya Haki. Katika dini ya Kiislám, vivyo hivyo, siyo kila sheria ilifunuliwa kwa uwazi, la, siyo kila sehemu ya kumi ya sehemu ya kumi ilijumuishwa katika Maandiko; ingawa masuala yote yenye umuhimu mkubwa hususani yalirejelewa, bila shaka zilikuwepo maelfu ya sheria ambazo hazikuainishwa. Hizi zilitungwa na makasisi wa zama za baadaye kulingana na sheria za kiislam vyombo vyake vya kisheria na makasisi binafsi walifanya marekebisho yenye mkanganyiko kutoka kwenye sheria zilizofunuliwa mwanzoni. Zote hizi ziliagizwa zitumike. Leo mchakato huu wa upunguzaji ni haki ya shirika la Nyumba ya Haki, na upunguzaji na mahitimisho ya wasomi binafsi havina mamlaka, vinginevyo kama imeidhinishwa na Nyumba ya Haki. Tofauti kwa uhakika ni hii, kwamba kutokana na mahitimisho na idhini ya shirika la Nyumba ya Haki ambayo wajumbe wake wamechaguliwa na, na wanajulikana kwa Jumuiya ya Kibahá'í kote ulimwengu, hakuna tofauti zitakazoibuka; ambapo mahitimisho ya makasisi binafsi na wasomi, kwa hakika yatasababisha tofauti, na matokeo yake yatakuwa mfarakano, mgawanyiko na msambaratiko. Umoja wa Neno utaharibiwa, umoja wa Imani utatoweka na jengo la Imani ya Mungu litatikiswa.

58.8 Katika Utaratibu wa Bahá'u'lláh kuna kazi fulani ambazo zimetengwa kwa ajili ya asasi fulani, na zingine ambazo hufanywa kwa ushirika, hata ingawa zinaweza kuwa zaidi katika eneo moja maalum la

moja au la nyingine. Kwa mfano, ingawa Mikono wa Hoja ya Mungu wanazo kazi mahususi za ulinzi na uenezi, na wamebobea kwa ajili ya kazi hizi, ni jukumu pia la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Mabaraza ya Kiroho kulinda na kufundisha Hoja—hakika ufundishaji ni jukumu takatifu lililowekwa na Bahá'u'lláh juu ya kila muumini. Vivyo hivyo, japokuwa baada ya fasiri zenye mamlaka za Bwana kukabidhiwa kwa Mlinzi pekee yake, na japokuwa kutunga sheria ni kazi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu pekee yake, Asasi hizi mbili, katika maneno ya Shoghi Effendi, "zinakamilishana katika lengo na kusudi lao." "Lengo lao la pamoja, la kimsingi ni kuhakikisha muendelezo wa yale mamlaka yaliyoteuliwa kitakatifu ambayo hutiririka kutoka Chanzo cha Imani yetu, kulinda umoja wa wafuasi wake na kudumisha uadilifu na unyumbulifu wa mafundisho yake." Wakati Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haiwezi kufanya kazi yoyote ihusishwayo na Mlinzi pekee, lazima iendelee kulifanyia kazi lile lengo ambalo hushirikisha pamoja na Asasi ya Ulinzi.

58.9 Kama unavyoonesha kwa nukuu nyingi, Shoghi Effendi alisisitiza mara kwa mara kutotengana kwa asasi hizi mbili. Wakati aliutazamia wazi utendaji kazi wao wa pamoja, kimantiki haiwezi kuhitimishwa kutokana na hili kwamba, moja haiwezi kufanya kazi pasipo nyingine. Katika kipindi chote cha miaka thelathini na sita cha Ulinzi wake Shoghi Effendi alifanya kazi bila Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Sasa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu lazima ifanye kazi bila Mlinzi, lakini kanuni ya kutotengana inabakia. Asasi ya Ulinzi haipotezi umuhimu wala nafasi yake katika Utaratibu wa Bahá'u'lláh eti tu kwa sababu hakuna Mlinzi aliye hai. Lazima tujihadhari dhidi ya kukithiri kwa aina mbili: moja ni kujenga hoja kwamba kwa sababu hakuna Mlinzi yale yote yaliyoandikwa kuhusu Asasi ya Ulinzi na nafasi yake katika Utaratibu wa Ulimwengu wa Kibahá'í ni waraka mfu na haukuwa na umuhimu; nyingine ni kushadidiwa mno na umuhimu wa Asasi ya Ulinzi kiasi cha kuchukulia kiwepesi nguvu ya Agano, au kushawishika kupuuzia maandiko dhahiri ili kwa namna fulani, kwa njia fulani, kuwa na "Mlinzi".

58.10 Huduma kwenye Hoja ya Mungu huhitaji uaminifu na uadilifu kamili na imani isiyotetereka Kwake. Hakuna jema bali uovu tu ndiyo unaweza kuja kutokana na kujichukulia jukumu kwa ajili ya kuendeleza Hoja ya Mungu kwa siku zijazo za kwenye mikono yetu wenyewe na kujaribu kuilazimisha kwenye njia ambazo tunataka iende bila kujali maandiko ya dhahiri na udhaifu wetu wenyewe. Ni Hoja Yake. Yeye ameahidi kwamba mwanga wake hautashindwa. Nafasi yetu ni kushikilia kwa ung'ang'anivu kwenye Neno lililofunuliwa na kwenye Asasi ambazo ameziunda kuhifadhi Agano Lake.

58.11 Kwa usahihi ni katika muunganiko huu kwamba waumini lazima watambue umuhimu wa uaminifu wa kiakili na unyenyekevu. Katika vipindi vilivyopita makosa mengi yaliibuka kwa sababu waumini katika Ufunuo wa Mungu walikuwa wenye shauku iliyopitiliza kuukumbatia Ujumbe Mtakatifu ndani ya mfumo wa ufahamu wao finyu, kufafanua itikadi za kiimani pale ambapo ufafanuzi ulipokuwa nje ya uwezo wao, kuelezea mafumbo ambayo hekima na uzoefu wa zama za baadaye tu ndiyo vingeufanya ufahamike, kujenga hoja kwamba kitu fulani kilikuwa kweli kwa sababu tu kilionekana kinahitajika na cha muhimu. Upuuziaji wa namna wa kweli muhimu, kiburi cha kifikra kama hicho, lazima tukiepuke kwa hadhari kubwa.

58.12 Kama baadhi ya matamko ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hayana utondoti marafiki wanapaswa watambue kwamba sababu ya hili siyo usiri, bali hasa ni dhamira ya chombo hiki kuepuka kufasiri mafundisho na kuhifadhi ukweli wa tamko la Mlinzi kwamba "Viongozi wa dini, wawakilishi wa nadharia za kisiasa, magavana wa asasi za kibinadamu … wanapaswa wasiwe na shaka au wasiwasi kuhusiana na asili, chanzo au uhalali wa asasi ambazo wafuasi wa Imani wanazijenga kote ulimwenguni. Kwani haya yametiwa ndani ya mafundisho yenyewe, hayachafuliwi na hayafichwi na mawazo yasiyoruhusiwa au fasiri zisizo na mamlaka za Neno Lake."

58.13 Tofauti ya wazi imefanywa katika Imani yetu kati ya fasiri za kimamlaka na fasiri au uelewa ambao kila mtu binafsi huufikia kwa ajili yake mwenyewe kutokana na ujifunzaji wake wa mafundisho yake. Wakati ile ya kwanza imetengwa kwa Mlinzi, ile inayofuata, kulingana na muongozo tuliopewa kutoka kwa Mlinzi mwenyewe, haipaswi kwa vyovyote vile kuzuiwa. Kwa kweli, fasiri binafsi kama hiyo inachukuliwa kama tunda la nguvu ya urazini ya mtu na inawezesha uelewa bora zaidi wa mafundisho, ilimradi hakuna mivutano au malumbano yanayoibuka kati ya marafiki na mtu binafsi mwenyewe anaelewa na kuweka wazi kwamba maoni yake ni ya kwake tu. Fasiri binafsi huendelea kubadilika kadiri mtu anavyokua katika ufahamu wa mafundisho. Kama Shoghi Effendi alivyoeleza:"Kujizamisha katika Hoja humaanisha kusoma maandiko ya Bahá'u'lláh na Bwana kikamilifu kiasi cha kuweza kuyatoa kwa wengine katika umbile lake halisi. Kuna wengi ambao wana baadhi ya mawazo ya kijuu-juu wa kile Hoja hukisimamia. Wao, kwa hiyo, huyawasilisha pamoja na aina zote za mawazo ambayo ni yao wenyewe. Kwa kuwa Hoja bado ipo katika siku zake za mwanzoni lazima tuwe waangalifu kabisa tusije tukaangukia katika kosa hili na kuiumiza Harakati tunayoihusudu sana. Hakuna kikomo kwenye ujifunzaji wa Hoja. Kadiri tunavyosoma maandiko ndivyo tunavyopata humo ukweli zaidi na ndivyo tutakavyoona zaidi kwamba dhana zetu za awali zilikuwa na makosa."6 Hivyo, ingawa maizi binafsi zinaweza kuwa zenye kuangazia na zenye kusaidia, pia zinaweza kupotosha. Marafiki kwa hiyo lazima wajifunze kusikiliza maoni ya wengine bila kuwa wenye kuingiwa na hofu au kuruhusu imani yao kutikiswa, na kuelezea maoni yao wenyewe bila kuyashinikiza kwa Wabahá'í wenzao.

58.14 Hoja ya Mungu i hai, inakua na kuendelea kama kiumbe hai. Tena na tena imekumbana na hali za hatari ambazo zimewatatiza wauumini, lakini kila mara Hoja, ikisukumwa na kusudi la Mungu lisilobadilika, iliishinda hali hii ya hatari na ilisonga mbele hadi kwenye vilele vikubwa zaidi.

58.15 Hata kutoweza kwetu kulielewa fumbo na athari za kufariki kwa Shoghi Effendi kuwe kukubwa jinsi gani, ugwe imara ambao wote lazima waung'ang'anie kwa uhakika ni Agano. Lugha ya msisitizo na yenye nguvu ya Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá katika wakati huu, kama ilivyo wakati wa kufariki kwake, ndiyo ulinzi wa Hoja:

Kwenye Kitabu Kitakatifu Kabisa kila mmoja lazima ageukie na chochote ambacho hakijaandikwa kwa uwazi humo lazima kirejelewe Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Kile ambacho Asasi hii itaamua, , iwe kwa sauti ya wote au kwa wingi wao, hicho kwa hakika ndiyo kweli na Kusudi la Mungu Mwenyewe. Yeyote akengeukaye, kwa hakika atakuwa miongoni mwa wapendao mfarakano, ameonesha uovu na kugeukia mbali kutoka kwa Bwana wa Agano. Na tena: "… Wote lazima watafute muongozo na wageukie kwenye Kitovu cha Hoja na Nyumba ya Haki. Na yule ambaye hukigeukia kingine chochote kile hakika yumo katika kosa baya mno."

58.16 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo Mlinzi alisema itachukuliwa na vizazi vijavyo kama "kimbilio la mwisho la ustaarabu unaotetereka" sasa, bila uwepo wa Mlinzi, ndiyo asasi pekee iongozwayo bila kukosea hapa ulimwenguni ambapo wote lazima wageukie, na juu yake lipo jukumu la kuhakikisha umoja na maendeleo ya Hoja ya Mungu kulingana na Neno lililofunuliwa.

---

[6] *Iliandikwa na katibu wa Mlinzi kwa muumini binafsi 25 Agosti 1926*

Kuna matamko kutoka kwa Bwana na kwa Mlinzi yaoneshayo kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu mbali na kuwa Shirika la Juu Kabisa la Kutunga Sheria la Imani pia ni shirika ambalo wote lazima wageukie, na ni “kilele” cha Utaratibu wa Utawala wa Kibahà’ì, kadhalika ni “chombo cha juu kabisa cha Dola ya Kibaha’i.’ Mlinzi katika maandiko yake aliiainishia Nyumba ya Haki yale majukumu ya msingi kama utengenezaji wa mipango ya baadaye ya ufundishaji ulimwengu kote, uendeshaji wa shughuli za kiutawala za Imani, na miongozo, utaratibu na uunganishaji wa shughuli za Hoja duniani kote. Zaidi ya hapo, katika “God Passes By” Mlinzi anatoa tamko lifuatalo: “Kitab-i-Aqdas … siyo tu kinahifadhi sheria na amri za msingi ambazo juu yake mfumo wa Utaratibu Wake wa vizazi vijavyo lazima ujengwe, bali kinaamuru, mbali na kazi ya fasiri ambayo kinamjalia Mrithi Wake, asasi za muhimu ambazo kwazo uadilifu na umoja wa Imani Yake pekee unaweza kulindwa.” Pia, katika “Kipindi cha Baha’u’llah”, imeandikwa kwamba wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu “na siyo shirika la wale ambao huwachagua kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, hivyo wamefanywa kuwa wapokeaji wa muongozo mtakatifu ambao mara moja ni damu ya uzima na kinga ya mwisho ya Ufunuo huu.”

58.17 Kama Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilivyokwishatangaza, haiwezi kutunga sheria kuwezesha uteuzi wa mrithi wa Shoghi Effendi, wala kuwezesha uteuzi wa Mikono zaidi wa Hoja, lakini lazima ifanye kila kilicho ndani ya mamlaka yake kuhakikisha utendaji wa zile kazi zote inazofanya kwa ushirika pamoja na asasi hizi mbili zenye nguvu. Lazima hapo baadaye iweke nyenzo kwa ajili ya utekelezaji unaofaa wa majukumu ya ulinzi na utangazaji, ambayo mashirika ya kiutawala yanashirikiana na Ulinzi na Mikono wa Hoja; lazima, katika kutokuwepo kwa Mlinzi, ipokee na kupanga matumizi ya Huququ’llah, kulingana na tamko lifuatalo la Abdu’l-Baha: “Matumizi ya Huququ, yote au sehemu yake, inaruhusiwa, lakini hili linapaswa lifanywe kwa ruhusa ya mamlaka ya Hoja ambayo kwayo wote lazima waigeukie”; lazima itengeneze muongozo katika Katiba yake kwa ajili ya kumuondoa yeyote wa wajumbe ambaye hutenda

dhambi ambayo “yenye kudhuru usitawi wa wote”. Juu ya yote, lazima, kwa imani kamili kwa Baha’u’llah, watangaze Hoja Yake na kutekeleza Sheria Yake ili kwamba Amani Kuu Kabisa iweze kusimamishwa hapa ulimwenguni na misingi ya Ufalme wa Mungu duniani uweze kutimizwa. *(Kutoka barua ya 27 Mei, 1966 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

59.1 Barua yako ya hivi karibuni, ambayo unashiriki nasi maswali ambayo yamejitokeza kwa baadhi ya vijana wakati wanajifunza “Kipindi cha Baha’u’llah”, imezingatiwa kwa makini, na tunahisi kwamba tupapaswa tutoe maoni kwa vyote viwili hususan juu ya kifungu maalum unachokitaja na juu ya kifungu kinachohusiana nacho katika maandiko hayo hayo, kwa sababu vyote viwili vinahusu uhusiano baina ya Ulinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

59.2 Kifungu cha kwanza kinahusu wajibu wa Mlinzi kusisitiza juu ya ufikiriwaji tena na wajumbe-wenza katika Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, wa utungaji wowote wa sheria anayoamini kuwa inapingana na maana na kukengeuka kutoka moyo wa Maandiko Matakatifu. Kifungu cha pili kinahusu kutofanya makosa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu bila Mlinzi, yaani tamko la Shoghi Effendi kwamba “Bila asasi hiyo [ya Ulinzi] … muongozo muhimu wa kufafanua wigo wa kitendo cha utungaji sheria wa wawakilishi wake waliochaguliwa utakuwa umeondolewa kabisa”.

59.3 Baadhi ya vijana, unaonesha, walikuwa wamekanganywa kuhusu jinsi gani ya kupatanisha vifungu viwili vilivyotangulia na matamko kama yale yaliyo kwenye Wasia wa Abdu’l-Baha ambao huthibitisha kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu “i huru kutokana na makosa yote”.

59.4 Kama ambavyo Wasia na Agano la Abdu’l-Baha lisivyopingana na Kitab-i-Aqdas kwa namna yoyote ile, lakini kwa maneno ya Mlinzi, “huthibitisha, hujaliza na hupatanisha vifungu vya ‘Aqdas’”, hivyo maandishi ya Mlinzi hayapingani na Neno lililofunuliwa wala fasiri za Bwana. Katika kujaribu kuelewa Maandiko, kwa hiyo, mtu lazima atambue kwamba hapawezi na hapataweza kuwa na ukinzani halisi

miongoni mwao, na kwa kuzingatia hili kwa ujasiri tunaweza kutafuta umoja wa maana ambazo zimeyabeba.

59.5 Mlinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wana baadhi ya majukumu na kazi zinazofanana; kila mmoja hutenda kazi ndani ya wigo mbalimbali na tofauti. Kama Shoghi Effendi alivyoeleza, "… imewekwa na dhahiri bayana pasipo shaka kwamba Mlinzi wa Imani amefanywa kuwa mfasiri wa Neno na kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imepewa jukumu la kutunga sheria juu ya masuala ambayo hayajafunuliwa wazi kwenye mafundisho. Kazi ya kufasiri ya Mlinzi, ikitenda kazi ndani ya mipaka yake mwenyewe, ni ya kimamlaka na yenye kufunga kama ilivyo utungaji wa sheria wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa, ambayo haki na stahili yake ya kipekee ni kuzitolea matamko na kutoa hukumu ya mwisho juu ya zile sheria na amri ambazo Bahá'u'lláh hakuzifunua wazi wazi. Anaendelea kuthibitisha kuwa "Hakuna anayeweza, wala kamwe kuthubutu, kuingilia milki takatifu na iliyoagizwa ya mwingine. Hakuna atakayetafuta kuhujumu mamlaka mahususi na yasiyo na shaka ambayo wote wawili wamepewa kitakatifu." Haiwezekani kudhani kwamba vituo viwili vya mamlaka, ambavyo Bwana amevitamka ''vyote viwili vipo chini ya uangalizi na ulinzi wa Uzuri wa Abha, chini ya kivuli na uongozi usiokosea wa Mtukufu, Alietukuka", vingeweza kusuguana kimoja kwa kingine, kwa sababu vyote ni nyenzo za Uongozi mmoja Mtakatifu"

59.6 Mbali na jukumu lake kama mtunga sheria, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imepewa majukumu mengine zaidi ya jumla ya ulinzi na utawala wa Hoja, kutatua maswali yenye utata na kuamua juu ya masuala ambayo yamesababisha mfarakano. Hakuna popote palipoelezwa kwamba kutokosea kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutokana na ujumbe wa Mlinzi au uwepo kwenye shirika hilo. Kwa kweli Abdu'l-Baha katika Wasia Wake na Shoghi Effendi katika "Kipindi cha Baha'u'llah" wote wawili wameelezaa wazi kwamba wajumne waliochaguliwa wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa ushauriano ni wapokeaji wa Muongozo Mtakatifu usioshindwa. Zaidi, Mlinzi mwenyewe katika "Utaratibu wa Ulimwengu wa Baha'u'llah" alidai kwamba "Lazima pia ieleweke

kinagaubaga na kila muumini kwamba asasi ya Ulinzi kwa vyovyote haifuti, au hata kwa kiwango kidogo kabisa kupunguza, uwezo uliotolewa na Bahá'u'lláh kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika Kitáb-i-Aqdas, na imethibitishwa mara kwa mara na kwa dhati na 'Abdu'l-Bahá katika Wasia Wake. Haifanyizi kinyume kwa namna yoyote ile Wasia na Maandiko ya Bahá'u'lláh, wala haibatilishi maagizo Yake yoyote yaliyofunuliwa."

59.7 Wakati jukumu maalum la Mlinzi ni kufasiri Neno, pia yeye amepewa uwezo na haki ya lazima ya kutekeleza kazi yake kama Ulinzi wa Hoja, Mkuu wake na mlinzi mkuu kabisa. Vile vile, yeye amefanywa mkuu asiyeondoleka na mjumbe wa maisha wa shirika kuu la kutunga sheria la Imani. Ni kama mkuu wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, na kama mjumbe wa shirika hilo, kwamba Mlinzi hushiriki katika mchakakto wa kutunga sheria. Ikiwa kifungu kifuatacho, ambacho ndicho kilichoibua swali lako kitachukuliwa kama kinachorejelea kwenye uhusiano huu wa mwisho, utaona kwamba hakuna ukinzani baina yake na maandiko mengine.

> "Ingawa Mlinzi wa Imani amefanywa kuwa Mkuu wa kudumu wa chombo cha juu kabisa hawezi kamwe, hata kwa kitambo tu, kujinyakulia haki pekee ya kutunga sheria. Hawezi kufanya maamuzi dhidi ya uamuzi wa wajumbe-wenza walio wengi, lakini analazimika kusisitiza juu ya ufikiriwaji tena na wao wa sheria yoyote anayoamini kwa ufahamu wake kamili kuwa inapingana na maana na kukengeuka kutoka moyo wa maneno yaliyofunuliwa na Bahá'u'lláh."

59.8 Ingawa Mlinzi, katika uhusiano wake na wajumbe-wenza ndani ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hawezi kutengua uamuzi wa walio wengi, haifikiriki kwamba wajumbe wengine wangepuuza pingamizi lolote alilotoa wakati wa ushauriano au kupitisha sheria kinyume na kile alichoeleza kuwa hakiendani na dhamira ya Hoja. Hata hivyo, ni uamuzi wa mwisho ambao hutolewa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambao hukubaliwa kuwa hauwezi kuwa na makosa na siyo maoni yoyote

yaliyotolewayo wakati wa mchakato wa utungaji sheria hiyo

59.9 Inaweza kuonekana, kwa hiyo, kwamba hakuna msuguano baina ya matamko ya Bwana yahusuyo muongozo mtakatifu usioshindwa uliojaaliwa juu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na kifungu cha hapo juu kutoka “Kipindi cha Baha’u’llah.”

59.10 Inaweza kuwasaidia marafiki kuelewa uhusiano huu ikiwa watatambua baadhi ya michakato ambayo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huifuata wanapotunga sheria. Kwanza, kwa kawaida, inafanya uangalifu mkubwa kabisa kusoma maandiko matakatifu na fasiri ya Mlinzi na vile vile kufikiria maoni ya wajumbe wote. Baada ya ushauriano wa muda mrefu mchakato wa kuandika tamko huanza. Wakati wa mchakato huu suala zima vile vile linaweza kufikiriwa tena. Kama matokeo ya ufikiriaji huo mpya, uamuzi wa mwisho unaweza kwa kiwango kikubwa kuwa tofauti na ule uliofikiwa mwanzo, au labda inaweza kuamua isitunge sheria kabisa juu ya jambo hilo kwa wakati huo. Mtu anaweza kuelewa ni umakini mkubwa kiasi gani ungetolewa kwa maoni ya Mlinzi wakati wa mchakato wa hapo juu kama angekuwa bado hai.

59.11 Katika kuzingatia kifungu cha pili lazima kwa mara nyingine tena tushikilie kwa uthabiti ile kanuni kwamba mafundisho hayapingani yenyewe.

59.12 Walinzi wa siku zijazo wanafikiriwa kwa uwazi na kurejelewa kwenye Maandiko, lakini hakuna ahadi yoyote mahali popote pale au uhakikisho kwamba mfuatano wa Walinzi utadumu milele; kinyume chake kuna viashiria wazi kuwa mfuatano huu unaweza kukatika. Bado, licha ya hili, kuna msisitizo wa mara kwa mara katika Maandiko juu ya kutovunjika kwa Agano na Kusudi la Mungu lisilobadilika kwa Siku hii.

59.13 Mojawapo ya vifungu vinavyovutia mno ambavyo huashiria uwezekano wa kuvunjika huko katika mfuatano wa Walinzi kipo katika Kitab-i-Aqdas chenyewe:

Mali wakfu kwa ajili ya hisani hurejea kwa Mungu, Mfunuaji wa Ishara. Hakuna aliye na haki ya kuzitoa bila ruhusa kutoka kwa Yeye Ambaye ni mahali pa mapambazukio ya Ufunuo. Baada Yake, mamlaka haya yanaenda kwa Aghsan [Matawi], na baada yao kwa Nyumba ya Haki—iwapo itakuwa imesimikwa katika ulimwengu kwa wakati huo—ili kwamba waweze kutumia mali wakfu hizi kwa manufaa ya zile Sehemu ambazo zimekwisha tukuzwa ndani ya Hoja hii, na kwa ajili ya chochote ambacho kimeagizwa kwao na Yeye Ambaye ndiye Mungu wa uweza na nguvu. Vinginevyo, mali wakfu hizo zitarejeshwa kwa watu wa Bahá ambao huwa hawasemi ila kwa idhini Yake na wala hawahukumu ila kufuatana na kile ambacho Mungu ameamuru ndani ya Waraka huu, wao ni mashujaa wa ushindi katikati ya mbingu na dunia, ili kwamba waweze kuzitumia kwa namna ambayo imeamriwa ndani ya Kitabu Kitakatifu na Mungu, Mwenye Uwezo, Mkarimu.

59.14 Kufariki kwa Shoghi Effendi mnamo 1957 kuliharakisha hali yenyewe iliyotajwa kweye kifungu hiki, kwamba mfuatano wa Aghsan uliisha kabla ya kuchaguliwa kwa Nyumba ya Haki. Ingawa, kama inavyoonekana kwamba mwisho wa mfuatano wa Aghsan katika hatua fulani ulikuwa umezingatiwa, lazima kamwe tusidharau pigo kubwa ambalo Imani imelipata. Kusudi la Mungu kwa binadamu linabakia bila kubadilika, hata hivyo, na Agano lenye nguvu la Baha'u'llah linabakia lisiloingilika. Kwani Baha'u'llah hajaeleza kibainifu "Mkono wa Mwenye Nguvu Zote umesimika Ufunuo Wake juu ya msingi usioshambulika, unaodumu."
Wakati Abdu'l-Baha huthibitisha: "Kwa hakika, Mungu husababisha kile Yeye akipendacho; hakuna kinachoweza kufuta Agano Lake; Hakuna kinachoweza kuzuia mapenzi Yake wala kupinga Hoja Yake!" "Kila kitu kinaweza kuchafuliwa; lakini Agano la Bwana wako litaendelea kusambaa katika maeneo yote." "Majaribu ya kila kipindi yapo katika uwiano wa moja kwa moja na ukubwa wa Hoja, na mpaka sasa Agano dhahiri kama hili lililoandikwa na Kalamu Kuu Kabisa ambalo halikuwahi kufanyika, kiuwiano majaribu yamekuwa makali zaidi.... Mitikiso hii ya wakiukaji

si zaidi ya mapovu ya bahari,….Mapovu haya ya bahari hayatadumu na muda si mrefu yatatawanyika na kutoweka, wakati bahari ya Agano hujimwaga na kurindima milele.” Na Shoghi Effendi ameelezea wazi: “Msingi wa mwamba ambao juu yake Utaratibu wa Utawala umejengwa ni Kusudi la Mungu lisilobadilika kwa ajili ya binadamu katika siku hii….” “…kito hiki cha thamani kubwa cha Ufunuo Mtakatifu,kwa sasa kilicho katika hali yake ya uchanga, kitakunjuka ndani ya ganda la sheria Yake na kitasonga mbele bila mgawanyiko na bila kuharibiwa mpaka kitakapoikumbatia jamii yote ya binadamu.”

59.15 Katika Imani ya Kibaha’i kuna vituo viwili vya mamlaka vilivyoteuliwa ambavyo waumini lazima wavigeukie, kwa kuwa kiuhalisia Mfasiri wa Neno ni tawi la kituo hicho ambalo ni Neno lenyewe. Kitabu ni kumbukumbu ya matamshi ya Baha’u’llah, wakati mfasiri aliyevuviwa kitakatifu ni Mdomo hai wa Kitabu hicho—ni yeye na yeye peke yake anayeweza kusema kwa mamlaka kile Kitabu humaanishwa. Hivyo, kituo kimoja ni Kitabu na Mfasiri wake, na kingine ni Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ikiongozwa na Mungu kuamua chochote ambacho hakijafunuliwa wazi katika Kitabu. Mtindo huu wa vitovu na uhusiano wao ni dhahiri katika kila hatua ya ukunjukaji wa Hoja. Katika Kitab-i-Aqdas Baha’u’llah huwaambia waumini kurejea kwenye Kitabu baada ya kifo Chake, na kwa “Yule Ambaye Mungu amemkusudia, ambaye ametokana na huu Mzizi wa Kale.” Katika Kitab-i-Ahdi (Kitabu cha Agano la Baha’u’llah), Anaweka wazi kuwa rejeao hili ni kwa Abdu’l-Baha. Katika Aqdas Baha’u’llah pia huagiza asasi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na ameijaalia uwezo uhitajikao kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyoamriwa kwake. Bwana katika Wasia na Agano Lake kwa uwazi anaanzisha asasi ya Ulinzi, ambayo Shoghi Effendi anaeleza kwamba kwa uwazi ilitazamiwa katika aya za Kitab-i-Aqdas, huhakikisha na kufafanua tena mamlaka ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na kuwarejelesha waumini kwa mara nyingine tena kwenye Kitabu: “Kwenye Kitabu Kitakatifu Kabisa kila mmoja lazima ageukie na chochote ambacho hakijaandikwa kwa uwazi humo lazima kirejelewe Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.” Na mwisho kabisa wa Wasia Anasema:

Wote lazima watafute muongozo na wageukie kwenye Kituo cha Hoja na Nyumba ya Haki. Na yule ambaye hukigeukia kingine chochote kile hakika yumo katika kosa baya mno."

59.16 Wakati eneo la mamlaka la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika masuala ya utungaji sheria hupanuka hadi kwenye chochote ambacho hakijafunuliwa wazi wazi katika Maandiko Matakatifu, ni dhahiri kwamba Kitabu chenyewe ndiyo mamlaka ya juu kabisa na huondoa mipaka ya eneo la kiutendaji la Nyumba ya Haki. Vivyo hivyo, Mfasiri wa Kitabu lazima pia awe na mamlaka kuelezea eneo la kiutendaji la utungaji sheria la wawakilishi waliochaguliwa wa Hoja. Maandiko ya Mlinzi na ushauri utolewao naye katika kipindi cha miaka thelathini na sita ya Ulinzi wake huonesha jinsi alivyotekeleza jukumu hili kuhusiana na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na vile vile na Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na ya Mahali.

59.17 Ukweli kwamba Mlinzi ana mamlaka ya kuelezea mipaka ya eneo la kiutendaji la utungaji sheria la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haubebi hatima ya kwamba bila muongozo huo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inaweza kupotoka mbali na mipaka yake ya mamlaka stahiki; upunguzaji kama huo ungepingana na maandiko mengine yanayorejelea kwenye kutokosea na madai dhahiri ya Mlinzi kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haiwezi na kamwe haitaweza kuingilia miliki takatifu na iliyoamriwa ya Ulinzi. Inapaswa ikumbukwe, hata hivyo, kwamba ingawa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na ya Mahali yaweza kupokea uongozi mtakatifu ikiwa yatashauriana katik hali na moyo kama ilivyoelezewa na Abdu'l-Baha, hayahusiki katika uhakikisho wa wazi wa kutokosea uliojaaliwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Mwanafunzi yeyote makini wa Hoja anaweza kuona ni kwa umakini gani Mlinzi alivyowaongoza wawakilishi hawa waliochaguliwa wa waumini baada ya kufariki kwa Abdu'l-Baha katika uinuaji wenye sulubu wa Utaratibu wa Kiutawala na katika uundwaji wa Katiba za Mahali na za Kitaifa za Kibahà'í.

59.18 Tunatumaini kwamba ufafanuzi huu utawasaidia marafiki katika kuelewa uhusiano kwa uwazi zaidi, lakini lazima wote tukumbuke

kwamba tunasimama karibu mno na vyanzo vya Mfumo ulioamriwa na Baha'u'llah kuweza kuelewa kikamilifu uwezo wake uliofichika au muingiliano baina ya sehemu zake zinazouunda. Kama katibu wa Shoghi Effendi alivyoandika kwa niaba yake kwa mtu binafsi 25 Machi,1930, "Maudhui ya Wasia wa Bwana yapo mbali mno kwa kizazi cha sasa kuyafahamu. Inahitaji angalau karne nzima ya kazi halisi kabla hazina zenye hekima zilizofichwa humo kuweza kufunuliwa…"
*(Kutoka barua ya 7 Desemba 1969 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

60.1 Ingawa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inapaswa kutumia na kujaliza sheria za Aqdas haina haki kabisa kubadilisha sheria yoyote ambayo ilifunuliwa wazi wazi na Baha'u'llah. Kama ilivyoelezwa kwa uwazi na Mlinzi, maelekezo ya Kitab-i-Aqdas yanabakia yasiyokiukwa katika Kipindi Chake chote.
*(Kutoka barua ya 28 Aprili,1974 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

61.1 Agano katika maana ya kidini ni makubaliano yanayofunga baina ya Mungu na mwanadamu, ambapo Mungu humtaka mwanadamu kuwa na tabia fulani ambayo kwayo humhakikishia baraka fulani, au pale ambapo Yeye humpa mwanadamu karama fulani ambapo Yeye hupokea kutoka kwa wale wanaokubali kuenenda kwa namna fulani. Kwa mfano, kuna Agano Kuu ambapo kila Mdhihirishaji wa Mungu hufanya na wafuasi Wake, akiwaahidi kwamba wakati ufikapo Mdhihirishaji mpya atatumwa na akiwataka kujiandaa kumkubali wakati hili litokeapo. Pia kuna Agano Dogo ambalo Mdhihirishaji hufanya na wafuasi Wake kwamba watamkubali mrithi Wake mteule baada Yake. Ikiwa watafanya hivyo, Imani itabaki imeunganika na iliyotakasika. La sivyo, Imani itagawanyika na nguvu yake kupotea. Ni Agano la aina hii ambalo Baha'u'llah alifanya na wafuasi Wake kuhusu Abdu'l-Baha na kwamba Abdu'l-Baha aliliendeleza kupitia Utaratibu wa Utawala ambao Baha'u'llah alikwishauunda.
*(Kutoka barua ya 23 Machi, 1975 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

62.1 Kuhusu swali lako la kwanza, ni muhimu unapofikiria kuhusu Ulinzi katika maandiko ya Imani na hasa wakati unapojitahidi kuelewa jinsi rejea hizi zinavyotumika kwa wakati huu, unapaswa utambue kwamba neno "Ulinzi" linatumika kwa maana nyingi kwa muktadha tofauti. Katika muktadha fulani humaanisha ofisi na majukumu ya Mlinzi mwenyewe, kwa mwingine hurejelea kwenye mfuatano wa Walinzi, na bado katika nyingine hubeba maana pana zaidi ikumbatiayo Mlinzi na asasi zinazomsaidia katika huduma. Hata hivyo, itakuwa si sahihi kabisa kusema kwa sasa ambapo hakuna Mlinzi kuwa Mikono wa Hoja ni wajumbe wa shirika la Ulinzi. Wala haitakuwa sahihi kuita hivyo Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, washauri, washauri wasaidizi na wasaidizi wao.

62.2 Katika maana maalum ya kurejelea ofisi na majukumu ya Mlinzi mwenyewe, Nyumba ya Haki hutambua kwamba haki na wajibu aliokabidhiwa ni wa aina tatu. Kwanza, kama ilivyoelezwa kwenye barua kwa muumini binafsi ambayo ilichapishwa kwenye "Chemchemi ya Uongozi"7 kuna majukumu na malengo ambayo Mlinzi hushirikiana na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo ni lazima Nyumba ya Haki iendelee kuyafuatilia. Pili, kuna majukumu mengine ya Ulinzi ambayo kwa kutokuwepo kwa Mlinzi huhamia kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kwa mfano, Ukuu wa Imani, wajibu wa kusimamia kazi za Asasi ya Mikono wa Hoja ya Mungu na kuhakikisha kuendelea kwa utekelezaji wa majukumu ya ulinzi na uenezaji ambayo yamekabidhiwa kwa Asasi hiyo, na haki ya kusimamia Huququ'llah. Tatu, kuna zile haki na wajibu ambavyo vimo katika eneo la Mlinzi mwenyewe tu, na kwa hiyo kwa kutokuwepo kwa Mlinzi hayafanyi kazi isipokuwa kama kazi ya kumbukumbu bora iliyokwishafanywa na Shoghi Effendi ambayo huendelea kuwa yenye manufaa ya kudumu kwa Imani. Kazi hiyo ni kama ile ya mamlaka ya kufasiri mafundisho.
*(Kutoka barua ya 5 Mei, 1977 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

63.1 Shoghi Effendi aliulizwa mara nyingi wakati wa utumishi wake kuelezea mipaka ya eneo lake la kiutendaji na kutokufanya kwake makosa. Majibu aliyotoa na ambayo yaliandikwa kwa niaba yake yanatoa mwanga kabisa. Anaelezea kwamba hana mamlaka ya kutokosea katika maeneo kama uchumi na sayansi, na wala hawezi kuingia kwenye masuala ya kitaalamu kwa kuwa kutokosea kwake kunahusiana tu na "mambo ambayo yanahusiana hasa hasa na Hoja".

Anaonesha zaidi kuwa "yeye si kama ilivyo kwa Nabii, mwenye maarifa yote'', kwamba kutokosea kwake hujumuisha ufafanuzi wa neno lililofunuliwa na matumizi yake" na kwamba pia kutokosea kwake kunahusu fasiri ya neno lililofunuliwa, na matumizi yake", na kwamba pia "hafanyi makosa katika ulinzi wa Imani." Zaidi ya hapo, katika mojawapo ya barua, muongozo ufuatao unawekwa:

> Si ruksa kwa waumini binafsi kuwekea mipaka eneo la mamlaka ya Mlinzi, au kuamua ni wakati gani wanapaswa kumtii Mlinzi na wakati gani wana uhuru kukataa maamuzi yake. Tabia kama hiyo husababisha mkanganyiko na mfarakano. Mlinzi akiwa ndiye mfasiri mteule wa mafundisho, ni wajibu wake kusema ni mambo gani yanaathiri maslahi ya Imani na kudai kwa upande wa waumini utii kamili na usio na masharti kwa maagizo yake.

63.2 Lazima daima ikumbukwe kwamba fasiri yenye mamlaka ya Mafundisho ilikuwa, baada ya Abdu'l-Baha, haki ya Mlinzi peke yake, na iliangukia katika "miliki takatifu na iliyoagizwa" ya Ulinzi, na kwa hiyo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haiwezi na haitaweza kuingilia miliki hiyo. Eneo pekee ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ni "kutamka na kutoa uamuzi wa mwisho juu ya sheria na amri ambazo Baha'u'llah hakuzifunua wazi wazi." Eneo pekee ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ni "kutamka na kutoa uamuzi wa mwisho juu ya sheria na amri ambazo Baha'u'llah hakuzifunua wazi wazi." Mbali na tofauti hii ya msingi katika kazi za nguzo pacha za Utaratibu wa Baha'u'llah, kwa kadiri majukumu mengine ya Mkuu wa Imani yahusikavyo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu

inashirikiana na Mlinzi majukumu ya utumiaji wa neno lililofunuliwa, ulinzi wa Imani, vile vile wajibu wa “kuhakikisha muendelezo wa yale mamlaka matukufu yaliyoteuliwa ambayo hutiririka kutoka Chanzo cha Imani yetu, kulinda umoja wa wafuasi wake na kutunza uadilifu na unyumbulikaji wa Mafundisho yake”. Hata hivyo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu siyo yenye maarifa yote; kama alivyo Mlinzi, inataka ipewe kweli zote inapotakiwa kufanya uamuzi, na kama yeye, inaweza vile vile kubadilisha uamuzi wake kama kweli mpya huibuka.
*(Kutoka barua ya 22 Agosti, 1977 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

64.1 … Nyaraka za Mpango Mtakatifu ambazo zilifunuliwa na Abdu’l-Baha wakati wa Vita ya Kwanza ya Dunia, ni Hati ya ufundishaji wa Imani. Mipango yote ya ufundishaji iliyozinduliwa na mpendwa Mlinzi, vile vile ile iliyoelekezwa baadaye na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, na hatua za utekelezaji wa mpango huu mkuu uliyobuniwa na Kitovu cha Agano kwa ajili ya utawanyaji wa Ujumbe wa Baha’u’llah.

64.2 Wakati inapoweka malengo ya mpango, kama vile Mpango wa Miaka Mitano, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa kushirikiana na Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa hulinganisha taarifa za hali ya sasa ya Imani duniani kote, hufikiria hali ya jamii ya binadamu kwa ujumla na muelekeo ambao matukio ya kisiasa na kiuchumi za dunia zinavyokwenda, huweka fikra juu mahitaji maalum ya mtindo unaobadilika wa jumuiya ya Kibahà’í katika kila nchi na kuweka malengo ambayo kuzingatia taarifa zilizo mbele yake, huamua juu ya mambo mawili; umuhimu wa upatikanaji na pia uwezo wa jumuiya za Kibahà’í kuyafikia. Malengo yote yanayowekwa hivyo ni kwa uchache; hivyo ndiyo kusema kwamba mahitaji ya binadamu ni makubwa mno kuliko chochote ambacho jumuiya ya Kibah inaweza kupanga kutimiza kwa muda huu, na kwa hiyo, ingawa malengo yanawekwa kuwa juu kwa kiwango ambacho Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huona inawezekana kwa Wabahà’í kuyafikia kwa muda uliotolewa, marafiki hawana budi kujitahidi kuyavuka ikiwa wanaweza.

64.3 Katika kuweka malengo Nyumba ya Haki haiwezi kutegemea utendaji usiotabirika wa Mpango Mkuu wa Mungu. Wakati mwingine yaweza kuonekana kwabma utendaji wa Mpango Mkuu huingilia kazi ya Mpango Mdogo, lakini marafiki wasiruhusu hili liwahuzunishe. Mnamo 1955 kuzuka tena kwa ghafla kwa mateso kwa Imani katika nchi ilimozaliwa kuliingilia kati kwa mfululizo maendeleo ya Mpambano wa Miaka Kumi.

Akirejelea hili Mlinzi aliandika, kama ilivyonukuliwa katika ukurasa wa 140 wa "Citadel of Faith";

> Ingawa Mpambano wa Kiroho wa Kidunia uliozinduliwa hivi karibuni, ukijumuisha hasa Mpango Mdogo tu katika utekelezaji wa kusudi la Mwenyezi kwa ajili ya ukombozi wa binadamu—kama matokeo ya msukosuko huu umewanyong'onyeza kwa muda wafuasi wengi mno waliojiandaa wa Baha'u'llah ndani ya nchi alimozaliwa, walipatwa na kikwazo kikubwa mno—hata hivyo Mpango wa jumla wa Mungu ukisonga mbele kimiujiza na ukiwa kinyume na michakato iliyopangiliwa na kujulikana vyema ya Mpango uliobuniwa kwa uwazi, umepata msukumo kwa uwezo ambao vizazi vijavyo tu vitaweza kutathmini vya kutosha.
> *(Kutoka barua ya 29 Septemba, 1977 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

65.1 Umeelezea hofu kwamba mamlaka aliyovikwa 'Abdu'l-Bahá, Mlinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu yanaweza kusababisha kuendelea kupungua katika "uwepo wa nafasi kwa ajili ya fasiri binafsi", na kwamba "maandiko halisi ya Mdhihirishaji yatapungua maana zaidi na zaidi", na unafanisha na kile kilichotokea katika Vipindi vilivyotangulia. Nyumba ya Haki inapendekeza kwamba, katika kufikiria juu ya hili tafakari jinsi Agano la Baha'u'llah kwa uhalisia lilivyofanya kazi na utaweza kuona jinsi ilivyo tofauti kabisa michakato yake kutoka ile ya, mfano, maendeleo ya sheria za Kirabbi ya Kiyahudi au utendaji wa Upapa katika Ukristo. Mazoea ya siku zilizopita katika dini hizi mbili, na pia kwa kiasi kikubwa katika Uislamu, yamekuwa kudhania kwamba Ufunuo uliotolewa na

Muasisi ulikuwa wa mwisho, ufunuo kamili wa Mapenzi ya Mungu kwa binadamu, na ufafanuzi wote uliofuata na utungajji wa sheria umekuwa wenye kufasiriwa kwa maana ya kwamba umelenga kutumia Ufunuo huu wa msingi kwa matatizo mapya na hali zilizojitokeza. Mantiki ya Kibaha'i tofauti kabisa. Ingawa Ufunuo wa Baha'u'llah unakubaliwa kama Neno la Mungu na Sheria Yake kama Sheria ya Mungu, inaeleweka toka mwanzo kabisa kwamba Ufunuo endelevu, na kwamba Sheria, ingawa Mapenzi ya Mungu kwa Wakati huu, pasipo shaka itabadilishwa na Mdhihirishaji ajaye wa Mungu. Pili, ni neno lililoandikwa tu la Ufunuo litachukuliwa kuwa lenye mamlaka. Hakuna Sheria ya Maneno kama ilivyo katika Uyahudi, hakuna Mapokeo ya Kanisa kama ilivyo katika Ukristo, hakuna Hadithi kama ilivyo katika Uislamu. Tatu, tofauti dhahiri imewekwa kati ya tafsiri na utungaji sheria. Fasiri yenye mamlaka ni haki ya Abdu'l-Bahá na Mlinzi pekee, wakati jukumu la utungaji sheria bila kukosea ni la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

65.2 Ukisoma Maandiko ya Abdu'l-Baha na Mlinzi, utaona jinsi tofauti ilivyo kubwa kutoka fasiri za Marabbi na Kanisa. Siyo visukuku endelevu vya Ufunuo, kwa sehemu kubwa ni maelezo ya kuweka wazi vifungu ambavyo vinadhaniwa kuwa vyenye utata, wanaonesha muingiliano wa karibu sana baina ya mafundisho mbalimbali, wanaeleza kwa kinaganaga athari za vidokezo vya maandiko, na wanawaelimisha Wabahà'í thamani kubwa ya Maneno ya Baha'u'llah. Kwa namna yoyote ile badala ya kuchukua nafasi ya Maneno ya Mdhihirishaji wanatuvuta kwao kila wakati.

65.3 Pia kuna tofauti muhimu iliyofanywa kati ya fasiri yenye mamlaka kama ilivyoelezwa hapo juu na fasiri ambayo kila muumini ana haki kabisa ya kuisemea. Waumini wapo huru, hakika wanatiwa moyo kujifunza Maandiko kwa ajili yao wenyewe na kuelezea uelewa wao wa hayo maandiko. Fasiri binafsi kama hizo zinaweza kuwa zenye kuangazia sana, lakini Wabahà'í wote, akiwemo yule anayeelezea maoni yake hata awe ameelimika kiasi gani, wanapaswa kutambua kwamba ni maoni binafsi tu

na hayawezi kuchukuliwa kama kipimo kwa wengine kuyakubali na wala mabishano hayapaswi kuibuka juu ya tofauti za maoni kama hayo.

65.4 Sheria iliyotungwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ni tofauti na fasiri. Fasiri yenye mamlaka kama ilivyotamkwa na Abdu'l-Baha na Mlinzi ni kauli ya muongozo mtakatifu ya kile kinachomaanishwa na Neno la Mungu. Utungaji sheria uliovuviwa kitakatifu wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haujaribu kusema kile ambacho Neno lililofunuliwa humaanisha—hueleza kinachopaswa kufanyika pale ambapo Neno lililofunuliwa au fasiri yake yenye mamlaka haipo bayana. Kwa hiyo, ni kwa kiwango tofauti kutoka Andiko Takatifu, na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imewezeshwa kufuta au kurekebisha sheria zake yenyewe wakati wowote inapoamua kwamba hali inapofanya hilo kuhitajika. Zaidi, muelekeo wa kutunga sheria ni tofauti katika Imani ya Kibahà'í. Tabia ya binadamu katika Vipindi vilivyopita imekuwa kutaka kila swali lijibiwe na kufikia maamuzi yenye kufunga yakigusa kila utondoti mdogo wa imani au kitendo. Tabia katika Kipindi cha Kibahà'í tangu wakati wa Baha'u'llah mwenyewe imekuwa ni kubainisha kanuni zinazoongoza, kufanya matamko yanayofunga juu ya tondoti ambazo huonekana muhimu, lakini kuacha eneo pana kwa ajili ya dhamira ya mtu binafsi. Tabia kama hiyo hiyo pia huonekana katika mambo ya kiutawala. Mlinzi alizoea kueleza kwamba ufanyaji kazi wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa unapaswa kuwa wa namna moja kwa mambo muhimu lakini utofauti katika ngazi ya pili siyo tu unaruhusiwa bali unahitajika. Kwa sababu hii, dondoo kadhaa hazielezewi katika Katiba ya Mabaraza ya Kitaifa (Maazimio ya Dhamana na Sheria Ndogo ndogo za Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa), haya yameachiwa kila Baraza la Kiroho la Kitaifa kuamua kwa ajili yake lenyewe.

*(Barua ya 3 Januari, 1982 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

66.1 Wakati hatimaye jukumu kuu la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu litakuwa ni lile la utungaji sheria, lina wajibu endelevu kwa ajili ya kazi za kiutawala na za kisheria za asasi.
*(Kutoka barua ya 19 Mei, 1985 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa)*

67.1 Barua yako inagusia mada ambayo kadiri muda upitavyo itaendelea kwa kiasi kikubwa kuvuta umakini wa Nyumba ya Haki kulingana na madaraka yake iliyopewa kwa udhahiri kwenye Maandiko Matakatifu. Kwa mfano Baha'u'llah hueleza:

> Kulingana na sheria za msingi ambazo tayari Tumezifunua kwenye Kitab-i-Aqdas na Nyaraka zingine, mambo yote yamewekwa kwenye uangalizi wa wafalme wa haki na maraisi na Wadhamini wa Nyumba ya Haki.
> *(Tablets of Baha'u'llah Revealed after the Kitab-i-Aqdas, pg.93)*

Na sehemu nyingine huelezea:

Inawapasa wajumbe wa Nyumba ya Haki kuchochea Amani Ndogo ili kwamba watu wa dunia waweze kupata ahueni kutokana na mzigo wa gharama iliyokithiri ya matumizi. Suala hili ni la haraka na muhimu kabisa maadam uhasama na migogoro vimo katika mzizi wa mateso na maafa.
*(Tablets of Baha'u'llah Revealed after the Kitab-i-Aqdas, pg.89)*

Na tena Anadai;

Masuala yote ya nchi lazima yarejelewe kwa Nyumba ya Haki, lakini matendo ya ibada lazima yafanywe kulingana na vile Mungu alivyofunua katika Kitabu Chake.
*(Tablets of Baha'u'llah Revealed after the Kitab-i-Aqdas, pg.27)*

Zaidi ya hapo, 'Abdu'l-Bahá alinukuliwa akisema katika mazungumzo:

Yeye [Bahá'u'lláh] ameamuru na kuanzisha Nyumba ya Haki ambayo imejaliwa wajibu wa kisiasa na kidini, muungano kamili na upatanisho wa kanisa na dola. Asasi hii ipo chini ya nguvu ya ulinzi ya Baha'u'llah.

Mwenyewe.
*("Promulgation of Universal Peaceu", 1982, pg. 455)*

67.2 Kama inavyoweza kuonekana kutoka hali ya sasa ulimwenguni na hali ya sasa katika maendeleo ya jamuiya ya Kibaha'i, matamko kama haya huonesha hatua ya baadaye katika utendaji wa Nyumba ya Haki na ya uendeshaji wa jumuiya yetu ya ulimwengu; lakini kwa sasa, Nyumba ya Haki itabaini, kadiri hali mahsusi zitakavyoruhusu, jinsi Wabahà'í na asasi zao za kitaifa na za mahali zitakavyohusiana na serikali zao.
*(Kutoka barua ya 23 Juni, 1987 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

68.1… lazima izingatiwe kwamba katika maeneo mengi ya tabia ya mwanadamu kuna matendo ambayo ni dhahiri yapo kinyume na sheria ya Mungu na mengine ambayo ni dhahiri yanakubalika au kuruhusiwa; kati ya haya mara nyingi kuna eneo la shughuli zisizokuwa na muelekeo ambalo haifahamiki mara moja nini kifanyike. Imekuwa ni mazoea ya binadamu kupenda kuondoa maeneo haya ya shughuli zisizo kuwa na muelekeo ili kwamba kila nyanja ya maisha ielezeke kwa uwazi. Matokeo ya mwelekeo huu yamekuwa ni ongezeko kubwa sana la fasiri na uwekaji sheria za ziada ambazo zimekandamiza moyo wa uhakika wa dini za zamani. Katika Imani ya Kibahà'í, kiasi, ambacho kinatetewa kwa nguvu kubwa na Baha'u'llah kinatumika hapa pia. Nafasi inatolewa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kutunga sheria za kujazilizia—utungaji ambao yenyewe yaweza kufuta na kurekebisha kadiri hali zinavyobadilika. Pia kuna ruwaza dhahiri ambayo tayari imeanzishwa katika Maandiko Matakatifu, katika fasiri zilizifanywa na Abdu'l-Baha na Shoghi Effendi, na katika maamuzi ambayo hadi sasa yamefanywa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambapo eneo la matumizi ya sheria linaachwa kwa makusudi kwa dhamira ya kila muumini binafsi. Hizi ni zama ambamo binadamu lazima wafikie upevu, na sura moja ya hii ni kuchukulia kwamba watu binafsi wana wajibu wa kuamua, kwa msaada wa ushauriano, njia ya utendaji wao wenyewe katika maeneo ambayo yameachwa wazi na sheria ya Mungu.

68.2 Pia lazima izingatiwe kwamba haiwezekani na wala haipendelewi kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kuweka orodha ya kanuni zinazotosheleza kila hali. Badala yake ni kazi ya kila muumini binafsi kuamua, kulingana na uelewa wake wa Maandiko baada ya kujizamisha katika sala, kwa usahihi ni njia yake ipi ya kufuata kulingana na hali anazokutana nazo katika maisha ya kila siku. Ikiwa anataka kutimiza wito wake katika maisha kama mfuasi wa Ukamilifu Uliobarikiwa atapangilia maisha yake kulingana na Mafundisho. Muumini hawezi kufikia kusudi hili kwa kuishi tu kulingana na orodha ya taratibu zisizonyumbulika. Maisha yake yanapoelekezwa kwenye huduma kwa Baha'u'llah na wakati kila kitendo chenye utambuzi hufanyika ndani ya umbo hili la marejeleo, hatashindwa kufikia kusudi la kweli la maisha.

68.3 Kwa hiyo, kila muumini lazima aendelee kusoma Maandiko Matakatifu na maelekezo ya mpendwa Mlinzi, akijitahidi daima kufikia uelewa mpya na bora zaidi wa maana zake kwake na kwa jamii yake. Anapaswa asali kwa bidii kwa ajili ya muongozo mtakatifu, hekima na nguvu kufanya kinachompendeza Mungu, na kumtumikia Yeye muda wote na kwa uwezo wake wote.
*(Kutoka barua ya 5 Juni, 1988 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

69.1 Mojawapo ya mambo makubwa sana yanayohusu Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kadiri Utaratibu wa Kiutawala wa Kibahà'í unavyokunjuka, litakuwa kuhakikisha kwamba unasonga mbele kuendana na moyo wa Ufunuo wa Kibaha'i. Wakati vipengele vingi vyenye manufaa kwa jamii ya binadamu kwa jumla vyaweza kwa usalama kujumuishwa kwenye Utawala wa Kibahà'í, Nyumba ya Haki itakinga dhidi ya ushawishi wenye uharibifu wa dhana na vitendo vya kisiasa na kijamii visivyo vya Kibaha'i ambavyo havipo katika upatano na viwango vitakatifu.
*(Kutoka barua ya 27 Aprili,1995 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

70.1 Nyumba ya Haki imeambua kwamba umekuwa ukisumbuliwa na baadhi ya maandishi yaliyowekwa katika kundi la majadiliano la baruapepe ambalo umekuwa mshiriki hivi karibuni. Makundi ya mijadala ya barua pepe ni jambo jipya; yanaweza kutoa faida kubwa mno kwa ajili ya mawasiliano baina ya watu na kwa ajili ya kufundisha Imani, lakini, kama ulivyoona yanaweza pia kuibua matatizo yanayoweza kufika maeneo ya mbali. Matumizi ya barua pepe yanahitaji marekebisho ya mtazamo. Wakati uliopita, majadiliano baina ya Wabahà'í yangefanyika kwa mdomo kati ya vikundi vya marafiki pekee yao au katika shule za kiangazi na matukio mengine ya Kibahà'í au kwa barua baina ya watu binafsi. Bila kutarajiwa, kauli nyingi zenye makossa zilitolewa; siyo maoni yote yalikuwa ya kiasi kama yalivyotakiwa kuwa; kauli nyingi hazikueleweka kwa wale waliozisikia. Hata hivyo, si Wabahà'í wote wana uelewa wa kina wa mafundisho, na ni dhahiri kwamba hata umaarufu wa kitaaluma siyo kigezo cha kuelewa kwa sahihi Ufunuo wa Mungu. Kabla ya baruapepe matumizi yaliyokithiri ya namna hiyo yalikuwa na mipaka na yenye asili ya muda mfupi. Sasa, majadiliano ya aina hiyo yanasambaa baina ya watu kwa mamia au zaidi, ambao mara nyingi hawafahamiani, yapo katika mfumo wa kudumu kuliko wa kuongea na yanaweza kusambazwa kwa wasomaji wengi kwa kugusa tu kitufe. Kiwango kipya cha nidhamu, binafsi kwa hiyo, kinahitajika kwa wale wanaoshiriki. Majadiliano kama hayo baina ya Wabaha'i yanahitaji kujihini na usafi wa nia na vile vile ukunjufu, ukweli na uwazi.

70.2 Kiini, kitu kiunganishayo cha Imani ni Agano. Hii ni asasi ambayo huhakikisha kwamba Imani na mafundisho yake yatabaki halisi kwa Ufunuo ulioletwa na Baha'u'llah na kufafanuliwa na Wafasiri Wake walioongozwa kitakatifu. Ni wakala mmoja ambaye anaweza kuilinda Imani dhidi ya upotoshaji na uharibifu ambao Funuo zote zilizotangulia zimesababishiwa kwa juhudi—iwe kwa nia njema au la—ya maoni binafsi na ya tamaa baina ya wafuasi wao kuilazimisha Hoja ya Mungu katika mitindo ambayo wao binafsi hupendelea.

70.3 Hivyo, kama mshiriki yeyote katika majadiliano ya baruapepe huhisi kwamba maoni yaliyotolewa huonekana kupingana au kudhoofisha vipengele vya Agano, ajisikie huru kusema hivyo, akieleza kwa uwazi na adabu kwa nini anahisi kama anavyojihisi. Yule aliyetoa kauli ya kwanza sasa ataweza kutathmini upya maoni yake na kama bado anaamini yupo sawa, anapaswa aweza kuelezea kwa nini hayapo kinyume na ama maandiko au kwa moyo wa Agano. Washiriki katika mjadala kama huo wanapaswa waepuke mabishano na kama hawawezi kutatua suala hilo, wanapaswa kulirejelea suala hilo kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa kuwa, kwa mujibu wa Wasia na Agano la Abdu'l-Baha, "Kwa shirika hili matatizo yote magumu yatapata ufumbuzi… "na lina mamlaka kuamua juu ya "matatizo yote ambayo yamesababisha tofauti, maswali ambayo ni ya utata na mambo ambayo hayajaandikwa wazi wazi katika Kitabu." Kwa njia hii Agano linaweza kuangazia na kutuliza majadiliano na kuyafanya yenye manufaa….

70.4 Utaratibu wa Utawala wa Baha'u'llah upo katika mchakato wa ukuaji na ukunjukaji. Katika muundo na ufanyajikazi wake kuna vipengele ambavyo, Mlinzi alieleza, vinapaswa kuwa sawa sawa kote duniani. Pia kuna vipengele vinavyofuata ambavyo vinaweza kuwa tofauti kutoka nchi hadi nchi kama ilivyoamuliwa na Baraza la Kiroho la Kitaifa husika kulingana na mahitaji na hali katika eneo lililo chini ya mamlaka yake. Vipengele ambavyo lazima viwe sawa sawa vimeoneshwa katika Katiba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Katiba za Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na ya Mahali.

70.5 Kadiri jumuiya za Kibahà'í zinavyokua, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itahakikisha kwamba mfumo huu ulioanzishwa kitakatifu utakunjuka kulingana na muongozo usiokosea ambao yenyewe ndiyo mpokeaji.

70.6 Wale ambao wakati hadi wakati huonesha kutoridhishwa na muundo wa sasa wa Utaratibu wa Utawala wangeshauriwa vyema zaidi kuelekeza umakinifu wao katika kujifunza kikamilifu kanuni ambazo juu yake umejengwa, kama ilivyofafanuliwa na Abdu'l-Baha na Shoghi Effendi, na

kumakinikia juhudi zao katika kuweka katika vitendo moyo na maandishi ya maandiko haya. Kwa ukweli kila tatizo ambalo hulalamikiwa kwa mapungufu ya muundo kwa kweli linaweza kufuatiliwa hadi kwenye dosari kwa namna ambavyo waumini binafsi huelewa na kutekeleza kanuni za kiutawala za Imani.

70.7 Katika "Kipindi cha Baha'u'llah", Shoghi Effendi husema:
Utaratibu huu mchanga wa Utawala hujumuisha katika muundo wake vipengele kadhaa ambavyo hukutwa katika kila mojawapo ya mifumo itambulikayo ya serikali za kidunia, bila kuwa durufu kwa namna yoyote ya yoyote mojawapo; na bila kuingiza katika mfumo wake sura zozote za upingaji ambazo kiasili wanazo.
70.8 Mifumo mitatu ya serikali za kidunia ambayo Mlinzi huirejelea ni autokrasia (utawala wa mtu mmoja), aristokrasia (utawala wa watu bora) na demokrasia (utawala wa watu wote). Akirejelea tena kwenye mifumo hii mitatu ya serikali za kidunia, Mlinzi huandika baadaye katika hati hiyo hiyo:

Ambapo haiwezi kusemwa kuwa Utaratibu huu wa Utawala umeundwa kwa kuiga mifumo yoyote kati ya hii inayotambulika ya kiserikali, hata hivyo unajumuisha, kupatanisha na kulishizwa ndani ya umbo lake vipengele vya jumla kama vile vipatikanavyo katika kila mmoja wapo. Mamlaka ya kiurithi ambayo Mlinzi ameitwa kuyatumia, majukumu ya lazima na muhimu ambayo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huyatekeleza, maelekezo mahsusi yakihitaji uchaguzi wa kidemokrasia unaofanywa na wawakilishi wa waumini—haya kwa pamoja huonesha ukweli kwamba Utaratibu huu mtakatifu uliofunuliwa, ambao hauwezi kamwe kutambulishwa na aina nyingine yoyote ya serikali iliyotajwa na Aristotle katika kazi zake, hujumuisha na kuchanganya kweli za kiroho ambamo vimejengwa vipengele vyenye manufaa ambavyo hukutwa katika kila mojawapo. Maovu yaliyokubalika kiasili katika kila moja ya mifumo hii yakitengwa king'ang'anivu na kwa kudumu, Utaratibu huu wa kipekee, hata udumu kwa muda mrefu kiasi gani na hata ukizaa matawi yake mengi kiasi gani, hauwezi kamwe kuharibika na kuwa katika hali yoyote ya

kiimla, utawala wa wachache au utawala wa kimihemko ambao punde au baadaye utaharibu miundo yote iliyobuniwa na binadamu na hasa asasi za kisiasa zenye kasoro.

70.9 Katika kitabu "God Passes By" Mlinzi anatoa maoni zaidi juu ya mada ya sifa za Utaratibu wa Utawala wa Kibaha'i:

Unajumuisha katika muundo wake vipengele fulani ambavyo hupatikana kwenye kila mfumo wa ile mitatu inayotambulika ya serikali za kidunia, hauna kasoro ambazo kila mmoja kiasili unazo na huchanganya ukweli ufaao ambao kila mmoja bila shaka unao bila kuharibu kwa namna yoyote uadilifu wa kweli Takatifu ambamo kimsingi umejengwa. Mamlaka ya kiurithi ambayo Mlinzi ameitwa kuyatumia, na haki ya kufasiri Maandiko Matakatifu aliyopewa yeye pekee; mamlaka na haki ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ikiwa na haki peke yake ya kutunga sheria juu ya masuala ambayo hayajafunuliwa wazi wazi katika Kitabu Kitakatifu Kabisa; sheria inayowasamehe wajumbe wake wajibu wowote kutoka kwa wale wanaowawakilisha, na kutoka wajibu wa kupatana na maoni yao, misimamo au hisia zao; maelekezo mahsusi yanayohitaji uchaguzi huru na wa kidemokrasia wa umma wa waaminifu wa Shirika ambalo huunda chombo pekee cha kutunga sheria katika jumuiya ya Kibahà'í kote duniani—hizi ndizo baadhi ya sifa ambazo huungana kutenganisha Utaratibu uliotambulishwa na Ufunuo wa Baha'u'llah kutoka mfumo wowote uliopo wa serikali ya watu.

70.10 Ingawa Utaratibu wa Utawala sasa lazima ufanye kazi bila kuwa na Mlinzi aliye hai, na hivyo bila chanzo endelevu cha fasiri zenye mamlaka ziongozwazo kitakatifu, vipengele vyenye manufaa vya aina zote tatu za serikali bado vimeunganishwa ndani ya Utaratibu huu: katika mamlaka yanayoendelea ya Neno Takatifu na matokeo yafungayo ya fasiri za Abdu'l-Baha na Mlinzi; juu ya wajibu wa wajumbe wa Nyumba ya Haki "kufuata kwa mwelekeo wa kiibada maamrisho na ushawishi wa dhamiri zao" bila kuongozwa na "hisia, maoni ya jumla na hata misimamo ya umma wa waaminifu…"; katika uchaguzi (wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja) wa wajumbe wa mashirika yote ya kiutawala kwa kura huru ya

umma wa waumini, bila ushawishi wa mapendekezo au kampeni na bila kusumbuliwa kwa moyo wa makundi na uroho wa madaraka ambazo ni tabia za kawaida za jamii ya sasa. Juu ya yote, una mizizi mirefu katika "kweli za kiroho" zilizofunuliwa na Baha'u'llah.

70.11 Katika miaka baada ya kuandikwa kwa maneno yaliyonukuliwa hapo juu, aidha, Shoghi Effendi siyo tu kwamba alichapuza mchakato wa kuunda Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa kuteua Halmashauri ya Kimataifa ya Kibaha'I, bali pia, kwa kufuatana na maelekezo ya Wasia wa Abdu'l-Baha aliteua Mikono wa Hoja ya Mungu na akaanza kuanzisha mfululizo wa asasi zilizojumuisha "waumini mashuhuri na waliojifunga walioteuliwa kwa makusudi mahsusi ya kulinda na kueneza Imani ya Baha'u'llah chini ya Mkuu wa Imani",8 umuhimu mkubwa ambao sasa unaweza kuonekana wazi katika utendaji wa Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, Bodi za Washauri wa Bara, Washauri wasaidizi na wasaidizi wao.

70.12 Kutoka maeneo fulani kwa miongo kadhaa, kumekuwa na majaribio ya mara kwa mara kuingiza kwenye Utawala wa Kibahà'í dhana kwamba inafaa na ni vizuri kuleta mabadiliko katika jumuiya kwa kuanzisha jimbo la uchaguzi la waumini wenye fikra sawa ili kuweka shinikizo kwa mabaraza yaliyochaguliwa. Dhana kama hiyo inafanana sana na kuanzisha vyama na makundi ambayo yanakubalika na ni tabia iliyozoeleka katika demokrasia nyingi za uwakilishi. Hata hivyo, hii ni kinyume kabisa na Utaratibu wa kiroho wa Utawala wa Kibaha'i na ingeweza kupotosha asili yake na kudhoofisha umoja ambao Agano limeundwa kuuhifadhi.

70.13 Asasi za kuchaguliwa, hasa zina wajibu wa "kujifahamisha zenyewe na hali inayoendelea katika jumuiya" na "lazima wapime bila jazba katika fikra zao umuhimu wa kila jambo linaloletwa mbele yao kushughulikiwa", lakini mchakato huu hausaidiwi na kuenea kwa ukosoaji hasi na mifarakano baina ya marafiki.
*(Kutoka barua ya 16 Februari, 1996 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

71.1 Umeonesha wasiwasi kwamba majaribio yanayofanywa kutambulisha tofauti kati ya “Wabaha’i maamuma” na “Wabaha’i wasomi” kwa kuzingatia ujifunzaji wa Imani ni tabia inayosababisha roho ya utengano miongoni mwa marafiki. Hofu yako imethibitishwa kikamilifu. Uendeaji kama huo katika ujifunzaji wa Hoja ungeusaliti msingi wa kutotofautiana wa mwenendo wa jumuiya ya Kibahà’í kama inavyoainishwa katika Mafundisho ya Imani.

71.2 Kama ujuavyo, Bahá’u’lláh husema kwamba utafutaji wa elimu umeamriwa kwa kila mmoja, na elimu yenyewe inaelezwa Naye kama “mabawa ya maisha ya mwanadamu” na “ngazi ya kupaa kwake”. Wale ambao wamefikia viwango vya juu katika suala hili kufanya iwezekane kwa wao kuchangia katika njia muhimu kwenye uendelezaji wa ustaarabu wanastahili kutambuliwa na kupongezwa na jamii.

71.3 Katika ujifunzaji wa Ufunuo wa Mungu, ujuzi wa mtu binafsi katika mojawapo ya sayansi ya maumbile au ya jamii, katika sheria, taaluma ya kukua kwa lugha au nyanja zingine za ubobeaji mara nyingi utatoa mwanga wa thamani kwenye masuala yachunguzwayo, na michango kama hiyo itathaminiwa kwa kiasi kikubwa. Uwanja wa masomo wa Mashariki ya Karibu, uliotajwa katika barua yako, ni mmojwapoa unaoweza kusaidia kwa njia hii. Hata hivyo, hakuna hata eneo moja la ubobezi miongoni mwa matawi mengi ya utafiti wa kisomi linaloweza kuwapa wataalamu wake jukumu la kimamlaka katika jitihada ya kawaida ya kuchunguza athari kubwa za kuyumba na shirika la ukweli likumbatiayo vyote.

71.4 Sambamba na miito Yake ya utafutaji wa elimu, Bahá’u’lláh amekataza kabisa ile sura ya dini zote zilizopita ambayo kipengele maalumu cha watu kama vile wachungaji wa Kikristo na ‘maulama’ wa Kiislamu walipotokea kutumia mamlaka juu ya ufahamu wa kidini na matendo ya waumini wenzao. Katika barua iliyoandikwa kwa Kiajemi kwa niaba yake kwenda kwa Baraza la Kiroho la Wabahà’í wa Istanbul, Mlinzi yu katika maumivu kiasi kusisitiza umuhimu wa uondokanaji na historia hii ya dini za kizamani:

Lakini sifa ziwe kwa Mungu kwamba Kalamu ya Utukufu amefanya kinyume na mawazo yasiyobadilika na ya kimabavu ya wasomi na wenye hekima, ametupilia mbali hoja za watu binafsi kama kigezo cha kimamlaka, hata kama walitambuliwa kama waliokamilika na wasomi miongoni mwa watu, na kuamuru kwamba masuala yote yarejelewe kwenye vituo vyenye mamlaka na mabaraza yanayoainishwa.

71.5 Kipindi cha Kibaha'i kinaelezewa katika maneno ya Muasisii wake kama "mchana ambao hautafuatiwa na usiku". Kupitia Agano Lake, Bahá'u'lláh ametoa chanzo kisichoshindwa cha muongozo mtakatifu ambacho kitadumu wakati wote wa Kipindi. Mamlaka ya kusimamia masuala ya kijamii na kuhakikisha vyote viliwi; uadilifu wa Neno la Mungu na utangazaji wa ujumbe wa Imani imepewa Utaratibu wa Utawala ambao umezaliwa kutokana na Agano. Ni kwa kupitia tu mchakato wa uchaguzi huru au uteuzi usiotafutwa kwamba wajumbe wa asasi za Utaratibu huu wanapewa nyazifa zao ndani yake. Hakuna taaluma ama katika ufundishaji wa Imani au utawala wake ambayo kwayo mtu anaweza kufunzwa au ambayo kwayo muumini anaweza kuigombea kwa usahihi. Maneno ya tahadhari ya Bahá'u'lláh hususani yanahusika:

Tangu utafutaji wa upendeleo na upekee vilipoanza kutumika, ulimwengu umeharibiwa. Umekuwa mkiwa….

Hakika mwanadamu yu bora, kwa vile kila mmoja ni hazina ya ishara ya Mungu. Hata hivyo, kujichukulia binafsi kama bora zaidi katika maarifa, ujuzi, au njema, au kujikuza binafsi, au kutafuta upendeleo, ni ukiukaji mkubwa sana.

71.6 Uendelezaji wa ujifunzaji wa kila aina miongoni mwa waumini wa Imani ni shughuli ya msingi kwa ajili ya utimizaji wa malengo mengi ya jumuiya. Kwa sababu hiyo, utiwaji moyo wa waumini binafsi kujipatia maarifa, uendeshaji shule za Kibahà'í, vyuo vikuu na asasi za mafunzo, uandaaji wa vikundi vya mafunzo na kazi ya vikosi kazi vilivyojifunga kuhusisha kanuni za Ufunuo kwa changamoto zinazowakabili wanadamu

vyote huwakilisha shughuli ambazo kwazo wote wawili; Washauri na wasaidizi wao, kwa upande mmoja, na Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na ya Mahali, kwa upande mwingine, lazima yajishughulishe nao. Katika kubeba majukumu haya yenye kudai, asasi za Kibaha'i, kila mahali hujikuta juhudi zao zinakuzwa kwa kiwango kikubwa kwa usaidizi wa waumini ambao utafutaji wao wa maarifa, ubora wa tabia na kujitoa kwao kwa Hoja huwafanya wafae kuchangia huduma yao.

71.7 Jukumu maalum katika jambo hili limewekwa kwa Washauri kwa sababu ya wajibu waliopewa wa kumsaidia muumini binafsi kuonesha uwezo wake. Wajumbe wa asasi hii, wanaoteuliwa kwa vipindi maalum wamepewa jukumu la kuendeleza katika siku zijazo kazi ya ulinzi na uenezi wa Imani iliyopewa katika Wasia na Agano la Abdu'l-Baha kwa Mikono wa Hoja. Hivyo, Washauri wanaitwa 'kutawanya Manukato Matakatifu', kuinua mioyo ya watu, kukuza ujifunzaji, kuendeleza tabia za watu wote, kuwa wakati wote na katika hali zote, waliotakasika na kujitenga na vitu vya kidunia." Kama ilivyo kwa Mikono, Washauri hawana mamlaka ya kufasiri, mamlaka yaliyowekwa na Agano kwa Abdu'l-Baha na Mlinzi wa Imani tu. Wakati baadhi ya Washauri, kama ilivyo kwa baadhi ya Mikono, wanaweza kuwa waliosomea taaluma au utaalamu mbalimbali katika kazi zao binafsi, utekelezaji wa majukumu yao hautegemei ujuzi wa aina hii. Wote hushiriki kikamilifu katika wajibu huu muhimu wa kuwatia moyo waumini kila mahali katika upataji wa elimu, katika ukubwa wake wote. Wote hushiriki, vile vile, katika jukumu ililopewa asasi yao ambayo wao ni wajumbe wa kulinda Imani dhidi ya maadui zake, wote wawili wa nje na wa ndani, jambo ambalo wote wawili; Bwana na Mlinzi walilipa umuhimu adhimu.

71.8 Uelewa wa kanuni tuzitumiazo kuchunguza Ufunuo wa Baha'u'llah hutegemea pia utambuzi wa asili ya ukubwa wa mamlaka yaliyotolewa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Likiongelea juu ya majukumu ya wajumbe wake waliochaguliwa: Wasia na Agano hutamka:

Inawabidi wajumbe hawa (wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu) kukusanyika eneo fulani na kushughulikia matatizo yote yanayoleta

tofauti, maswali ambayo yenye utata na mambo ambayo hayajaandikwa wazi wazi katika Kitabu. Chochote watakachoamua kina nguvu sawa sawa na Andiko lenyewe.

71.9 Akisisitiza katika Hati hiyo ya Utaratibu wa Utawala, umuhimu wa waumini kushikilia kwa moyo wote kwenye muongozo uliotolewa na wote wawili; Mlinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, Abdu'l-Baha husema: Chochote wanachoamua ni cha Mungu. Yeyote asiyemtii yeye wala wao hajamtii Mungu; yeyote anayemuasi yeye na dhidi yao amemuasi Mungu; yeyote anayempinga yeye amempinga Mungu; yeyote anayeshindana nao ameshindana na Mungu….
*(Kutoka barua ya 14 Machi, 1996 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

72.1 Ni Eneo pekee la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu "kutamka na kutoa uamuzi wa mwisho juu ya sheria na amri ambazo Baha'u'llah hakuzifunua wazi wazi." Inachukua jukumu la kutumia Neno lililofunuliwa, ulinzi wa Imani na vile vile jukumu la "kuhakikisha muendelezo wa yale mamlaka yaliyoteuliwa kitakatifu ambayo hutiririka kutoka Chanzo cha Imani yetu, kulinda umoja wa wafuasi wake na kutunza uadilifu na unyumbulikaji wa Mafundisho yake".

Hata hivyo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu sio mjua yote na marafiki wanapaswa kuelewa kuwa kuna tofauti kati ya kutokosea na kuwa mjuzi wa yote. Kama ilivyo kwa Mlinzi, Nyumba ya Haki inahitaji kupata taarifa zote wanapotakiwa kutoa uamuzi na kama yeye inaweza kubadilisha uamuzi wake wakati ukweli mpya huibuka au kulingana na mabadiliko ya uhalisia katika siku za mbele. Hatukupata popote katika maandishi ya Shoghi Effendi ambayo huonesha kuwa Nyumba ya Haki itafanya 'maamuzi yenye makosa'.
*(Kutoka barua ya 14 Juni, 1996 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

73.1 Asasi za Utaratibu wa Utawala wa Baha'u'llah zikijikita katika vifungu vya Ufunuo Wake, zimeibuka pole pole na hatua kwa hatua,

kama ambavyo jamii ya Kibaha'i ilivyokua kupitia nguvu na msukumo uliotolewa kwa binadamu katika zama hizi. Sifa na utendaji wa kila moja ya asasi hizi umekua, na unaendelea kukua, kama ambavyo imekuwa kwa uhusiano baina yao. Maandiko ya Mpendwa Mlinzi hufafanua mambo ya kimsingi ya mfumo huu wenye nguvu na kuweka wazi Utaratibu huu wa Kiutawala, ingawa kwa namna nyingi ni tofauti kutoka Utaratibu wa Ulimwengu ambao ni hatima ya muda mrefu ya Ufunuo wa Kibaha'i kuleta katika uhai kwa vyote viwili; "kiini" na "muundo" wa Utaratibu wa Ulimwengu.

Hivyo, mabadiliko ya asasi za Utaratibu wa Kiutawala, wakati zikifuata taratibu nyingi ili kukidhi hali zibadilikazo katika nyakati na mahali tofauti, zinapaswa zifuate kikamilifu kanuni muhimu za Utawala wa Kibaha'i ambazo zimewekwa katika Maandiko Matakatifu na fasiri zilizotolewa na Abdu'l-Baha na Mlinzi.
*(Kutoka Ujumbe wa 30 Mei, 1997 uliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa).*

74.1. Tayari katika "Kipindi cha Baha'u'llah" Shoghi Effendi ameonesha, pasipo shaka yoyote, kwamba kazi ya kufanya fasiri za kimamlaka za Mafundisho imewekwa pekee na kwa Mlinzi tu. Si Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wala asasi nyingine yoyote, mtu au kikundi cha watu kinaweza kujichukulia kazi hiyo. Kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haitaweza kuingilia kazi zilizotengwa maalum kwa ajili ya Mlinzi inaoneshwa si tu kwa maneno na matendo yake yenyewe, bali na kauli za Shoghi Effendi katika waraka huo huo: "Haiwezi, na wala kamwe haitaweza, kuingilia milki takatifu iliyoagizwa ya mwingine." Inathibtishwa na ukweli kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na vile vile Mlinzi wote wawili wapo "chini ya uangalizi na ulinzi wa Uzuri wa Abha, chini ya kinga na muongozo usiokosea wa Mtukufu, Aliyetukuka."
*(Kutoka barua ya 3, Juni 1997 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

75.1. Maana za istilahi “ufafanuzi” na “fasiri” kama inavyotumika kuhusiana na utendaji wa asasi za Kibahà’í, kwa kweli hazipaswi kukanganywa moja kwa nyingine. Ufafanuzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutokana na kazi yake ya utungaji sheria, na kwa hivyo hutofautiana na fasiri. Utungaji sheria wenye uvuvio mtakatifu wa Nyumba ya Haki haujaribu kusema nini Neno lililofunuliwa humaanisha--inaeleza kile ambacho lazima kifanyike pale ambapo Maandiko yaliyofunuliwa au fasiri yake yenye mamlaka haiko wazi; na katika muktadha huu inatoa maelezo. Kwa hiyo, ni kwenye kiwango tofauti kabisa kutoka Maandiko Matakatifu, na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imepewa uwezo kufuta au kurekebisha sheria zake yenyewe wakati wowote inapoona infanya hili kuhitajika. Tofauti kubwa baina ya kazi mbili za ufafanuzi na fasiri, kurudia hoja hiyo kwa namna tofauti, ni kwamba sheria hiyo na matokeo ya ufafanuzi wake ina uhitaji wa marekebisho ya Nyumba ya Haki yenyewe, ambapo fasiri ya Mlinzi ni tamko la ukweli usiohitaji kubadilishwa.
*(Kutoka barua ya 27 Agosti 1998 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

76.1. Tumepokea barua kutoka kwa muumini mmoja huko Iran yenye maswali kuhusu Ulinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Tunatambua kwamba uthabiti katika Agano ni miongoni mwa sifa za kipekee za waumini katika nchi hiyo, ambao wanatambua juu ya kanuni na kweli za msingi zinazohusu urithi wa mamlaka kwenye Hoja. Hata hivyo, asiwepo yeyote miongoni mwao atakayesita kuomba ufafanuzi wa masuala ambayo wana maswali nayo, kwa kuwa maadui wa Imani hawajachoka katika majaribio yao ya kupanda mbegu za mkanganyiko na shaka. Zaidi ya hapo, kuna manufaa, kwa kuzingatia nasaha za Mpendwa Bwana wetu kwetu sote kuwa na tahadhari kila wakati kuhusiana na masuala ya ulinzi, kwa ajili ya marafiki kupitia mambo muhimu mara kwa mara. Kwa hivyo, tumeamua kukupa maoni yafuatayo….

76.2. Maswali yanayohusiana na ulinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu yanaweza kutatuliwa kupitia usomaji makini wa maandiko ya Baha’u’llah, Abdul’l-Baha na Shoghi Effendi na fafanuzi zilizofanywa na Nyumba

ya Haki ya Ulimwengu, ambayo, Abdu'l-Baha husema, "watajadili juu ya matatizo yote ambayo yamesababisha tofauti, maswali ambayo yana utata na mambo ambayo hayajaandikwa wazi wazi katika Kitabu. Chochote wanachoamua, "Anawahakikishia marafiki, "kina athari sawa na Maandiko yenyewe."

76.3 Kabla ya kufariki kwa Abdu'l-Baha mnamo 1921, maelezo aliyokuwa ameyatoa katika Wasia na Agano Lake ili kulinda Imani na kuhakikisha maendeleo yake thabiti katika siku zijazo kwa ujumla hayakujulikani. Waumini walitazamia siku ambayo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ingesimikwa kwa kuwa ilikuwa imetajwa mahsusi katika Maandiko Matakatifu. Hata hivyo, hapakuwepo na uelewa wa hakika kwamba pangekuwepo na Mlinzi. Kwa kweli, Shoghi Effendi baabaye aliashiria kwamba hakufahamu mapema juu ya nafasi ambayo angeitwa. Zaidi, ilielezewa kuwa alidhani Wasia na Agano lingempa jukumu, kama mjukuu mkubwa wa kiume wa Abdu'l-Baha, jukumu la kuandaa uchaguzi wa Nyumba ya Haki. Ni baada tu ya usomaji wa Wasia ndipo asasi ya Ulinzi ilipotokea kujulikana kwa mapana, na jumuiya ya Kibaha'i kote ulimwenguni ilipomtambua Shoghi Effendi kama Mkuu wa Imani ambaye kwake wote lazima wageukie.

76.4 Usomaji wa makini wa Wasia wa Abdu'l-Baha huweka wazi kuwa Yeye hakuashiria kwamba kulikuwa na matokeo yaliyokwishaamuliwa kabla bali aliagiza kwa ajili ya hali tofauti tofauti ambazo kwa kutegemea mazingira ya baadaye, zingeweza hatimaye kuikabili Imani. Sehemu ya pili ya Wasia, mathalani, ambayo huirejelea Nyumba ya Haki ya Ulimwengu tu, bila kutaja juu ya Ulinzi, iliandikwa wakati ambapo maisha Yake yenyewe yalipokuwa katika hatari kubwa na Shoghi Effendi alikuwa kijana mdogo tu. Katika kipindi hicho hicho, Abdu'l-Baha alikuwa amefanya maandalizi ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kufanyika haraka, ikiwa tishio juu ya maisha Yake lingefanikiwa. Kupitia Rehema za Mungu, hali ya hatari ilipita, na hatimaye aliachiwa Shoghi Effendi miaka mingi baadaye, kama Mlinzi na Mkuu wa Imani, kuamua ni wakati gani wa kuundwa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Mapema alifikiria uwezekano wa

kufanya uchaguzi mara tu baada ya kufariki kwa Abdu,l-Baha, kwa hali hiyo Nyumba ya Haki na Mlinzi wangefanya kazi sambamba. Bila shaka, aliamua kwamba misingi ya Utaratibu wa Kiutawala kwanza ilihitaji iwe imewekwa thabiti kuanzia ngazi za mahali hadi kitaifa, na hatimaye ilijulikana kwamba Nyumba ya Haki ingeanzishwa miaka kadhaa baada ya kifo chake mwenyewe. Kwamba kipindi cha mpito kutoka utumishi wa Mlinzi hadi uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kutokea kwa urahisi namna ile, kwenyewe kwaweza kuhusishwa na jinsi maelekezo fulani yalivyoandaliwa katika Wasia.

76.5 Wasia na Agano la `Abdu'l-Bahá huruhusu wazi wazi uwezekano wa mrithi wa Shoghi Effendi, na kwa muktadha huu, tunakuta matamshi yaliyoandikwa naye au kwa niaba yake katika kipindi cha miaka thelathini na sita ya utumishi wake yanayoashiria Walinzi wa wakati ujao. Walakini, hakuna hakikisho katika Maandiko kwamba mfululizo wa Walinzi ungeendelea katika Kipindi chote; badala yake, uwezekano umefikiriwa kuwa mfululizo huo ungefika mwisho. Kuhusu suala hili, Bahá'u'lláh husema katika Kitáb-i-Aqdas:

> Mali zilizowekwa wakfu kwa hisani zinarejea kwa Mungu, Mfunuaji wa Ishara. Hakuna aliye na haki ya kuzitoa bila ruhusa kutoka kwa Yeye Ambaye ni mahali pa mambazukio ya Ufunuo. Baada Yake, mamlaka haya yanaenda kwa Aghsan, na baada yao kwa Nyumba ya Haki—iwapo itakuwa imesimikwa katika ulimwengu kwa wakati huo—ili kwamba waweze kutumia mali wakfu hizi kwa manufaa ya zile Sehemu ambazo zimekwisha tukuzwa ndani ya Hoja hii, na kwa ajili ya chochote ambacho kimeagizwa kwao na Yeye Ambaye ndiye Mungu wa uweza na nguvu. Vinginevyo, mali wakfu hizo zitarejeshwa kwa watu wa Bahá ambao huwa hawasemi ila kwa idhini Yake na wala hawahukumu ila kufuatana na kile ambacho Mungu ameamuru ndani ya Waraka huu—lo, wao ni mashujaa wa ushindi katikati ya mbingu na dunia—ili waweze kuzitumia kwa namna ambayo imewekwa ndani ya Kitabu na Mungu, Muweza, Mkarimu.

Kifo cha Shoghi Effendi kiliharakisha hali iliyoelezwa, ambamo mamlaka iliyowekwa kwa Aghsan – kwanza kwa `Abdu'l-Bahá na kisha kwa Shoghi Effendi -- iliishia kabla ya Nyumba ya Haki kusimikwa.

76.6 Katika Wasia na Agano Lake, `Abdu'l-Bahá huyafafanua kwa maneno ya wazi wazi kabisa masharti ambayo kwa mujibu wake Shoghi Effendi alingemtaja mrithi wake kuwa Mlinzi:

> Enyi wapendwa wa Bwana! Inampasa Mlinzi wa Hoja ya Mungu kuteua katika kipindi cha uhai wake yeye ambaye atakuwa mrithi wake, kwamba tofauti zisiweze kuibuka baada ya kufariki kwake. Yule ambaye atateuliwa lazima adhihirishe ndani mwake mwenyewe kujitenga kutokana na vitu vyote vya kidunia, lazima awe asili ya usafi, lazima aoneshe ndani mwake kicho cha Mungu, maarifa, hekima na ujifunzaji. Hivyo, ikiwa mtoto wa kwanza wa Mlinzi wa Hoja ya Mungu asipodhihirisha ndani mwake ukweli wa maneno:—"Mtoto ni siri ya asili ya baba yake," yaani, asiporithi hali ya kiroho iliyomo ndani yake (Mlinzi wa Hoja ya Mungu) na uzao wake mtakatifu usipoendana na tabia nyoofu, hapo ni lazima yeye, (Mlinzi wa Hoja ya Mungu) achague tawi lingine kumrithi yeye.
>
> Mikono wa Hoja ya Mungu lazima wachague kutoka miongoni mwao watu tisa ambao kwa wakati wote watajishughulisha katika huduma muhimu kwenye kazi ya Mlinzi wa Hoja ya Mungu. Uchaguzi wa watu hawa tisa lazima ufanyike ama kwa kauli ya pamoja au kwa kura ya wengi, kutoka kwenye kundi la Mikono wa Hoja ya Mungu na hawa, iwe kwa kauli ya pamoja au kwa wingi wa kura, lazima watoe idhini yao kwa chaguo la Yule ambaye Mlinzi wa Hoja ya Mungu amemchagua kama mrithi wake. Idhini hii lazima itolewe kwa busara ambayo sauti za wanaokubali na wasiokubali zisiweze kutofautishwa (yaani, kura ya siri).

76.7 Maoni binafsi ya mtu yeyote kuhusiana na tamko la hapo juu, hata awe msomi namna gani, hayawezi kulinganishwa na uelewa usio na kosa

wa Mlinzi juu ya kifungu hicho. Shoghi Effendi, ambaye alifuata kwa uaminifu matakwa ya Bahá'u'lláh na `Abdu'l-Bahá katika utumishi wake wote, asingeweza kamwe kuwa mzembe katika jambo lililo muhimu kwa uadilifu wa Imani kama suala la uteuzi wa mrithi wake. Haifikiriki kwamba angemteua mtu wa kumrithi ambaye hakuwa na sifa zilizoandikwa na `Abdu'l-Bahá katika Wasia Wake. Kadhalika, isingetetewa kwamba angefanya hivyo kwa namna ambavyo inakiuka mahitaji dhahiri yaliyomo katika waraka huo huo, ambayo hujumuisha idhini ya chaguo lake na wale Mikono tisa wa Hoja ya Mungu walioteuliwa, ili kwamba "tofauti" "zisingeibuka baada ya kifo chake." Ni uotofu kiasi gani pendekezo la wavunja Agano kwamba Shoghi Effendi angepuuza maagizo ya Bwana na kufanya uteuzi wa kificho na usio wa moja kwa moja wa mrithi wake! Bali, ukweli kwamba Shoghi Effendi hakuteua mrithi ichukuliwe kwamba ni ishara ya uaminifu wake kushikilia kikamilifu kila neno lililomo katika `Abdu'l-Bahá na hitimisho la kwamba hapakukuwepo na yeyote mwenye sifa zilizostahili ambaye yeye angeweza kumteua.

76.8 Kwa hiyo, inapaswa ieleweke wazi kwa kila mfuasi thabiti wa Bahá'u'lláh kwamba mwisho wa mfululizo wa Walinzi haikuwa matokeo ya uamuzi au hatua yoyote iliyochukuliwa na Mikono wa Hoja ya Mungu kufuatia kifo cha ghafla cha Shoghi Effendi. Mfuatano ulifikishwa mwishoni, wakati uliposhurutishwa na hali zilizokuwepo na masharti makali ya Wasia, Shoghi Effendi hakumtaja mirth. Kufikiria uwezekano kwamba siku moja uweze kuanzishwa tena hakuna maana. `Abdu'l-Bahá aliandika kwamba "kabla ya kumalizika kwa miaka elfu moja, hakuna mtu mwenye haki kusema neno lolote, hata kudai daraja la Ulinzi." Na katika kifungu hicho hicho Yeye huwaasa marafiki, "endapo pakiwepo na tofauti za maoni, Nyumba Kuu Kabisa ya Haki mara moja ingetatua matatizo hayo." Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, mara tu baada ya kuundwa kwake, ilieleza kwamba "inaoni kuwa hakuna njia ya kuteua au kutunga sheria kwa ajili ya kupata uwezekano wa kuteua Mlinzi wa pili kumrithi Shoghi Effendi."

76.9 Wakati mfuatano wa Walinzi umekoma, Agano limelindwa. Kiasi kikubwa cha fasiri za Shoghi Effendi hutambulisha maamuzi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kadiri Imani inavyoendelea kusonga mbele. Umoja wa Imani umelindwa, na utambuzi wa kusudi kuu la Bahá'u'lláh kwa wanadamu limehakikishwa. Mkono wa Mwenye Nguvu Zote umesimika Ufunuo Wake juu ya msingi usioshambulika, unaodumu," Bahá'u'lláh amesema. Tufani za ugomvi wa wanadamu hazina nguvu kudhoofisha msingi wake, wala nadharia dhanifu za watu kufanikiwa katika kuuharibu muundo wake."

***

76.10 Kwa kurejelea kwenye maswali mahsusi yaliyoulizwa katika barua tumepokea, moja inahusiana na maana ya jina "Aghsán", kama linavvopatikana katika Maandiko. Wakati katika badhi ya mambo, kama inavyothibitishwa na Mlinzi, jina hili linatumika hususani kwa wana wa kiume wa Bahá'u'lláh, nyakati zingine linatumika kwa mapana zaidi kujumuisha wazao Wake wa kiume. Kwa mfano, katika Wasia na Agano Lake `Abdu'l-Bahá anamrejelea Shoghi Effendi kama "tawi teule". Rejeleo kwa Shoghi Effendi kama Ghusn hapa–kielelezo cha umoja kwa neno Aghsán–hufuata matumizi ya Bahá'u'lláh kuhusiana na majina aliyowapa wanae, yaani, Tawi Kuu Kabisa, Tawi Kuu Zaidi na Tawi Safi Kabisa. Barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi inaeleza kwamba neno Aghsán "hurejelea wazao wa Bahá'u'lláh"; nyingine humuelezea Hussein Rabbani, ndugu yake Mlinzi, kama "mjukuu wa Bwana, Afnán na Aghsán waliotajwa katika Wasia na Agano la Bwana." Ni wazi, hivyo, kwamba jina Aghsán au Ghusn, hujumuisha Shoghi Effendi na wazao wengine wa kiume wa Bahá'u'lláh.

76.11 Ikiwa, wakati wowote, wazao wa kiume wa Bahá'u'lláh watajitokeza ambao ni waaminifu kwa Agano, hata hivyo isingewezekana kwao kuchukua ofisi ya Mlinzi, kwani, kama ilivyokwishaelezwa, Shoghi Effendi kutofanya uteuzi, hawawezi kudai daraja la Ulinzi na hakuna njia kwa mtu kuteuliwa kupitia sheria ya Nyumba ya Haki.

***

76.12 Hoja nyingine inahusu usimikwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Mahsusi, swali limeulizwa ikiwa utendaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Kibahá'í iliyoko katika Nchi Takatifu "inayotambulika rasmi", iliyotajwa na Shoghi Effendi, ilikuwa hatua ya mwanzoni ya kimsingi katika mabadiliko ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

76.13 Kama ujuavyo bila shaka, Shoghi Effendi alieleza kwamba "`Abdu'l-Bahá Mwenyewe katika moja ya Nyaraka Zake za mwanzoni kabisa, alitafakari uwezekano wa uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wakati wa uhai Wake." Bwana alifafanua masharti ya lazima kwa ajili ya uundwaji wake, ambayo hayakujumuisha uanzishwaji wa mahakama ya kidini:

Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki inapaswa kuchaguliwa kwa mujibu wa mfumo unaofuatwa katika uchaguzi wa mabunge ya Ulaya. Na wakati nchi zingeongozwa Nyumba za Haki za nchi mbali mbali zingechagua Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki.

Wakati wowote wapendwa wote wa Mungu katika kila nchi wateuapo wawakilishi wao, na hawa kwa upande wao huchagua wawakilishi wao, na wawakilishi hawa huchagua shirika, shirika hilo litachukuliwa kama Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki. Uanzishwaji wa Nyumba hiyo hautegemei juu ya ubadilishwaji wa mataifa yote ya ulimwengu kuwa katika Imani moja. Kwa mfano, kama hali zikiruhusu na hakutakuwa na usumbufu utakaosababishwa, marafiki huko Uajemi watachagua wawakilishi wao, na vivyo hivyo marafiki huko America, India na maeneo mengine pia watachagua wawakilishi wao na hawa wachaguwe Nyumba ya Haki. Nyumba hiyo ya Haki itakuwa ndiyo Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki. Ndiyo ilivyo.

76.14 Wakati wa miaka thelathini na sita ya utumishi wake, alipoongoza ulimwengu wa Kibahá'í, akijitahidi kuweka misingi ya Utaratibu wa Utawala, Shoghi Effendi alieleza hatua mahsusi za kimaendeleo za

kuchukuliwa, ambazo zilikusudiwa kuongoza hadi kufikia kwenye usimikwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Utimizwaji wa baadhi yao ulitegemea kwa kiasi kikubwa juu ya juhudi za waumini wenywe–ongezeko la idadi ya Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na ya Kitaifa, uteuzi wa Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa na ukuaji wake kuwa shirika la kuchaguliwa. Nyinginezo, walakini, zilitegemea nguvu zifanyazo kazi katika jamii, na hata jitihada za namna gani zilizofanywa na jamii ya Kibbahá'í, hazikuweza kutimizwa.

76.15 Mnamo 1929, mathalani, Mlinzi alisema, "Kama hali nzuri zingeruhusu, ambapo Wabahá'í wa Uajemi na wa nchi jirani zilizokuwa chini ya utawala wa Kisovieti, wangewezeshwa kuchagua wawakilishi wao wa kitaifa…kikwazo pekee ambacho kingebakia katika uundwaji wa hakika wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa kingekuwa kimeondolewa." Baadaye, baada ya kufukuzwa kwa Wabahá'í kutoka Urusi na wenye mamlaka, barua iliyoandikwa kwa niaba yake ilieleza, "Wakati alipoirejelea Urusi kulikuwepo na Wabahá'í kule, sasa jumuiya imekoma kiutendaji haipo tena; hivyo, uundaji wa Nyumba ya Kimataifa ya Haki hauwezi kutegemea Baraza la Kiroho la Kitaifa la Urusi.

76.16 Kwa namna hiyo hiyo, malengo yaliainishwa na Shoghi Effendi kwa ajili ya uanzishwaji wa Mahakama ya Kibahá'í, pamoja na mahakama ya kitaifa katika nchi kadhaa ndani ya Asia, na kama hatua katika maendeleo ya Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa, kiashiria cha mwanzoni cha Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, Mahakama katika Nchi Takatifu. Kutambuliwa kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa na serikali ya Misri kama mahakama huru ya Kibahá'í kulitafutwa tangu huko nyuma mnamo 1929. Baada ya muda, mabadiliko ya mambo yalifanya uundwaji wa mahakama za kidini kama hizo kushindikana. Kama Mikono wa Hoja ya Mungu walivyotamka mnamo 1959 wakiitisha uchaguzi wa Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa na hatimaye usimikwaji wa Nyumba ya Haki. Tunapenda kuwahakikishia waumini kwamba kila juhudi itafanyika kusimika Mahakama ya Kibahá'í katika Nchi Takatifu kabla ya tarehe

iliyowekwa kwa ajili ya uchaguzi huu. Hatuna budi, walakini, kuzingatia kwamba Mlinzi mwenyewe aliashiria wazi lengo hili, kutokana na muelekeo wa nguvu kuelekea uwekwaji wa Mahakama za Kidini katika sehemu hizi za ulimwengu, isingewezekana kufanikishwa.

***

76.17 Bado swali lingine lililoulizwa linahusu utekelezaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wa kazi fulani zilizofanywa na Mlinzi hapo awali. Kuhusiana na Huqúqu'lláh, `Abdu'l-Bahá ameeleza kwamba "Utumiaji wa Huqúq, wote au kwa sehemu, unaruhusiwa, lakini hili sharti lifanyike kwa idhini ya mamlaka katika Hoja ambayo kwake lazima wote waigeukie." Vivyo hivyo, kufukuzwa kwa wavunja-Agano ni wajibu unaotekelezwa na Mkuu wa Imani katika muktadha wa wajibu wa kuilinda Hoja kutoka wale wanaotafuta kudhoofisha umoja wake. Shoghi Effendi, inafahamika vyema, alilazimika kuwafukuza wavunja-Agano kutoka katika Imani kwa nyakati mbali mbali za kipindi chote cha utumishi wake, kabla na baada ya uteuzi wa Mikono wa Hoja ya Mungu. Jukumu hili sasa huangukia kwenye mikono ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kama kitovu cha mamlaka ambacho wote lazima wakigeukie. Taratibu zinazofuatwa sasa kuhusiana na suala hili zimeelezewa katika tamko "Asasi ya Washauri".

76.18 Katika suala hili inapaswa ikumbukwe kwamba baada ya kufariki kwa Shoghi Effendi, ingawa ulimwengu wa Kibaháí uligubikwa na huzuni, ulidumisha umoja wake katika kipindi tete kati ya kipindi cha utumishi wake na uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Changamoto pekee kwa uadilifu wake ilitokea mnamo miaka miwili baada ya kifo chake wakati Charles Mason Remey, ambaye wakati huo alikuwa mmoja wa Mikono wa Hoja, alipodai kuwa Mlinzi. Kama mjuavyo, Remey alisisitiza kuwa uteuzi wake mwaka 1951 kama rais wa Halmashauri changa ya Kibahá'í ya Kimataifa ulimaanisha kwamba moja kwa moja anapaswa kuchukua nafasi ya mkuu wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na, hivyo, awe Mlinzi wa pili.

76.19 Upuuzi wa dai la Remey ni dhahiri na linahitaji ufafanuzi mdogo tu. Mnamo 1957, alikuwa miongoni mwa Mikono wa Hoja waliokusanyika katika Nchi Takatifu kujadili hatua gani kuchukua kufuatia kifo ambacho hakikutarajiwa cha Mlinzi. Yeye binafsi alikiri kwamba Shoghi Effendi hakuteua mrithi, akiweka sahihi hati ya kauli ya pamoja iliyotolewa na Mikono kwa suala hili. Kama mtia sahihi wa hati nyingine kama hiyo, alikubali kwamba shirika zima la Mikono wa Hoja lingeamua lini na jinsi gani mabadiliko ya Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa yangeishia kwenye uchaguzi wa Nyumba ya Haki. Kwa miaka miwili, kama mmoja wa Mikono tisa walioteuliwa kutumikia katika Nchi Takatifu, alishiriki katika ushauriano ambao uliongoza maendeleo ya jumuiya ya Kibahá'í. Kisha, bila taarifa au majadiliano na Mikono wenzake, alidai daraja la Ulinzi, pasipo uteuzi dhahiri wa Shoghi Efendi kama ilivyoainishwa katika Wasia na Agano na katika ukiukaji wa moja kwa moja wa agizo la `Abdu'l-Bahá kwamba hakuna yeyote awezaye kudai hivyo. Wakitumia mamlaka waliyopewa kwa mujibu wa Wasia wa `Abdu'l-Bahá, Mikono wa Hoja walimfukuza kutoka kwenye Imani kama mvunja-Agano.

***

76.20 Katika masuala yanayohusu Agano, marafiki lazima wawe imara na thabiti; wanapaswa wawe waangalifu, isije hoja zinazotolewa na wale wapandao mbegu za shaka ziwe chanzo cha mkanganyiko au kusababisha mabishano na mfarakano. Endapo maswali yakiibuka ambayo hayawezi kusuluhishwa, lazima mara moja yawasilishwe mbele ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Marafiki wanapaswa hasa wawe waangalifu kuepuka kushawishiwa na minong'ono ya mabaki ya wavunja-Agano na wafuasi wao, ambao wanatafuta kutikisa imani ya waumini. Ambapo zamani wakiukaji wa Agano walitafuta kudhoofisha mamlaka ya Bahá'u'lláh, `Abdu'l-Bahá na Shoghi Effendi, leo wanaipinga Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Jambo la wasiwasi hasa ni wale ambao, kama aonyavyo `Abdu'l-Bahá, "husisitiza uthabiti na uimara wao katika Agano lakini wanapokuta na masikio pokevu kisi-risiri hupandikiza mbegu za wasi wasi."

76.21 Kikundi kidogo cha washirika wa Remey, kikifadhaishwa kwa nusu karne ya ugomvi wa ndani kati ya vikundi vinavyoshindana, kimekuwa na athari ndogo sana juu ya maendeleo ya Imani. Mvumo wa upepo uliosababishwa na vitendo vyao hauna matokeo zaidi ya kutikisa vijitawi na majani machache yasivyo na uhai kutoka kwenye mti wa Hoja. Wale ambao ni wajinga, wale ambao hawaajizamisha kwa kina katika Mafundisho au siyo imara katika Agano, wale ambao hutawaliwa na ubinafsi na tamaa kwa ajili ya uongozi wanaweza kupotoshwa na kuangukia mbali. Marafiki wanahimizwa kujilinda wenyewe na jumuiya yao kwa kushikilia kwa uthabiti kwenye nasaha zenye msisitizo zilizorudiwa-rudiwa katika Maandiko Matakatifu. Kama `Abdu'l-Bahá anavyosema:

> Kwenye Kitabu Kitakatifu Kabisa kila mmoja lazima ageukie na chochote ambacho hakijaandikwa kwa uwazi humo lazima kirejelewe Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Kile ambacho shirika hili litaamua, iwe kwa sauti ya wote au kwa wingi wao, hicho kwa hakika ndiyo kweli na Kusudi la Mungu Mwenyewe. Yeyote akengeukaye, kwa hakika atakuwa miongoni mwa wapendao mfarakano, ameonesha uovu na kugeukia mbali kutoka kwa Bwana wa Agano. Kwa Nyumba hii humaanishwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo itachaguliwa kutoka nchi zote, yaani kutoka sehemu zile za Mashariki na Magharibi ambako wapendwa wanapatikana, kufuatana na namna ya uchaguzi wa kawaidia katika nchi za Magharibi kama zile za Uingereza….
>
> Na sasa, moja kati ya kanuni kuu kabisa na ya kimsingi ya Hoja ya Mungu ni kuwakana na kuepukana kabisa na wavunjaji-Agano, kwa kuwa wataiharibu kabisa Hoja ya Mungu, kuangamiza Sheria Yake na kufanya jitihada zote zilizofanywa wakati uliopita zitakuwa si kitu kabisa. Enyi marafiki! Inawapasa kukumbuka kwa upole majaribu ya Mtukufu, Yule Aliyetukuka, na kuonesha uaminifu wenu kwa Uzuri Uliobarikiwa Daima. Juhudi ya hali ya juu kabisa yapaswa ifanywe isije mabaa, majaribu na mateso

haya yote, damu hii yote safi na takatifu ambayo imemwagwa kwa wingi hivyo katika Njia ya Mungu, visijekuwa kazi bure.

Enyi wapendwa wa Bwana! Jitahidini kwa mioyo yenu yote kulinda Hoja ya Mungu kutokana na mashambulio ya wasio wanyofu, kwani roho kama hizi husababisha kilichonyoka kupind-pinda na jitihada zote za ukarimu kuzaa matokeo hasi.

76.22 Waumini kwenye Chanzo cha Imani, ambao wamevumilia zaidi ya karne moja mashambulizi ya serikali na makasisi, ambao walishinda juu ya hatari zilizosababishwa na uasi wa Azal na Muhammad-`Alí, waliojitenga wenyewe kutoka kwa wale waliompinga Shoghi Effendi, kwa urahisi watapuuza hoja danganyifu na za kijinga za wale wachache wanaochuana miongoni mwao wenyewe ili kunufaika na mkengeuko wa Remey kama kisingizio cha kuwavuta wafuasi wachache binafsi kwao. Muwe na hakika ya maombi yetu kwenye Kizingiti Kitakatifu kwa niaba ya marafiki wapendwa kila mahali katika nchi hiyo takatifu.
*(Kutoka ujumbe wa 18 Februari 2008 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Marafiki wa Iran)*

77.1 Kwa jumla, Nyumba ya Haki inapenda kuhifadhi nafasi pana iwezekanavyo kwa ajili ya marafiki kuchunguza Ufunuo wa Bahá'u'lláh na kushirikiana uelewa wao binafsi wa Mafundisho. Hata hivyo, inapaswa ikumbukwe kwamba, kuhusu mambo yaliyofasiriwa kutoka Maandiko, Bwana amesema wazi:

… mambo yaliyofasiriwa na mahitimisho ya wasomi binafsi havana mamlaka, vinginevyo kama imeidhinishwa na Nyumba ya Haki. Tofauti kwa uhakika ni hii, kwamba kutokana na mahitimisho na idhini ya shirika la Nyumba ya Haki ambayo wajumbe wake wamechaguliwa na, na wanajulikana kwa Jumuiya ya Kibahá'í kote ulimwengu, hakuna tofauti zitakazoibuka; ambapo mahitimisho ya makasisi binafsi na wasomi, kwa hakika yatasababisha tofauti, na matokeo yake yatakuwa mfarakano, mgawanyiko na msambaratiko.

Umoja wa Neno ungeharibiwa, umoja wa Imani ungetoweka na kuba ya Imani ya Mungu ingetikiswa.

77.2 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haidhamirii wakati huu kufafanua zaidi juu ya maelezo yaliyokwishatolewa kuhusu majukumu na mamlaka yake. Kwamba Nyumba ya Haki yenyewe haioni ulazima wa kufanya hivyo yapaswa kuwatahadharisha marafiki kuhusu isivyo hekima kujaribu kufafanua kwa usahihi eneo lake la kiutendaji. Hata hivyo, inapaswa itajwe kwamba, ingawa kuna vifungu dhahiri katika maandiko yenye mamlaka ambavyo vinarejelea kwenye kutofanya kosa kwa Nyumba ya Haki katika utungaji wa sheria, hoja kwamba ipo huru kutokana na kutofanya kosa katika eneo hili tu haina utetezi. Kwa hakika, matamko mengi yenye msisitizo yapatikanayo katika Maandiko, kama vile dondoo ifuatayo kutoka katika Wasia na Agano la `Abdu'l-Bahá, inapaswa itoshe kukataa madai yoyote ya aina hii:

> Tawi takatifu na chipukizi, Mlinzi wa Hoja ya Mungu pamoja na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, itakayochaguliwa na kuanzishwa na wote, zote zipo chini ya uangalizi na ulinzi wa Uzuri wa Abhá, chini ya hifadhi na ulinzi wa uhakika wa Yule Aliyetukuka (maisha yangu na yatolewa dhabihu kwa ajili yao wote). Lolote waamualo ni la Mungu. Yeyote asiyemtii yeye, wala kuwatii wao, hajamtii Mungu; yeyote anayeasi dhidi yake na dhidi yao ameasi dhidi ya Mungu; yeyote anayempinga yeye amempinga Mungu; yeyote anayebishana na yeye amebishana na Mungu. …

77.3 Mbali na suala la kutokufanya makosa, kuna suala la mamlaka. Barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi hueleza: "Siyo kwa waumini binafsi kuweka mipaka eneo la mamlaka ya Mlinzi, au kuamua wakati gani wamtii Mlinzi na wakati gani wapo huru kuyakana maamuzi yake. Msimamo kama huu kwa uwazi ungesababisha mkanganyiko na utengano." Kuhusu Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, uelewa kama huo huo unahusika.

77.4 Kutokufanya makosa ni dhana ya ndani sana ya kiroho iliyomo katika Maandiko ya Kibahá'í. Katika kutafakari juu ya vifungu husika, waumini kwa kawaida watafikia uelewa wao binafsi juu ya mada. Maoni ya mtu binafsi, hata hivyo, hayapaswi kushurutishwa juu ya wengine, wala kuyakuza hadi kuwa itikadi ambazo hazipatikani katika Maandiko dhahiri. Wanapobadilishana mawazo kuhusu Nyumba ya Haki ya Ulimwengu–shirika ambalo kwalo mambo yote lazima yarejelewe—marafiki sharti wachukue tahadhari wasije kuvuka mipaka, ama kwa kupunguza daraja lake au kuipatia sifa zilizokuzwa. Ni onyo gani zuri zaidi kuzingatia katika suala la aina hii kuliko lile lililotolewa na mpenwa Bwana, wakati baadhi ya waumini walipoangukia katika kutokukubaliana juu ya daraja Lake Mwenyewe:

Majadiliano haya hayataleta matokeo wala manufaa; lazima tuweke kando kabisa malumbano na mabishano yote kama haya–la, lazima tuyasaha na kuinuka kutimiza kile kilichoamriwa na kinachohitajika katika Siku hii. Malumbano haya ni manemo matupu yasiyo na maana ya kindani, ni njozi tu na siyo uhalisia.

Kile ambacho ni cha kweli na halisi ni hiki: kwamba tuungane na tukubaliane katika kusudi letu na tuinuke kuujaza mwanga ulimwengu huu wa giza, kuondoa chuki na ugeni kutoka miongoni mwa watoto wa watu, kuutia manukato na kuuhuisha ulimwengu kwa upepo mwanana mtakatifu wa tabia na mwenendo wa Uzuri wa Abhá, kutawanya mwanga wa uongozi mtakatifu juu ya Mashariki na Magharibi, kuinua hema la upendo wa Mungu na kukusanya watu wote chini ya kivuli chake kilindacho, kujalia juu ya kila roho iliyo chini ya kivuli cha Mti uliobarikiwa amani na utulivu, kuonesha upendo kama ule kiasi cha kumshangaza adui, kuwageuza mbwa-mwitu walafi na wenye kiu ya damu kuwa swala wa konde la upendo wa Mungu, kumfanya dhalimu kuonja ladha tamu ya upole, kuwafundisha wale wauaji kujisalimisha na kuwa kama wale wanaojitoa wenyewe kuuawa, kueneza mbali aya za Mungu mmoja wa kweli, kusifu njema na ukamilifu wa Bwana mwenye utukufu-wote,
kuinua hadi mbingu ya juu kabisa wito wa "Ee ewe Mtukufu wa Utukufu wote!", na kusababisha mwito wa "Dunia itang'aa kwa mwanga wa

Bwana wake9!" kuyafikia masikio ya wakaazi wa Ufalme Wake.

77.5 Nyumba ya Haki inawaasa marafiki kutojihusisha na aina ya majadiliano yasiyo na faida ya kiteolojia yaliyosababisha migogoro na mabishano katika vipindi vilivyopita, wasije wakapoteza muelekeo wa jukumu lao la kutangaza umoja wa binadamu na lile la Agano lililowekwa na Bahá'u'lláh katika kuunganisha fikra, mioyo na roho.
*(Kutoka barua ya 7 Aprili 2008 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Hakiya Ulimwengu kwa Marafiki wa Irani)*

78.1 Inatia moyo kuona kwamba marafiki wanauendea ujifunzaji wa jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu zinazohusiana na Mpango kwa bidii yenye uangalifu. Kiwango cha majadiliano yanayofanywa wakati wakijidiisha kuweka katika vitendo miongozo iliyopokelewa, na kujifunza kutokana na uzoefu, inavutia. Hatuwezi kukosa kutambua, hata hivyo, kwamba mafanikio yanaelekea kudumu zaidi katika maeneo yale ambamo marafiki hujitahidi kuelewa ujumla wa maono yanayowasilishwa katika jumbe, ilhali mara nyingi matatizo huibuka wakati vifungu vya maneno na sentensi vinapochukuliwa nje ya muktadha na kuangaliwa kama vipande vipande vilivyotengwa. Asasi na mawakala wa Imani sharti wawasaidie waumini kuchambua lakini siyo kukataa, kutafakari maana lakini siyo kubakia sana kwenye maneno, kutambua maeneo bainifu ya kiutendaji lakini siyo kuyatenganisha. Tunatambua kwamba si kazi ndogo. Jamii huongea zaidi na zaidi kwa msamiati. Tunatumaini kwamba mazoea ambayo marafiki wanayajenga katika masomo ya mzunguko ya kufanya kazi na mawazo kamili na yenye utata na kufikia uelewa, yataenezwa hadi kwenye maeneo mbali mbali ya shughuli.
*(Kutoka ujumbe wa 28 Desemba 2010 ulioandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara)*

79.1 Kama inavyoendelea kuonekana wazi zaidi, mchakato hai wa ukuaji uliofafanuliwa na Nyumba ya Haki katika Mipango ya hivi karibuni umefikia viwango vya juu zaidi vya utata, hasa katika klasta zile ambapo idadi ya washiriki watendaji imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Mabadiliko ya jumuiya yanayoendelea kote ulimwenguni katika

klasta baada ya klasta, japokuwa bado zipo katika hatua zake za awali, huzigusa nguvu za kimsingi sana za kijamii na kiutamaduni, mielekeo, na matarajio. Mchakato huu wa ukuaji huhusisha mtindo unaofungamana na wa kimfumo wa shughuli unaolenga juu ya ujengaji wa jumuiya na kujumuisha uongezekaji wa vikundi vya mafunzo na kampeni za taasisi, elimu ya watoto, uwezeshaji wa kiroho wa vijana chipukizi, jitihada za ufundishaji za mtu binafsi na za pamoja, ziara kwenye nyumba za waumini na marafiki zao, uendelezaji wa maisha ya kiibada ya pamoja na matendo ya kijamii, ushiriki mkubwa zaidi katika mazungumzo ya kijamii, pamoja na vipengele vingine vingi vitakavyoboresha uwezo wa watu binafsi, asasi na jamii–wahusika wakuu watatu wa Mpango. Mhimili kwa mtindo huu wa shughuli ni ukuzaji wa rasilimali watu kupitia taasisi ya mafunzo, na mfululizo wa kozi ambazo huimarisha katika washiriki mkao wa ujifunzaji ambao kwake uelewa huendelea kupanuka kadiri wanavyootekeleza vitendo vya huduma vinavyoongezeka kwa utata. Mchakato huu wa kielimu hulea kiu kwa ajili ya Neno la Mungu, siyo tu kukuza tabia ya kudumu ya ujifunzaji na tafakari juu ya ile chemchemi ya ukuaji wote, lakini pia kuwawezesha marafiki kutumia Mafundisho katika maisha yao wenyewe na katika maisha ya mapambano ya jumuiya. Katika mawasiliano yake na ulimwengu wa Kibahá'í, Nyumba ya Haki imeeleza na kufafanua maendeleo haya yanayokunjulika, na Washauri na Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, Washauri Wasaidizi na wasaidizi wao, vile vile asasi za kikanda na za mahali, wamefanya kazi bega kwa bega na waumini wanaojitahidi kuelewa na kuitikia muongozo huu.

Kadiri marafiki, wakijumuisha wale wasiopendelea kujifunza kozi za taasisi, wanapokumbatia miongozo ya Nyumba ya Haki katika ujumla wake na, kwa upendo na kwa moyo wa kweli wa Kibahá'í, wakiandamana kuzizunguka asasi zao, wanakuta kwamba maswali ambayo wangeweza kuwa nayo yanasuluhishwa.
*(Kutoka barua ya 18 Januari 2013 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa)*

---

[9] *Qur'án 39:69*

80.1 Kama bila shaka unavyofahamu, mafundisho ya Kibahá'í husisitiza mambo yote mawili kutobadilika kwa sheria za Bahá'u'lláh na unyumbulikaji unaohusiana na matumizi yake. Bahá'u'lláh ameipa Nyumba ya Haki jukumu la kuongezea na kutumia sheria Zake, na Yeye husema kwamba Wajumbe wake "waweze kutenda kulingana na mahitaji na masharti ya wakati."
*(Kutoka barua ya 1 Desemba 2013 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

81.1 Katika kujitahidi kuondokana na matatizo yao na kuunda ruwaza mpya za utendaji, marafiki wanapaswa, ama kama watu binafsi au wajumbe wa asasi, kuzingatia onyo la `Abdu'l-Bahá kuhusu umuhimu wa upendo na upatano na uhakikisho Wake kwamba "ni katika umoja ukweli utafumbuliwa na kosa kusahihishwa". Mfumo ambao Bahá'u'lláh ameuleta ulimwenguni utachukua miongo na karne kukunjuka, ukifikia viwango vinavyoongezeka daima vya utata, ufanisi na ushawishi. Shoghi Effendi alieleza kwamba "lazima tuwe na imani na wakati, na uongozi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ya Mungu, kupata uelewa dhahiri na mkamilifu zaidi wa maelekezo na athari zake." Pia alionya kwamba "utukufu ulioahidiwa wa Milki ambao mafundisho ya Kibahá'í yanaubashiri unaweza tu kufunuliwa katika ukamilifu wa wakati."
*(Kutoka barua ya 17 Februari 2014 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

82.1 Utawala wa Kibahá'í, bila shaka, ni sehemu muhimu ya Mafundisho ya Bahá'u'lláh. Kisha, kwa hiyo, ni jukumu endelevu la wapendwa Wake kujiongezea ufahamu wao wa kuthamini kanuni ambazo juu yake umejengwa na kuzitii kwa uaminifu katika vitendo vyao. Asasi za Utaratibu wa Kiutawala wa Kibahá'í, Mlinzi husema, huwa kama mifereji ambayo kupitia humo baraka zilizoahidiwa na Bahá'u'lláh huweza kutiririka. Zinatumika "kuendeleza maslahi, kuratibu shughuli, kutumia kanuni, kuwakilisha maadili na kutekeleza kusudi la Imani ya Kibahá'í" na kufanya kazi "siyo tu kama kiini bali ruwaza yenyewe ya Utaratibu Mpya wa Ulimwengu.

*(Kutoka barua ya 9 Julai 2015 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa)*

83.1 Nyumba ya Haki imetuomba kukuhakikishia kwamba inatambua dukuduku yako ya kina uliyonayo kuhusu uwakilishi wake kuwekwa maalum kwa wanaume, hali kadhalika heshima yako kwa kanuni ya usawa wa kijinsi. Walakini, kama Nyumba ya Haki ilivyoelezea hapo awali, "jambo muhimu kwa Wabahá'í kukumbuka ni kwamba katika suala la matamshi dhahiri katika Maandiko Matakatifu ya Kibahá'í yanayoweka usawa wa wanaume na wanawake, kutostahili kwa wanawake kuwa wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haiweki ushuhuda wa ubora wa wanaume juu ya wanawake." Kuhusu uwakilishi kwenye Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, mpendwa Mlinzi alieleza katika barua ya 14 Desemba 1940 iliyoandikwa kwa niaba yake: "Kutokana na ukweli kwamba hakuna usawa wa majukumu baina ya jinsi, mtu hapaswi, hata hivyo, kuchukulia kwamba jinsi yoyote kiasili ni bora au duni kuliko nyingine, au kwamba hawana usawa katika haki zao." Kwamba hatuwezi kwa sasa kuelewa hekima ya mipaka hii–hekima ambayo `Abdu'l-Bahá aliahidi kwa msisitizo hatimaye ingekuwa dhahiri–haimaanishi kwamba hekima hii haipo au hatimaye haitakuja kujulikana hapo baadaye.

83.2 Baada ya kukubali dai la Bahá'u'lláh kwamba ni Mdhihirishaji wa Mungu na kwamba Mafundisho Yake ni matamko ya ukweli mtakatifu, waumini wanaweza kuhakikishiwa kwamba maelezo yaliyomo

katika Maandiko kuhusiana na uwakilishi kwenye Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hayahitilafiani na kanuni ya usawa wa wanaume na wanawake ambapo Maandiko hayo hayo hutangaza. Kama Shoghi Effendi alivyosema kuhusiana na hili …, "Wabahá'í sharti wakubali tamko hili la Bwana kwa moyo wa imani ya kina, wakiamini kwamba kuna muongozo wa kimungu na hekima nyuma yake ambayo pole pole itakunjuliwa mbele ya macho ya ulimwengu."10
*(Kutoka barua ya 16 Februari 2016 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

84.1 Usomaji makini wa maandiko ya Kibahá'í na miongozo ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huweza kufafanua wazi jinsi mambo mawili ambayo huonekana kuwa na mvutano baina yao yanaendana pale ambapo muktadha na kanuni zinazoyaunganisha zinapoeleweka. Hali maalum mahali fulani, wakati unaofaa, na uhitaji wa umakinikiaji wa kipindi hadi kipindi pia vina athari juu ya masuala kama hayo.
*(Kutoka barua ya 27 Aprili 2017 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

85.1 Kama vile Mlinzi alivyopokea uhakikisho wa uongozi mtakatifu na ulinzi katika kutimiza majukumu yake, vivyo hivyo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imepewa uhakikisho huu katika Maandiko Matakatifu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Ni uongozi huu, kuliko uwezo mwingine wowote kwa ajili ya fasiri ya kimamlaka, ambao huhakikisha upatanishaji wa maamuzi yake na maana ya Maandiko Matakatifu. …

85.2 … ili kutimiza majukumu yaliyoteuliwa kitakatifu kama hayo na kufikia mahitimisho yake yanayoongozwa kitakatifu juu ya kile ambacho Wabahá'í wanapaswa kufanya wakati maana ya Kitabu haipo dhahiri, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutafakari kwa makini na kikamilifu yote mawili; Maandiko Matakatifu na maandiko ya Shoghi Effendi juu ya mada na kisha kufikia uamuzi.
*(Kutoka barua ya 19 Machi 2018 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

86.1 Barua yako inayouliza kuhusu masuala fulani fulani yanayojadiliwa miongoni mwa marafiki kuhusiana na kutofanya makosa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilipokelewa …

86.2 Kama ujuavyo kwa hakika, kuna matamko mengi katika maandiko ya Kibahá'í ambayo huweka kwa hali ya mapana na msisitizo uhakikisho wa uongozi mtakatifu na ulinzi uliotolewa kwa Mlinzi na kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na huelezea kutotenda makosa walikojaliwa katika namna hii. Miongoni mwa matamko haya ni haya yanayofuata ya `Abdu'l-Bahá:

> Tawi takatifu na chipukizi, Mlinzi wa Hoja ya Mungu pamoja na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, itakayochaguliwa na kuanzishwa na wote, zote zipo chini ya uangalizi na ulinzi wa Uzuri wa Abhá, chini ya hifadhi na ulinzi wa uhakika wa Yule Aliyetukuka (maisha yangu na yatolewa dhabihu kwa ajili yao wote). Lolote waamualo ni la Mungu. Yeyote asiyemtii yeye, wala kuwatii wao, hajamtii Mungu; yeyote anayeasi dhidi yake na dhidi yao ameasi dhidi ya Mungu; yeyote anayempinga yeye amempinga Mungu; yeyote anayebishana na yeye amebishana na Mungu. …

***

> Kwenye Kitabu Kitakatifu Kabisa kila mmoja lazima ageukie na chochote ambacho hakijaandikwa kwa uwazi humo lazima kirejelewe Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Kile ambacho shirika hili litaamua, iwe kwa sauti ya wote au kwa wingi wao, hicho kwa hakika ndiyo kweli na Kusudi la Mungu Mwenyewe.

***

[10]*tazama dondoo 15.*

Ikiwa Nyumba hiyo ya Haki huamua, iwe kwa kauli moja au kwa wingi, juu ya suala ambalo halikuandikwa wazi wazi katika Kitabu, uamuzi huo na amri vitalindwa kutoka makosa. Sasa, wajumbe wa Nyumba ya Haki kama watu binafsi siyo lazima kwamba hawawezi kutenda makosa, lakini shirika la Nyumba ya Haki lipo chini ya ulinzi na uongozi usiookosea wa Mungu: huku huitwa majaliwa ya kutotenda makosa.

***

Acha isidhaniwe kwamba Nyumba ya Haki itafanya uamuzi wowote kulingana na dhana na mawazo yake yenyewe. Mungu apishie mbali! Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki itafanya maamuzi na kuanzisha sheria kupitia uvuvio na uthibitisho wa Roho Mtakatifu, kwa sababu ipo katika usalama na chini ya hifadhi na ulinzi wa Uzuri wa Kale, na utii kwa maamuzi yake inapasa na ni wajibu muhimu na jukumu kamilifu na hakuna nafasi ya kukwepa kwa yeyote.

Sema, Enyi watu: Kwa hakika, Nyumba ya Juu Kabisa ya Haki ipo chini ya mabawa ya Bwana wenu, Mwenye Huruma, Mwenye Rehema—Zote, yaani, chini ya ulinzi Wake, uangalizi Wake na hifadhi Yake; kwa kuwa Yeye amewaamuru waumini thabiti kutii shirika hilo lililobarikiwa, kutakasika na litiishalo, ambalo mamlaka yake yameamriwa kitakatifu na ya Ufalme wa Mbinguni na ambalo sheria zake huvuviwa na ni za kiroho.

*Aidha, Shoghi Effendi husema:*

Katika uendeshaji wa masuala ya kiutawala ya Imani, katika utungaji wa sheria muhimu katika kujaliza sheria za Kitáb-i-Aqdas, wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, inapaswa izingatiwe, kama matamshi ya Bahá'u'lláh yanavyoashiria wazi, hawawajibiki kwa wale wanaowawakilisha, wala hawaruhusiwi kutawaliwa na hisia, mtazamo wa jumla, na hata ushawishi wa umma wa waaminifu, au wa wale wanaowachagua moja kwa moja. Watatakiwa kufuata, katika hali ya sala, muongozo na ushawishi wa utashi wao. Wanaweza, hakika inawalazimu,

wajizoeze wenyewe na hali iliyopo ndani ya jamii, lazima wapime bila upendeleo akilini mwao manufaa ya hoja yoyote inayowasilishwa kwao kwa ajili ya maamuzi yao, lakini lazima wajihifadhie ile haki ya uamuzi usiofungamana. "Mungu kwa hakika atawavuvia kwa chochote kile Atakacho," ni uhakikisho usiopingika wa Bahá'u'lláh. Ni wao, hivyo, na siyo kundi la wale ambao huwachagua ama kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, ambao wamefanywa kuwa wapokeaji wa muongozo mtakatifu ambao papo hapo ni damu ya uhai na ndiyo kinga ya mwisho ya Ufunuo huu.

86.3 Mbali na haya na nukuu zingine, vifungu kadhaa kutoka maandiko vinaelezea anuwai ya majukumu aliyopewa Mlinzi na iliyopewa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Ya kwanza, ni wazi kwamba kila moja ina eneo tofauti na la kipekee la kiutendaji. Kama Shoghi Effendi anavyoelezea katika "Kipindi cha Bahá'u'lláh", "imewekwa dhahiri na pasipo shaka kwamba Mlinzi wa Imani amefanywa kuwa Mfasiri wa Neno na kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imejaliwa kazi ya utungaji sheria juu ya masuala ambayo hayajafunuliwa wazi wazi katika mafundisho." Hivyo, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haijihusishi na fasiri ya Maandiko, na Mlinzi hakutunga sheria, ingawa katika hali fulani fulani, kama Mkuu wa Imani, alifanya maamuzi kadhaa ili kuongoza vitendo vya marafiki hadi wakati ule ambapo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ingesimikwa.

86.4 Wakati fasiri na utungaji wa sheria ni maeneo ya kipekee, mtawalia, ya Mlinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kazi hizi haziwakilishi kwa vyovyote kiwango kamili cha mamlaka na majukumu yao kama ilivyowekwa katika maandiko. Kwa mfano, kuhusu asasi hizi mbili Shoghi Effendi ameandika: "Lengo lao la pamoja, la kimsing ni kuhakikisha kuendelea kwa mamlaka ile iliyoteuliwa kitakatifu ambayo hutiririka kutoka Chanzo cha Imani yetu, kulinda umoja wa wafuasi wake na kuhifadhi uadilifu na unyumbulikaji wa mafundisho yake. Zikifanyakazi kwa ushirikiano moja kwa nyingine asasi hizi mbili zisizotenganishwa husimamia mambo yake, huratibu shughuli zake, hukuza maslahi yake,

hutekeleza sheria zake na kulinda asasi zake saidizi.” Zaidi, kuhusu Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, `Abdu’l-Bahá amesema katika Wasia na Agano Lake, “Kwa chombo hiki matatizo yote magumu yatatatuliwa….” Na anaeleza kwamba inaipasa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kujadiliana juu ya “matatizo yote ambayo yamesababisha mfarakano, maswali ambayo yana utata na masuala ambayo hayajaandikwa wazi wazi katika Kitabu.”

86.5 Katika kujibu maswali yanayohusu upeo wa kutotenda makosa kwa Mlinzi, barua iliyoandikwa kwa niaba yake inaeleza: “Kutotenda makosa kwa Mlinzi kumewekewa mipaka kwa mambo yanayohusiana hasa hasa na Hoja na fasiri ya mafundisho Yake; yeye si mamlaka isiyokosea juu ya mambo mengine, kama vile uchumi, sayansi, n.k.” Barua nyingine kama hiyo hueleza: “Kutokutenda makosa kwa Mlinzi kunahusu fasiri ya neno lililofunuliwa, na matumizi yake”. Hali kadhalika, maagizo yoyote awezayo kutoa yanayohusiana na ulinzi wa Imani, au usitawi wake, lazima yatiiwe kwa ukaribu, kwani yeye hatendi makosa katika ulinzi wa Imani. Yeye anahakikishiwa muongozo wa wote wawili Bahá’u’lláh na Báb, kama Wasia na Agano la `Abdu’l-Bahá linavyofunua wazi.” Hivyo, wakati kwa hakika kulikuwa na mipaka kwenye majaliwa ya kutotenda makosa, haikuzuiliwa tu kwenye fasiri ya kimamlaka ya Maandiko ya Kibahá’í bali kulipanuliwa hadi kwenye upeo wa majukumu yake kama Mlinzi na Mkuu wa Imani. “Si ruksa kwa waumini binafsi kuwekea mipaka eneo la mamlaka ya Mlinzi, au kuamua ni wakati gani wanapaswa kumtii Mlinzi na wakati gani wana uhuru kukataa maamuzi yake. Tabia kama hiyo husababisha mkanganyiko na mfarakano”, bado barua nyingine iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi husema: Vifungu hivi vinavyohusu majaliwa ya kutotenda makosa kwa Mlinzi na mamlaka yake vinaweza pia kutumika kuwasaidia waumini katika uelewa wa upeo wa majaliwa ya kutotenda makosa na mamlaka ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

86.6 Hatimaye, unauliza kama inawezekana kutunga sheria ndani ya kiunzi cha Maandiko ya Bahá'u'lláh bila uelewa kamili na sahihi wa maana ya kila moja ya Maandiko. Katika Maandiko ya Bahá'u'lláh na `Abdu'l-Bahá, hakuna rejeleo kwenye asili na kiwango cha taarifa ambayo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ingebidi kukipata wakati ikifanya uamuzi wake. Nyumba ya Haki yenyewe huamua ni taarifa gani inahitaji kufikia uamuzi. Kabla ya kutunga sheria au kuamua juu ya jambo lolote muhimu, hutafakari kwa makini na kikamilifu yote mawili; Maandiko Matakatifu na maandiko ya Shoghi Effendi juu ya mada. Pia hutafuta maoni ya wataalam kama inavyohitajika. Dhana ya majaliwa ya kutotenda makosa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu haitegemei juu ya nguvu ya fasiri ya kimamlaka wala upataji wa maarifa kamili na uelewa—ni uhakikisho usiohitaji sifa wa muongozo mtakatifu na ulinzi kutokana na makosa kama inavyofafanuliwa katika maandiko ya Kibahá'í.

86.7 Majadiliano juu ya dhana ya majaliwa ya kutotenda makosa yanayosisitza muongozo mwingi uliowekwa katika maandiko ya Kibahá'í na kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huweza kuchangia uthabiti na imani. Walakini marafiki wasiwe wajinga au kusita linapokuja suala la kimsingi kama vile ulinzi wa Hoja na uadilifu wa mafundisho kama maagizo yalivyo katika Agano. Wale wanaopinga Imani na kwa masikitiko, katika maeneo machache, waumini ambao wanapenda kuendeleza maoni yao binafsi, wanaweza kutumia majadiliano kama haya kama fursa kudhoofisha imani ya Wabahá'í kwa uongozi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

Wakati wa kipindi cha utumishi wa Mlinzi, je, ukosefu wake wa ujuzi wote ungekuwa sababu ya marafiki kuhoji kitendo chake cha kiulinzi cha kumfukuza mtu kutoka kwenye Imani? Je, maagizo ya Mpambano wa Miaka Kumi yalitegemea matakwa ya marafiki walio wengi? Je, hatua za muda za kiutawala alizotunga kabla ya uanzishwaji wa Nyumnba ya Haki ya Ulimwengu zilikuwa wazi kwa ajili ya malumbano kwa watu binafsi au asasi? Bila uhakikisho wa Bahá'u'lláh na`Abdu'l-Bahá kutegemea kitovu kilichoteuliwa na chenye mamlaka, mtu yeyote binafsi angeweza kusisitiza

usahiihi wa maoni yake juu ya jambo lolote, na Imani ingekwama katika mabishano, machafuko na mgawanyiko yasiyo na kikomo.
86.8 Hivyo, pengine kilicho muhimu zaidi kwa Wabahá'í kuliko uelewa wa pamoja wa maana ya majaliwa ya kutotenda makosa ni uelewa wa pamoja wa kusudi lake na matokeo kwa jinsi wanavyotakiwa kuenenda. Agano huweka kituo ambacho kwacho Wabahá'í wote hukigeukia, kituo ambacho kimehakikishiwa uongozi na ulinzi mtakatifu, na ambacho huhakikisha muendelezo wa mamlaka iliyoteuliwa kitakatifu ambao hutiririka kutoka Chanzo cha Imani, kinacholinda umoja wa wafuasi wake na kudumisha uadilifu na unyumbulikaji wa mafundisho yake. Shoghi Effendi hueleza kwamba Bahá'u'lláh na `Abdu'l-Bahá "kwa lugha isiyo na shaka na yenye msisitizo, waliteua zile asasi pacha za Nyumba ya Haki na ya Ulinzi kama Warithi wao waliowachagua, waliokusudiwa kutekeleza kanuni, kutangaza sheria, kulinda asasi, kuoanisha kwa uaminifu na kiakili Imani na mahitaji ya jamii inayoendelea, na kukamilisha urithi usioharibika ambao Waasisi wa Imani wameuachia ulimwengu."  Huu ni uhakikisho kwamba kusudi la Bahá'u'lláh hatimaye litatimizwa. "Kwani hakuna kingine pungufu ya maelekezo ya wazi ya Kitabu chao, na lugha yenye msisitizo wa kushangaza ambayo kwayo wamevika maelekezo ya Wasia wao," Shoghi Effendi hueleza, "yangeweza kuilinda Imani ambayo kwa ajili yake wote wawili wameitumikia kitukufu mno katika maisha yao yote. Hakuna kingine pungufu ya hiki kingeweza kuilinda kutokana na uasi na uzushi ambavyo kwavyo madhehebu, watu na serikali wamefanya juhudi, na wataendelea, kwa nguvu kubwa, kufanya juhudi kuishambulia siku zijazo." Katika tamko la kutetea Agano, `Abdu'l-Baha huelekeza:

Je, kwani Uzuri Uliobarikiwa alianzisha Agano na Wasia huu ili kushurutisha utii wa wote au kusababisha uasi? Ikiwa lile la mwisho ndilo kusudi, basi, hatuna cha kusema; lakini ikiwa utiifu na ukubali ndiyo lengo, basi kusita kutasababisha hasara kabisa, na kutotii na upotofu ni kosa kubwa.

Tena anasema:

Sasa mtu anapaswa ama aseme kwamba Uzuri Uliobarikiwa amekosea na aliwapotosha watu, kwani aliwaelekeza kumtii mtu ambaye asingestahili kutiiwa, au vinginevyo aseme kwamba mkengeuko mdogo kabisa kutoka kwenye Agano na Wasia husababisha kunyimwa fadhili za Yeye Ambaye ni Mwangaza wa ulimwengu. Kati ya chaguo hizi mbili, lazima moja ni la kweli, hakuna chaguo la tatu.

86.9 Ni dhahiri kwamba kusudi la Agano, kusudi la muongozo na ulinzi mtakatifu vilivyopewa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kusudi la lugha ya wazi na yenye msisitizo ambayo kwayo hakikisho la muongozo huu limetolewa, vyote ni kwa ajili ya kusimika na kuhifadhi umoja wa Imani. Bila Agano kama hili, kama ilivyokuwa katika vipindi vilivyopita, kila mmoja angesisitiza juu ya usahihi wa maoni yake, Imani ya Mungu ingevunjika-vunjika, na kusudi takatifu—umoja wa binadamu—usingeweza kufikiwa.

86.10 Marafiki wangefanya vizuri kutafakari “Mfumo huu wa kipekee, wa ajabu” alioutoa Bahá’u’lláh kwa ulimwengu. Shoghi Effendi hueleza: “Ufahamu sahihi na mkamilifu wa mfumo mkubwa mno kiasi hicho, ufunuo wenye utukufu mno kiasi hicho, dhamana takatifu mno kiasi hicho, kwa sababu zilizo wazi, huzidi ufikiaji na ufahamu wa akili zetu zenye mipaka”; hata hivyo, anatuhakikisha: “Tunaweza, walakini, na ni wajibu wetu wa lazima kutafuta kupata uvuvio mpya na riziki iliyoongezwa kadiri tunavyojitahidi kutangaza Imani Yake kupitia uelewa dhahiri zaidi wa kweli zinazo ndani yake na kanuni ambazo juu yake hutegemezwa.” Kujaribu kufafanua kwa usahihi utendaji wa majaliwa ya kutotenda makosa, kuhusisha nguvu zilizokithiri kwa Nyumba ya Haki kama vile ajuaye yote au hata fasiri za kimamlaka, au kusisitiza kwamba watu wawezao kutenda makosa wanaweza kutumia nguvu zao za fikra zenye mipaka kupima uhalali wa maamuzi yanayoongozwa kitakatifu na kuamua kuyapinga ingekuwa ni kazi bure, na hatimaye, vyenye madhara.

Bali, marafiki wanatakiwa kujitahidi kuelewa miongozo inayotolewa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na kuitumia kiakili. Wapo huru kushirikiana maoni, taarifa au maswali na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Lakini wasijiruhusu kunaswa kwenye mazoea yenye mgawanyiko na migogoro migumu ambavyo vimeangamiza dini katika vipindi vilivyopita. Masilahi ya pamoja ya Imani hukuzwa kupitia ushauriano na ushirikiano, siyo ugomvi na kushindana.
*(Kutoka barua ya 18 Mei 2018 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)*

87.1 Nyumba ya Haki inakiri kupokea maoni yako angalifu na yanayogusa moyo kuhusu uhusiano baina ya kanuni ya usawa wa kijinsi na kuzuiliwa kwa wanawake kuhudumu katika Nyumba ya Haki. Kama utambuavyo, Bahá'u'lláh Mwenyewe ameanzisha kanuni ya usawa wa wanaume na wanawake. Kama Yeye alivyoweka kanuni hii, pia aliagiza, kama ilivyothibitishwa katika matamko ya kimamlaka ya `Abdu'l-Bahá na Shoghi Effendi, kwamba uwakilishi kwenye Nyumba ya Haki uwekwa maalum kwa wanaume. Katika barua yako, unachunguza vipengele anuwai na kuhitimisha kuwa huwezi kukubali "sababu zilizotolewa hadi sasa". Hata hivyo, hakuna sababu iliyotolewa katika maandiko ya Kibahá'í, na Nyumba ya Haki haijatoa hata moja. Katika maandiko ya Kibahá'í, kuna rejeleo tu kwenye "hekima" kwamba "itakunjuliwa pole pole kwenye macho ya ulimwengu". Bila shaka, kwamba hatuwezi kwa sasa kuelewa hekima ya mipaka haimaanishi kwamba hekima hii haipo au hatimaye haitakuja kujulikana hapo baadaye. Mpaka hapo, kwa sababu sisi ni Wabahá'í tunamtambua Bahá'u'lláh kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii na kuweka Imani yetu Kwake kama Tabibu Mtakatifu ambaye ataponya tatizo la kutokuwa na usawa kijinsi, tunakiri kanuni kwamba "Yeye hufanya chochote Apendacho".
*(Kutoka barua ya 18 Juni 2019 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi*

# *Faharasa*


Utaratibu wa Utawala, 69.1, 70.4, 71.5, 73.1, 82.1
msaada wa waumini wa, 50.1; imani, 57.14,
58.10, 83.2; unyenyekevu, 57.14, 58.11,
71.5; upendo, 70.13, 77.4, 81.1 mfereji ambao kupitia huo baraka hutiririka, 82.1
Unyumbulikaji katika vipengele vya pili, 55.1,
65.4, 70.4
asasi za, huibuka kwa nguvu, 32.1–3, 73.1
viini na muundo wa Utaratibu wa Ulimwengu,
34.1, 54.1, 73.1, 82.1
asili ya, 1.1, 4.1–2, 33.1–3, 38.1, 59.15
na mifumo mingine ya serikali, 39.1, 70.7–10, 70.12
nguzo pacha za, 38.2, 63.2
bila Mlinzi, 38.4, 57.10, 58.9, 70.10, 76.9
Aghṣán, cheo cha, 76.10 Vituo vya kimamlaka, 16.1, 59.5, 59.15, 86.7
Utakatifu, muendelezo wa, 38.3, 46.1, 51.1,
55.1, 58.8, 63.2, 72.1, 86.4, 86.8
ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 52.1, 53.1, 77.2–3; kama shirika ambalo kwalo wote lazima wageukie, 13.1, 52.2, 58.15–16,
59.15, 76.17, 86.8; kama shirika ambalo kwalo vitu vyote lazima virejelewe, 11.1,
55.1, 77.4; asili pana ya, 71.8,
77.2–3, 86.4; kutengeneza sheria ndogondogo (tazama chini ya sheria za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu); juu ya masuala ambayo hayajafunuliwa wazi wazi, 5.1,
12.1–2, 20.1, 36.1, 57.11, 57.13, 58.15, 59.15, 70.3, 71.8, 75.1, 76.2, 76.21, 86.2, 86.4; juu ya maswali yanayogubika, 12.2, 53.1, 57.3, 57.13, 57.15, 59.6, 70.3, 71.8, 76.2, 86.4;
Juu ya matatizo ambayo husababisha tofauti,
12.2, 16.1, 17.1, 53.1, 57.8, 57.13, 59.6, 70.3, 71.8, 76.2, 76.8, 86.4;
kutengua sheria zake yenyewe, 12.2, 37.1,
46.1, 57.13, 65.4, 68.1, 75.1
Warithi pacha, 34.1, 34.3, 51.1, 57.11, 86.8

Carmel, Waraka wa, 4.1–2, 33.3, 42.1, 49.1
Asasi za Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na Kitaifa, 59.17, 65.4, 70.4
Asasi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 51.1, 52.1–2, 53.1, 54.1, 57.16, 58.17, 70.4
Ufisadi, ulinzi dhidi, 2.1, 34.1–5, 35.1, 59.14, 69.1, 77.1
Agano, 2.1, 10.1, 22.2, 34.2–3, 55.1, 57.14, 57.11, 58.10, 59.12, 61.1, 70.2–3, 71.5, 76.20, 77.5, 86.7–9 mfereji wa mwongozo mtakatifu umebakia wazi, 55.1, 71.5, 86.8
Muendelezo wa, 4.2, 59.14, 76.9, 86.8
Kuu Kabisa na Ndogo Kabisa, 61.1
uvunjaji Agano, 13.1, 16.2, 57.7, 57.16, 71.9, 76.17–22, 86.2

uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 20.1, 32.1, 54.1, 70.9, 86.2 mbinu ya, 10.1, 11.1, 12.1, 17.2–3, 22.1, 57.8, 76.13, 76.21
mchakato wa hatua tatu, 29.1–3, 57.8,

76.13 upatiaji muda wa, 32.3, 33.3, 48.1, 54.1, 57.3,
57.6, 57.9, 58.1, 76.3–4 ufafanuzi, 53.1, 57.13, 75.1 uanzishwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 4.1–2, 8.1–2, 23.1, 30.1,
33.3, 42.1, 49.1, 59.15, 76.13–16 maandalizi kwa, 24.1, 25.1, 26.1, 28.1, 33.1–2, 41.2, 47.1, 50.1, 57.14,
70.11, 76.4, 76.14

Kazi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu
Ufanyaji maamuzi, msingi wa, 17.1, 19.2,
39.1, 58.7, 76.9, 86.2; dhamiri ya mtu binafsi, kuhusiana na,
65.4, 68.1–2, 77.1; ushauriano katika mchakato wa, 5.1, 59.8; kweli, jukumu la, 63.2, 72.1, 86.6; makatazo ya Mlinzi, jinsi ilivyoshughulikiwa, 59.8; mfumo, 17.1, 20.1, 21.3, 57.8,
86.2
Siku za baadaye, 26.1, 32.2, 33.3, 42.1, 67.1–2;
Kuhusiana na serikali,
11.1, 36.1

Bila Mlinzi, 57.10–11, 57.16,
58.6, 58.9, 58.12, 58.17, 59.2,
59.16–17. ’pia tazama uhusiano kati ya Nyumba ya Hakiya Ulimwengu na Mlinzi

Mlinzi wa Ulinzi, 10.1, 62.1, 76.3
nafasi katikati ya mistari, 3.1, 56.1, 57.3, 58.2,
59.12–14, 76.5, 76.8–9
mkuu wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu,
11.1, 57.11, 58.5, 59.7 jukumu la,
57.11–13, 58.4, 59.7,
62.2, 63.1, 74.1, 86.3
pia tazama uhusiano kati ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Mlinzi; Shoghi Effendi, urithi wa muongozo wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu,
13.1, 27.2, 57.6, 57.14–15, 58.3,
58.15, 59.15, 71.5, 71.9, 78.1, 79.1,
81.1, 84.1, 86.7, 86.10

Mikono wa Hoja ya Mungu, 38.1, 57.4–5,
57.7, 58.2, 58.17, 62.1–2, 76.6–7, 76.19
Mkuu wa Imani, 52.2, 62.2, 63.2, 70.11,
76.3–4, 76.17, 86.3, 86.5 heresy, 18.1, 34.4, 86.8

isiyokosea, 21.1, 45.1, 77.4
iliyojaaliwa, 21.2–3, 86.2, 86.6–8, 86.10 umuhimu, 21.1, 21.4
wa Mlinzi, 59.5, 63.1, 74.1, 77.3,
85.1, 86.5, 86.7
Mabaraza ya Kitaifa na ya mahali hayana ubia katika, 59.17
wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 86.1;
maana ya/kidokezi cha, 10.1, 17.1, 19.2,
57.8, 58.7, 59.5, 74.1, 76.21, 77.2,
86.2; na Habari inazozipokea,
72.1, 86.6; siyo mjumbe binafsi,
86.2; siyo juu ya mtu binafsi kuweka kikomo/mipaka,
77.3, 86.5; ahadi ya, 5.1, 10.1,
19.3, 39.1, 58.7, 58.16, 59.17, 77.2,
85.1, 86.2, 86.6, 86.9; mawanda ya/ eneo la/nafasi ya/uwezo wa,
77.2, 85.1, 86.5; uwanja/fani/eneo la utendaji wa kisheria, kuhusiana na,

Utaratibu wa Utawala, 69.1, 70.4, 71.5, 73.1, 82.1
msaada wa waumini wa, 50.1; imani, 57.14,
58.10, 83.2; unyenyekevu, 57.14, 58.11,
71.5; upendo, 70.13, 77.4, 81.1 mfereji ambao kupitia huo baraka hutiririka, 82.1
Unyumbulikaji katika vipengele vya pili, 55.1,
65.4, 70.4
asasi za, huibuka kwa nguvu, 32.1–3, 73.1
viini na muundo wa Utaratibu wa Ulimwengu,
34.1, 54.1, 73.1, 82.1
asili ya, 1.1, 4.1–2, 33.1–3, 38.1, 59.15
na mifumo mingine ya serikali, 39.1,
70.7–10, 70.12
nguzo pacha za, 38.2, 63.2
bila Mlinzi, 38.4, 57.10, 58.9,
70.10, 76.9
Aghṣán, cheo cha, 76.10 Vituo vya kimamlaka, 16.1, 59.5, 59.15, 86.7
Utakatifu, muendelezo wa, 38.3, 46.1, 51.1,
55.1, 58.8, 63.2, 72.1, 86.4, 86.8
ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 52.1, 53.1, 77.2–3; kama shirika ambalo kwalo wote lazima wageukie, 13.1, 52.2, 58.15–16,
59.15, 76.17, 86.8; kama shirika ambalo kwalo vitu vyote lazima virejelewe, 11.1,
55.1, 77.4; asili pana ya, 71.8,
77.2–3, 86.4; kutengeneza sheria ndogondogo (tazama chini ya sheria za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu); juu ya masuala ambayo hayajafunuliwa wazi wazi, 5.1,
12.1–2, 20.1, 36.1, 57.11, 57.13,
58.15, 59.15, 70.3, 71.8, 75.1, 76.2,
76.21, 86.2, 86.4; juu ya maswali yanayogubika, 12.2, 53.1, 57.3, 57.13, 57.15, 59.6, 70.3, 71.8, 76.2, 86.4;
Juu ya matatizo ambayo husababisha tofauti,
12.2, 16.1, 17.1, 53.1, 57.8, 57.13,
59.6, 70.3, 71.8, 76.2, 76.8, 86.4; kutengua sheria zake yenyewe, 12.2, 37.1,
46.1, 57.13, 65.4, 68.1, 75.1
Warithi pacha, 34.1, 34.3, 51.1, 57.11, 86.8

Carmel, Waraka wa, 4.1–2, 33.3, 42.1, 49.1
Asasi za Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na Kitaifa, 59.17, 65.4, 70.4
Asasi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 51.1, 52.1–2, 53.1, 54.1, 57.16, 58.17, 70.4
Ufisadi, ulinzi dhidi, 2.1, 34.1–5, 35.1, 59.14, 69.1, 77.1
Agano, 2.1, 10.1, 22.2, 34.2–3, 55.1,
57.14, 57.11, 58.10, 59.12, 61.1,
70.2–3, 71.5, 76.20, 77.5, 86.7–9
mfereji wa mwongozo mtakatifu umebakia wazi, 55.1, 71.5, 86.8
Muendelezo wa, 4.2, 59.14, 76.9, 86.8
Kuu Kabisa na Ndogo Kabisa, 61.1
uvunjaji Agano, 13.1, 16.2, 57.7, 57.16, 71.9, 76.17–22, 86.2

uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 20.1, 32.1, 54.1, 70.9, 86.2 mbinu ya, 10.1, 11.1, 12.1, 17.2–3, 22.1, 57.8, 76.13, 76.21
mchakato wa hatua tatu, 29.1–3, 57.8, 76.13 upatiaji muda wa, 32.3, 33.3, 48.1, 54.1, 57.3,

57.6, 57.9, 58.1, 76.3–4 ufafanuzi, 53.1, 57.13, 75.1 uanzishwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 4.1–2, 8.1–2, 23.1, 30.1,
33.3, 42.1, 49.1, 59.15, 76.13–16 maandalizi kwa, 24.1, 25.1, 26.1, 28.1, 33.1–2, 41.2, 47.1, 50.1, 57.14,
70.11, 76.4, 76.14

Kazi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu
Ufanyaji maamuzi, msingi wa, 17.1, 19.2,
39.1, 58.7, 76.9, 86.2; dhamiri ya mtu binafsi, kuhusiana na,
65.4, 68.1–2, 77.1; ushauriano katika mchakato wa, 5.1, 59.8; kweli, jukumu la, 63.2, 72.1, 86.6; makatazo ya Mlinzi, jinsi ilivyoshughulikiwa, 59.8; mfumo, 17.1, 20.1, 21.3, 57.8,
86.2
Siku za baadaye, 26.1, 32.2, 33.3, 42.1, 67.1–2;
Kuhusiana na serikali,
11.1, 36.1

Bila Mlinzi, 57.10–11, 57.16,
58.6, 58.9, 58.12, 58.17, 59.2,
59.16–17. ’pia tazama uhusiano kati ya Nyumba ya Hakiya Ulimwengu na Mlinzi

Mlinzi wa Ulinzi, 10.1, 62.1, 76.3
nafasi katikati ya mistari, 3.1, 56.1, 57.3, 58.2,
59.12–14, 76.5, 76.8–9
mkuu wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu,
11.1, 57.11, 58.5, 59.7 jukumu la, 57.11–13, 58.4, 59.7,
62.2, 63.1, 74.1, 86.3

pia tazama uhusiano kati ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Mlinzi; Shoghi Effendi, urithi wa muongozo wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu,
13.1, 27.2, 57.6, 57.14–15, 58.3,
58.15, 59.15, 71.5, 71.9, 78.1, 79.1,
81.1, 84.1, 86.7, 86.10

Mikono wa Hoja ya Mungu, 38.1, 57.4–5,
57.7, 58.2, 58.17, 62.1–2, 76.6–7, 76.19
Mkuu wa Imani, 52.2, 62.2, 63.2, 70.11,
76.3–4, 76.17, 86.3, 86.5 heresy, 18.1, 34.4, 86.8

isiyokosea, 21.1, 45.1, 77.4
iliyojaaliwa, 21.2–3, 86.2, 86.6–8, 86.10 umuhimu, 21.1, 21.4
wa Mlinzi, 59.5, 63.1, 74.1, 77.3,
85.1, 86.5, 86.7
Mabaraza ya Kitaifa na ya mahali hayana ubia katika, 59.17
wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 86.1;
maana ya/kidokezi cha, 10.1, 17.1, 19.2,
57.8, 58.7, 59.5, 74.1, 76.21, 77.2,
86.2; na Habari inazozipokea,
72.1, 86.6; siyo mjumbe binafsi,
86.2; siyo juu ya mtu binafsi kuweka kikomo/mipaka,
77.3, 86.5; ahadi ya, 5.1, 10.1,
19.3, 39.1, 58.7, 58.16, 59.17, 77.2,
85.1, 86.2, 86.6, 86.9; mawanda ya/ eneo la/nafasi ya/uwezo wa,
77.2, 85.1, 86.5; uwanja/fani/eneo la utendaji wa kisheria, kuhusiana na,
58.6, 59.17; bila Mlinzi,
57.10, 58.4, 58.6, 59.6

Utaratibu wa Utawala, 69.1, 70.4, 71.5, 73.1, 82.1
msaada wa waumini wa, 50.1; imani, 57.14,
58.10, 83.2; unyenyekevu, 57.14, 58.11,
71.5; upendo, 70.13, 77.4, 81.1 mfereji ambao kupitia huo baraka hutiririka, 82.1
Unyumbulikaji katika vipengele vya pili, 55.1,
65.4, 70.4
asasi za, huibuka kwa nguvu, 32.1–3, 73.1
viini na muundo wa Utaratibu wa Ulimwengu,
34.1, 54.1, 73.1, 82.1
asili ya, 1.1, 4.1–2, 33.1–3, 38.1, 59.15
na mifumo mingine ya serikali, 39.1,
70.7–10, 70.12
nguzo pacha za, 38.2, 63.2
bila Mlinzi, 38.4, 57.10, 58.9,
70.10, 76.9
Aghṣán, cheo cha, 76.10 Vituo vya kimamlaka, 16.1, 59.5, 59.15, 86.7
Utakatifu, muendelezo wa, 38.3, 46.1, 51.1,
55.1, 58.8, 63.2, 72.1, 86.4, 86.8
ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 52.1, 53.1, 77.2–3; kama shirika ambalo kwalo wote lazima wageukie, 13.1, 52.2, 58.15–16,
59.15, 76.17, 86.8; kama shirika ambalo kwalo vitu vyote lazima virejelewe, 11.1,
55.1, 77.4; asili pana ya, 71.8,
77.2–3, 86.4; kutengeneza sheria ndogondogo (tazama chini ya sheria za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu); juu ya masuala ambayo hayajafunuliwa wazi wazi, 5.1,
12.1–2, 20.1, 36.1, 57.11, 57.13,
58.15, 59.15, 70.3, 71.8, 75.1, 76.2,
76.21, 86.2, 86.4; juu ya maswali yanayogubika, 12.2, 53.1, 57.3, 57.13,
57.15, 59.6, 70.3, 71.8, 76.2, 86.4;
Juu ya matatizo ambayo husababisha tofauti,
12.2, 16.1, 17.1, 53.1, 57.8, 57.13,
59.6, 70.3, 71.8, 76.2, 76.8, 86.4; kutengua sheria zake yenyewe, 12.2, 37.1,
46.1, 57.13, 65.4, 68.1, 75.1
Warithi pacha, 34.1, 34.3, 51.1, 57.11, 86.8

Carmel, Waraka wa, 4.1–2, 33.3, 42.1, 49.1
Asasi za Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na Kitaifa, 59.17, 65.4, 70.4
Asasi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 51.1, 52.1–2, 53.1, 54.1, 57.16, 58.17, 70.4
Ufisadi, ulinzi dhidi, 2.1, 34.1–5, 35.1, 59.14, 69.1, 77.1
Agano, 2.1, 10.1, 22.2, 34.2–3, 55.1,
57.14, 57.11, 58.10, 59.12, 61.1,
70.2–3, 71.5, 76.20, 77.5, 86.7–9
mfereji wa mwongozo mtakatifu umebakia wazi, 55.1, 71.5, 86.8
Muendelezo wa, 4.2, 59.14, 76.9, 86.8
Kuu Kabisa na Ndogo Kabisa, 61.1
uvunjaji Agano, 13.1, 16.2, 57.7, 57.16, 71.9, 76.17–22, 86.2

uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 20.1, 32.1, 54.1, 70.9, 86.2 mbinu ya, 10.1, 11.1, 12.1, 17.2–3, 22.1, 57.8, 76.13, 76.21
mchakato wa hatua tatu, 29.1–3, 57.8, 76.13 upatiaji muda wa, 32.3, 33.3, 48.1, 54.1, 57.3,

57.6, 57.9, 58.1, 76.3–4 ufafanuzi, 53.1, 57.13, 75.1 uanzishwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 4.1–2, 8.1–2, 23.1, 30.1,
33.3, 42.1, 49.1, 59.15, 76.13–16 maandalizi kwa, 24.1, 25.1, 26.1, 28.1, 33.1–2, 41.2, 47.1, 50.1, 57.14,
70.11, 76.4, 76.14

Kazi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu
Ufanyaji maamuzi, msingi wa, 17.1, 19.2,
39.1, 58.7, 76.9, 86.2; dhamiri ya mtu binafsi, kuhusiana na,
65.4, 68.1–2, 77.1; ushauriano katika mchakato wa, 5.1, 59.8; kweli, jukumu la, 63.2, 72.1, 86.6; makatazo ya Mlinzi, jinsi ilivyoshughulikiwa, 59.8; mfumo, 17.1, 20.1, 21.3, 57.8,
86.2
Siku za baadaye, 26.1, 32.2, 33.3, 42.1, 67.1–2;
Kuhusiana na serikali,
11.1, 36.1

Bila Mlinzi, 57.10–11, 57.16,
58.6, 58.9, 58.12, 58.17, 59.2,
59.16–17. ’pia tazama uhusiano kati ya Nyumba ya Hakiya Ulimwengu na Mlinzi

Mlinzi wa Ulinzi, 10.1, 62.1, 76.3
nafasi katikati ya mistari, 3.1, 56.1, 57.3, 58.2,
59.12–14, 76.5, 76.8–9
mkuu wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu,
11.1, 57.11, 58.5, 59.7 jukumu la, 57.11–13, 58.4, 59.7,
62.2, 63.1, 74.1, 86.3

pia tazama uhusiano kati ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Mlinzi; Shoghi Effendi, urithi wa muongozo wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu,
13.1, 27.2, 57.6, 57.14–15, 58.3,
58.15, 59.15, 71.5, 71.9, 78.1, 79.1,
81.1, 84.1, 86.7, 86.10

Mikono wa Hoja ya Mungu, 38.1, 57.4–5,
57.7, 58.2, 58.17, 62.1–2, 76.6–7, 76.19
Mkuu wa Imani, 52.2, 62.2, 63.2, 70.11,
76.3–4, 76.17, 86.3, 86.5 heresy, 18.1, 34.4, 86.8

isiyokosea, 21.1, 45.1, 77.4
iliyojaaliwa, 21.2–3, 86.2, 86.6–8, 86.10 umuhimu, 21.1, 21.4
wa Mlinzi, 59.5, 63.1, 74.1, 77.3,
85.1, 86.5, 86.7
Mabaraza ya Kitaifa na ya mahali hayana ubia katika, 59.17
wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 86.1;
maana ya/kidokezi cha, 10.1, 17.1, 19.2,
57.8, 58.7, 59.5, 74.1, 76.21, 77.2,
86.2; na Habari inazozipokea,
72.1, 86.6; siyo mjumbe binafsi,
86.2; siyo juu ya mtu binafsi kuweka kikomo/mipaka,
77.3, 86.5; ahadi ya, 5.1, 10.1,
19.3, 39.1, 58.7, 58.16, 59.17, 77.2,
85.1, 86.2, 86.6, 86.9; mawanda ya/eneo la/nafasi ya/uwezo wa,
77.2, 85.1, 86.5; uwanja/fani/eneo la utendaji wa kisheria, kuhusiana na,
58.6, 59.17; bila Mlinzi,
57.10, 58.4, 58.6, 59.6

kuvuviwa na Mungu, 5.1, 8.2, 19.2–3, 26.1,
39.1, 58.7, 65.4, 75.1, 86.2
Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa, 47.1, 57.2–3,
70.11, 76.14, 76.16, 76.19
Mahakama ya Kibahá'í ya Kimataifa, 76.12–13, 76.16 fasiri, 40.1, 57.12–13, 58.4, 58.8,
58.13, 59.5, 59.7, 59.15, 63.2, 68.1,
70.9, 71.7, 74.1
tofauti kutoka ufafanuzi, 57.13, 75.1 tofauti kutoka fasiri katika dini zingine, 65.1–2, 68.1
binafsi, 19.4, 58.7, 58.11, 58.13, 65.1, 65.3, 68.1, 71.3–4, 77.1, 77.4

Kitáb-i-'Ahd, 34.3, 59.15, 86.8
Kitáb-i-Aqdas, 8.1, 32.1, 32.4, 33.1, 38.1,
38.5, 39.1, 40.1, 57.11, 58.16, 59.4,
59.6, 59.13, 59.15, 60.1, 67.1, 76.5, 86.2
as Hati ya ustaarabu wa siku zijazo wa ulimwengu, 23.1
sheria za, 37.1, 39.1, 40.1, 60.1

ujifunzaji mambo yaliyofasiriwa/ yaliyochukuliwa/katwa/ondolewa ya, kutokuwa na mamlaka vinginevyo imeidhinishwa, 19.4, 58.7, 77.1
views of, 65.3, 71.4, 76.7
ujifunzaji, utangazaji wa, 71.6–7, 78.1, 79.1 sheria ya Nyumba ya Haki ya Ulimwngu, 49.1, 53.1, 58.7–8, 59.5, 59.8, 66.1, 68.1–2
tofauti kutoka fasiri, 40.1,
58.4, 65.1, 65.4, 75.1 tofauti kutoka sheria katika dini zingine, 19.4, 58.7, 65.1, 65.4, 68.1

na ufafanuzi, 75.1 kiasi katika, 68.1
mchakato wa, 39.1, 57.12, 58.6, 59.10, 63.2, 72.1, 85.2, 86.2, 86.6
Uwanja/fani/eneo la/, 38.4, 57.10, 58.6, 59.2, 59.16–17
Sheriandogo ndogo, 11.1, 17.1, 20.1, 39.1,
40.1, 44.1, 53.1, 57.8, 57.11, 57.13,
58.4, 59.5, 59.16, 60.1, 63.2, 72.1,
80.1, 86.2–3; mbinu za kufanya,
65.4, 68.1; mahitaji ya wakati,
12.2, 19.1, 53.1, 58.7; hekima za,
19.1, 19.4, 35.1, 46.1, 57.13, 58.7

upevukaji wa jamii ya binadamu, 68.1 ujumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 23.1, 43.1
ufukuzaji kutoka, 11.1, 57.16, 58.17
sifa kwa ajili ya, 11.1
wanawake na, 15.2, 83.1–2, 87.1
unyofu wa kimaadili kama hitaji la wawakilishi waliochaguliwa, 41.1–2

Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa yameteuliwa kama Nyumba ya pili ya Haki, 11.1, 26.1, 29.3, 32.1, 33.3 wachaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 29.3, 54.1, 76.13
Nguzo za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 33.1, 50.1

utiifu kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 8.2, 10.1, 12.1, 13.1, 14.1,
16.1, 17.1, 19.2–3, 20.1, 57.8, 58.7,
58.15, 71.9, 76.21, 77.2–3, 86.2

ulindwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Mungu, 17.1, 19.2–3, 58.7, 59.5,
85.1, 86.2, 86.6

uhusiano baina ya Nyumba ya Haki ya

Ulimwengu na Mlinzi, 32.4,
38.3, 57.11, 58.4, 58.6, 59.5, 63.2,
74.1
Kuhusiana na, 40.1, 57.11–12, 58.4–6,
59.7–8
kutotenganika kwa, 38.3, 58.9, 86.4
pia tazama Mlinzi na Ulinzi, mkuu wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu
jukumu la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, 53.1, 66.1, 77.2
hutenda kufuatana na mahitaji ya wakati, 8.2, 12.2, 19.1, 35.1, 53.1,
57.11, 57.13, 57.15, 58.7, 68.1,
72.1, 80.1, 86.8
mambo ya watu, 8.1, 9.1 raghba za watu, 6.1
masuala ya nchi, 8.2, 36.1, 67.1–2
ulinzi: wa Imani, 58.8, 59.6, 72.1,
76.17; wa watu, 2.1, 6.1, 7.1 uhifadhi wa hadhi ya binadamu, 7.1, 53.1 uhifadhi wa uadilifu na umoja wa Imani, 51.1, 52.2, 57.13, 58.16

uhifadhi wa dini, 9.1
shared with the Guardian: 34.1, 57.11,
58.8, 58.17, 62.2, 63.2, 76.17;
utumikaji wa Maandiko yaliyofunuliwa,
57.13, 63.2, 72.1, 86.4; udumishwaji wa uadilifu na unyumbulikaji wa Mafundisho, 38.3, 51.1, 58.8, 63.2,
72.1, 86.4, 86.8; uhifadhi,
Ulinzi, na utangazaji wa Imani, 53.1,
58.8, 58.16–17, 72.1,
86.8; ulindaji wa umoja wa waumini,
38.3, 58.8, 58.16, 63.2,
72.1, 86.4, 86.8 ufunzaji wa watu, 7.1 ujengaji wa mataifa, 7.1

wanazuoni, 19.4, 58.7, 71.1, 71.3,
77.1. 'pia tazama asasi za mafunzo ya kisayansi na kijamii, 33.3, 42.1,
71.6
Shoghi Effendi
Hakuwa na ufahamu wa awali wa kuteuliwa kama Mlinzi, 76.3
kufariki kwa, 58.15, 59.14, 76.5, 76.8,
76.18–19
urithi wa madaraka wa, 52.2, 56.1,
57.3, 58.2,
58.17, 76.6–8, 76.11, 76.19 agano la,
58.2–3
Nyaraka za Mpango Mtakatifu, 64.1
Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá, 27.2,
29.1, 29.3, 33.3, 34.3, 38.2, 38.5,
49.1, 54.1, 57.3, 57.8–9, 57.14–15,
58.2, 59.4, 59.15, 59.18, 71.7–8,
76.3–7, 76.10, 76.19, 86.5
kama Hati ya Utaratibu wa Utawala,
71.9
maana kamili ya, liyofunuliwa kwa muda mrefu,
27.2, 57.15
mafumbo na kweli za Ufalme uliomo ndani, 25.1
wanawake, 15.1–2, 83.1–2, 87.1
Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh, 1.1 waumini wanaitwa kuuchukua, 27.2,
50.1, 57.14
imani kwa muda na muongozo wa kupata uelewa wa, 27.2, 57.15, 58.3,
81.1 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu: kama taji la asasi za, 50.1; kamaa kilele cha chemchemi ya, 33.1; katika nafasi kufanya kila kiwezekanacho kuanzisha,
57.13 mizania ya ulimwengu imepinduliwa na, 1.1 ibada, vitendo vya, 8.2, 67.1

ISBN 978-9976-5251-9-9